**Shabaha ya Mungu tangu mwanzo:**


Mwanadamu alitenda dhambi
Mungu aliahidi Mtu atakayemponda kichwa Shetani (Mwanzo 3:15).

Mwanadamu alizidi kupotea katika dhambi (Mw 6:5)
Mungu alituma gharika, lakini waliookolewa ni Nuhu na familia yake (Mwanzo 12:1).
Kwa mara nyingine mwanadamu alianguka katika dhambi na kuabudu sanamu. Ili kuhifadhi uzao ambao kwa huo Mwokozi wa binadamu angezaliwa, Ibrahimu alichaguliwa kama baba wa taifa jipya, chini ya sheria ya Mungu ya mpito (Mw 12:1).
Dhambi iliendelea kukua, lakini Mungu aliendelea kuandaa ujio wa Mwokozi katika ulimwengu akiwabakiza taifa la Israeli tena na tena kwa uweza na kuingilia kati kwa Malaika wa Bwana (Kutoka 33:2; Isaya 63:9).

Katika utimilifu wa wakati, Mwokozi alizaliwa (Gal 4:4). Alifanya kazi aliyokuja kuifanya, alikufa kwa ajili ya dhambi za binadamu, na alishinda mauti, akawapa binadamu Injili ya wokovu (1 Wakorintho 15:3,4).
Halafu kwa kanisa, ndugu zake, akasema, “Enendeni ulimwenguni pote mkahubiri Injili kwa kila kiumbe…” (Marko 16:15,16).

**Mikono yetu imeaminiwa**
**kwa kazi yote ya Mungu!**
**Je, tunaitimiza au inakufa pamoja nasi?**

SAUTI YA KWELI KIMATAIFA




TOLEO LA 91

# SAUTI YA KWELI KIMATAIFA

(THE VOICE OF TRUTH INTERNATIONAL)
VOLUME 91

Kitabu hiki kinatolewa bure na Kanisa la Kristo
(This book is given for free by the Church of Christ)



# Kama Hujawahi Kamwe

Mary Kelly Oler

Kama hujawahi kamwe kuhisi furaha
Ya kushiriki kupotea kwa ndugu;
Kama mikono yako mwenyewe haina nguvu
Ya kubeba msalaba wa mwingine;

Kama kamwe hujawahi kuleta tabasamu
Katika uso uliochafuka kwa machozi na kuvumilia;
Kama mikono yako mwenyewe haikushikilia
Taa wakati njia ilipofifia;

Kama kamwe hukuwahi kumwambia mtu
Juu ya maisha bora ya baadaye,
Basi umetembea katika njia isiyojulikana
Kwa Mwanaume wa Galilaya!

## Majibu ya Chemshabongo

### Tafuta Aya (ukurasa wa 42)

1. Zinaa
2. Mumewe / mkewe
3. Faragha kwa kusali
4. Wasioe kama Paulo
5. Ushauri binafsi
6. Kuwaokoa
7. Kuepuka uasherati
8. Kuoa, kuwaka
9. Kuishi nao
10. Mwache aondoke
11. Amani

### Mwokoteza Mawindo (ukurasa wa 109)

Majibu:

1. "kwa kabila kumi na mbili waliotawanyika" (Wakristo wa Kiyahudi) 1:1
2. Furaha 1:2
3. "hauzuii ulimi wake" 1:26
4. Huruma 2:13
5. Ibrahimu 2:23
6. Farasi, merikebu 3:3-4
7. Wanyeyekevu 4:6
8. Mvuke (ukungu) 4:14
9. "kuomba kwake mwenye haki kwa faa sana, akiomba kwa bidii" 5:16
10. Ibrahimu, Rahabu, Ayubu, Eliya
    Yakobo 2:21-24; 2:25; 5:11; 5:17-18

# Sauti ya Kweli Kimataifa
## (The Voice of Truth International)

Toleo la 91 (Volume 91)

Tafsiri na uhariri
(Translation and Proof reading)
**P e t e r   K a m a t u l a**
Mshirika wa Kanisa la Kristo, mwalimu na mhubiri wa Injili.
(A member of the church of Crist, a Bible teacher and preacher)

Na (and),

**S h a d r a c k  S. M s a m b a z a**
Mhubiri pacha wa Kanisa la Kristo – Kisongo.
(Pulpit minister at Kisongo Church of Christ and Bible teacher)

Nakala hii kwa lugha ya Kiswahili imetolewa na ***Swahili Gospel Team*** **(SGT),** na kudhaminiwa na ***World Evangelism Team,*** chini ya **Kanisa la Kristo.**

**Mawasiliano:**

+255 (0) 764 792 979
+255 (0) 784 880 470
+255 (0) 765 098 981
Kisongo, Arusha, Tanzania

Ubunifu na Mpangilio
(Design and Layout)

**S h a d r a c k   S.  M s a m b a z a**

**Kitabu hiki kinatolewa bure na Kanisa la Kristo**
**(This book is given for free by the Church of Christ)**

**"…makanisa yote ya Kristo yawasalimu"**
**(Warumi 16:16)**

**JINSI YA KUJIFUNZA**
- Jua nani aliongea
- Aliambiwa nani
- Liliongelewa lini
- Kwanini liliongelewa

# Biblia - "Mungu Amesema"

**Waebrania 1:1-2**


**JINSI YA KUELEWA**
- Jifunze kwa ajili yako
- Soma muktadha
- Unganisha maandiko yote
- Amini kinachosemwa

**AGANO LA KALE**
**Vitabu 39**

**AGANO JIPYA**
**Vitabu 27**

**ALISEMA ZAMANI**
**Na baba zetu katika manabii**

**MWISHO WA SIKU HIZI**
**Amesema na sisi katika Mwana**




**DINI YA KIFAMILIA**
1. Sheria bila kuandikwa
2. Mungu aliongea kwa njia ya ndoto, maono, malaika.
3. Kuhani baba
4. Dhabihu ya wanyama
5. Madhabahu ya mawe

**AHADI YA KRISTO**
1. Hawa....................Mw 3:15
2. Shemu.................Mw 9:27
3. Ibrahimu...........Mw 12:1-2
4. Isaka..................Mw 17:21
5. Yakobo..............Mw 28:14
6. Yuda..................Mw 49:10

**DINI YA KITAIFA**
1. Sheria ya Musa
2. Mungu aliongea kwa njia ya Musa na manabii
3. Ukuhani wa Kilawi
4. Dhabihu ya wanyama
5. Hema ya kukutania na Hekalu

**UNABII KUHUSU KRISTO**
1. Wa Daudi......................Zab. 89:34-47
2. Wa bikira.........................Isa. 7:13-14
3. Bethlehemu..........................Mika 5:2
4. Usaliti...................................Zab. 41:9
5. Kusulibiwa..........................Zab. 22:16
6. Kufufuka............................Zab. 16:10

**SHERIA YA MUSA**
1. Musa mjumbe...............................................Gal. 3:9
2. Damu ya Wanyama...............................Ebr.8:18-20
3. Kwa taifa la Israeli..................................Kut. 20:1-2
4. Katika mbao za mawe.............................Kut. 24:12
5. Haikukamilisha neno..................................Ebr. 7:19
6. Iliingizwa kwa sababu ya makosa........Gal. 3:16-19
7. Torati imekuwa kiongozi.....................Gal. 3:23-24
8. Kivuli cha mambo yajayo...................Kolo. 2:16-17
9. Agano la Kale............................................Ebr. 8:6-9
10. Hatupo chini ya sheria............................Rum. 6:14
11. Sheria iligongomewa msalabani........Kolo. 2:14-16
12. Amri 10, Sheria ziliondolewa.............2 Kor. 3:6-18
13. Tuliifia sheria ya kale............................Rum. 7:1-4
14. Bila sheria...............................................1 Kor. 9:21
15. Yaliandikwa ili kutufundisha.................Rum. 15:4

**SHERIA YA KRISTO**
1. Kristo mjumbe wetu.............................Ebr. 9:15-17
2. Damu ya Kristo.....................................Ebr.9:11-14
3. Kwa mataifa yote.................................Mt. 28:19-20
4. Katika vibao vya mioyo..............................2 Kor 3:3
5. Amewakamilisha, wanaotakaswa......Ebr. 10:14-17
6. Hata aje huyo mzao..................................Gal. 3:19
7. Kutuleta kwa Kristo..............................Gal. 3:23-24
8. Mwili ni wa Kristo.....................................Kolo. 2:17
9. Agano Jipya............................................Ebr. 8:10-13
10. Tupo chini ya Neema............................Yohana 1:17
11. Yesu mwanzilishi wa sheria mpya..........Ebr. 12:1-2
12. Amri za Bwana.......................................1 Kor. 14:37
13. Mali ya Kristo..............................................Rum. 7:4
14. Chini ya sheria ya Kristo..........................1 Kor. 9:21
15. Msikieni Kristo katika mambo yote..........Mdo 3:22

**DINI YA ULIMWENGU**
1. Injili ya Kristo
2. Mungu ananena kwa njia ya Kristo na kuthibitishwa na mitume
3. Kristo Kuhani wetu Mkuu
4. Kristo alisulibiwa
5. Kanisa Mwili wa Kristo

**UTIMILIFU**

| AHADI | UNABII |
|---|---|
| 1. Gal. 4:4 | 1. Mt. 1:1 |
| 2. Luka 3:36 | 2. Luka 3:27 |
| 3. Gal. 3:16 | 3. Luka 2:4-7 |
| 4. Ebr. 11:18 | 4. Yohana 13:18 |
| 5. Gal. 4:28 | 5. Yohana 19:18 |
| 6. Ebr. 7:14 | 6. Mdo 2:31 |

Chati za Biblia za Barnes

# MIFANO YA WAONGOFU

| | | SIKIA INJILI | AMINI IMANI | TUBU DHAMBI | MKIRI KRISTO | UBATIZO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SIKU YA PENTEKOSTE<br>MDO 2:36 – 42 | SIKIA<br>2:37 | | TOBA<br>2:37-38 | | UBATIZO<br>2:38-41 |
| 2 | WASAMARIA<br>MDO 8:5 – 13 | SIKIA<br>8:6 | IMANI<br>8:12 | | | UBATIZO<br>8:12 |
| 3 | SIMONI<br>MDO 8:13 | SIKIA<br>8:6 | IMANI<br>8:13 | | | UBATIZO<br>8:13 |
| 4 | TOWASHI WA ETHIOPIA<br>MDO 8:36 - 41 | SIKIA<br>8:35 | | | KUKIRI<br>8:37 | UBATIZO<br>8:38 |
| 5 | SAULI – (PAULO)<br>MDO 9:14; 22:6-16; 26:12-19 | SIKIA<br>22:16 | | | | UBATIZO<br>8:18 |
| 6 | KORNELIO<br>MDO 10:25 – 48 | SIKIA<br>10:33 | IMANI<br>10:43 | | | UBATIZO<br>10:48 |
| 7 | LIDIA<br>MDO 16:13 – 15 | SIKIA<br>16:13-14 | IMANI<br>16:14 | | | UBATIZO<br>16:15 |
| 8 | MLINZI WA GEREZA<br>MDO 16:25 – 31 | SIKIA<br>16:32 | IMANI<br>16:31 | | | UBATIZO<br>18:33 |
| 9 | WAKORINTHO<br>MDO 18:8 | SIKIA<br>18:8 | IMANI<br>18:8 | | | UBATIZO<br>18:8 |
| 10 | WANAUME 12 WA EFESO<br>MDO 19:1 - 7 | SIKIA<br>18:5 | | | | UBATIZO<br>19:5 |
| | MAHUBIRI<br>WARUMI 10:17; WAGALATIA 1:6-9 | SIKIA<br>Marko 4:23<br>Mdo 10:22 | IMANI<br>Ebr. 11:6<br>Ebr. 5:8-9 | TOBA<br>Luka 13:1, 5<br>MDO 2:38 | KIRI<br>Warumi 10:10<br>Mt. 10:32-33 | UBATIZO<br>1 Pet. 3:21 |

# Sauti ya Kweli Kimataifa


## Wafanyakazi:

*Mhariri:* Louis Rushmore
*Mhariri Mshirika:* Jerry Bates
*Mhariri Mstaafu:* Byron Nichols
*Mhariri Mwanzilishi:* J.C. Choate
*Mpangilio:* Betty Burton Choate
Barbara Oliver
*Meneja:* Paula Bates
*Washauri wa Kompyuta:* Bradley S. Choate
Dennis Larson

## Waandishi:

**George Akpabli**
**Felix O. Aniamalu**
**Rex Banks**
**Wayne Barrier**
**Paula Bates**
**Roy Beasley**
**Mike Benson**
**Ron Bryant**
**Charles Burch**
**Kyle Butt**
**Frank Chesser**
**Betty B. Choate**
**Glenn Colley**
**Lance Cordle**
**Sunny David**
**Hans Dederscheck**
**David Deffenbaugh**
**Clarence DeLoach, Jr.**
**Bill Dillon**
**Bobby G. Dockery**
**Hershel Dyer**
**Earl Edwards**
**Demar Elam**
**Raymond Elliott**
**Reuben Emperado**
**David Everson**
**Royce Frederick**
**E. Claude Gardner**
**Gary C. Ham**
**Jack Harriman**
**Parker Henderson**
**Gordon Hogan**
**Wayne Jackson**
**Ancil Jenkins**
**Jeff Jenkins**
**John Kachelman, Jr.**
**Dayton Keesee**
**Dalton Key**
**Michael L. King**
**J. Randal Matheny**
**Cecil May, Jr.**
**Wes McAdams**
**Colin McKee**
**Stan Mitchell**
**Kevin L. Moore**
**Owen D. Olbricht**
**David Pharr**
**Neal Pollard**
**Mark Posey**
**Steve Reeves**
**Martha Rushmore**
**Rebecca Rushmore**
**David A. Sargent**
**David Tarbet**
**J.J. Turner**
**Ken Tyler**
**Allen Webster**
**R.H. Tex Williams**



# JARIBIO LA KUSIKITISHA

Louis Rushmore

Mwenyezi Mungu aliumba Jeshi la Malaika (Mwanzo 2:1, Isaya 45:12, Nehemia 9:6, Wakolosai 1:16) na wengi wao walimuasi Muumba wao (2 Petro 2:4, Yuda 6, Mathayo 25:41, Ufunuo 12:9). Kwa hiyo, inaweza kuonekana kuwa kuunda Malaika ilikuwa jaribio la kusikitisha.

Mungu aliumba wanadamu (Mwanzo 1:26-27), na wanandoa wa kwanza (Mwanzo 2:18,24), pamoja na sheria (Warumi 3:10, 23), waliasi maagizo ya Mungu yaliyotolewa kwao. Katika hali hiyo, binadamu hawakustahili kuwa katika uwepo wa Mungu Mtakatifu (mwanzo 3:22-24, Isaya 59:1-3, 2 Wathesalonike 1:9). Kumuumba mwanadamu, pia inaonekana kuwa ***jaribio la kusikitisha***.

Hatimaye, katika njia ya kuwaadhibu wanandamu waliopotea, Mungu, katika matukio zaidi ya moja aliubadilisha Ulimwengu uliouumba, ambao aliwaweka wanadamu (mwanzo 3:15-19, 7:11-12, 20-23, 11:1-9). Vitu vyote ambayo Mungu aliviumba, ambavyo alivifanya kuwa vyema (Mwanzo 1:4,10,12,18,21,25) na vyema sana (Mwanzo 1:31), vikawa chini ya kiwango kuliko vilivyokuwa hapo kwanza. Ulimwengu na kila ndani yake vinakaribia mwisho na kuchakaa taratibu. Hata ulimwengu ulioumbwa pamoja na kitu kingine chochote ambacho Mungu alikiumba pasipo chanzo (Waebrania 11:3) inaonekana kuwa ni sampuli za ***jaribio la kusikitisha.***

Mungu alipowapa malaika na wanadamu utashi, aliwapa uwezo wa kufanya uchaguzi wao wenyewe (Yoshua 24:15, 1Wafalme 18:21)

kwa bahati mbaya, baadhi ya malaika walichagua kumpinga Mungu. Vivyo hivyo kinachosikitisha, kila binadamu ambaye amepata uwezo wa kupambanua kati ya mema na mabaya, wakati mmoja au mwingine katika maisha yake amechagua kutomtii Mungu. Sio tu kwamba ulimwengu unachakaa, mara nyingi wanadamu wanaharakisha kuchakaa kwake kupitia uvunaji wa rasilimali za ulimwengu pasipo kurudishia (kupanda upya) ikiwemo na uchafuzi wa mazingira, hewa na maji. Hili ni ***jaribio la kusikitisha*** ambalo linatokana na kushindwa kwa malaika na binadamu, kujumlisha uharibifu wa sayari yetu.

Maana ya neno "**kusikitisha**" ni hali ya kutokuwa na furaha (au kuwa na huzuni). Neno "**jaribio**" linamaanisha "kipimo kinachopitia mchakato wa ugunduzi wa jambo au kitu fulani". Hatma ya anguko la malaika, anguko la mwanadamu na anguko la ulimwengu, inaonekana kutokana na mtazamo wa kibinadamu wa kutokuwa na furaha uliotokana na uchunguzi ili kugundua mambo yasiyojulikana. Hata hivyo, kwa mtazamo wa kimungu, hilo si jambo sahihi.

Mungu alipokuwa akiumba malaika, wanadamu na Ulimwengu mzima hakuwa akifanya majaribio. Zaidi, Mungu kupitia uumbaji haukuwa anajaribu kugundua kitu chochote asichokijua ili kuanzisha nadharia. Kupitia ufahamu wa kimungu (Isaya 42:9;46:10), Mungu alijua vizuri nini ambacho kingetokea kutoka katika uumbaji wake, hata hivyo, alichagua kuendelea na uumbaji. Zaidi ya hayo, Mungu aliweka mpango wa ukombozi ambapo kwa mara nyingine wanadamu waweze kupata nafasi ya kukaribia mbele za uwepo wa Mungu Mtakatifu (Tito 1:2-3, 1Petro 1:18-20).

Labda kilele cha kile kinachoweza kuonekana kuwa ni ***jaribio la kusikitisha*** ilikuwa wakati Mungu aliyevaa mwili alipouawa na binadamu aliowaumba, licha ya kwamba Mungu alimtuma Mwanawe kuwaokoa. Inastahajabisha jinsi Bwana wetu Yesu Kristo alivyoonesha uso wa kujizuia kwa watu wasio na shukrani alipokuwa akisulibiwa pale msalabani Kalvari. Hakuyaita majeshi kumi na mawili ya malaika ili kuuharibu ulimwengu na watu (Mathayo 26:53). Upendo wa Mungu na

wa Yesu Kristo ulikuwa na nguvu kuliko uovu wa kibinadamu ili tupate fursa ya kuokolewa (Warumi 5:8-10).

Mpenzi msomaji, azimu kutokuwa sehemu *iliyoshindwa* ya ***jaribio la kusikitisha***. Ukombozi wa kibinadamu si kitu chochote isipokuwa ni ***jaribio la kusikitisha,*** sanjali na hilo, kupuuza juhudi za Mungu na dhabihu ya Yesu Kristo aliyoitoa kwa niaba yetu inafanya kuwa ni *jaribio la kuhuzunisha*. ***"Sisi je! Tutapataje kupona tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale walisikia"*** (Waebrania 2:3).



# FAMILIA YA WARAIBU

**JERRY BATES**

Kuna jeshi la wahusika wasiojulikana katika Biblia, bado muda mwingine wanakuwa ni mifano mikubwa. Mfano mmojawapo ni Stefana anayepatikana katika vifungu viwili tu (1Wakorintho 1:16, 16:15-17). Nukuu ya pili ya Biblia inasema ***“Ndugu, nawasihi mnawajua watu wa nyumbani mwa Stefana, kwamba ni malimbuko ya Akaya, nao wamejikita katika kazi ya kuwashuhudia Watakatifu”.*** Angalia Paulo alisema kuwa watu wa nyumbani mwa Stefana “walijitoa” kwa ajili ya huduma. Stefana alijitoa kwa dhati kwa Mungu na kazi yake. Inawezekana pia kusema kwamba alikuwa Mraibu, sio yeye tu, bali na watu wote wa nyumbani mwake.

Mara nyingi tunajua kuwa madawa yote ni mabaya. Umati wa watu leo hii umejiingiza katika vitu vibaya vinavyodhuru au hata vitu viovu, kama vile madawa ya kulevya, pombe, uvutaji sigara n.k. Wengi pia wangefikiria kuwa kujitolea kupindukia kwa mambo ya dini vilevile ni vibaya. Neno “Ushabiki wa kidini” limebeba dhana mbaya. Walakini, tunapojitolea kweli kweli kwa Mungu na huduma yake, uraibu ni mzuri.

Stefana hakutafuta kisingizio cha kutoshiriki katika kazi ya Bwana, wala hakutarajia wengine kufanya kazi hiyo. Hakuweza kukaa katika hali ya uvivu wakati ambapo wengine wanafanya kazi au kazi haijaisha.

Wakati mwingine watu wanaweza kusema “kazi hii hainichoshi, ninaweza kukaa na kuiangalia siku nzima”, inapokuja kwenye masuala ya dini, kauli hiyo ya kichekesho mara nyingi ni kweli. Inaonekana kuwa wengi wa washirika wa Kanisa wanaweza kukaa na kuangalia kazi ya Kanisa siku nzima, nab ado hwajishughulishi vya kutosha. Utani wa mhubiri wa zamani ni kwamba 10% ya Kanisa hufanya 90% ya kazi na inaonekana kwamba utani hauko mbali na ukweli.

Stefana hakika alikuwa sehemu ya 10%. Stefana alikuwa ni moja wapo kati ya wachache waliobatizwa na Paulo binafsi (1 Wakorintho 1:16) na nyumba yake inasemekana ndio “*malimbuko”* ya kazi yake (Paulo) kule Akaya. Familia yake walitambua kuwa imani hiyo pasipo kazi (matendo) imekufa (Yakobo 2:20). Walielewa juu ya vipaumbele. Wengi wanakusudia kumtumikia Mungu, lakini vitu vingine vinaingilia kati. Walakini, mtu anapokuwa mraibu au kujitoa kwa jambo fulani,



hakuna kinachoweza kumsitisha. Mraibu wa dawa za kulevya atafanya karibu kila kitu kupata dawa yake. Stefana alikuwa ni sehemu ya Kanisa huko Korintho, Kanisa lenye matatizo mengi. Kusanyiko halikujishughulisha vya kutosha kwa ajili ya Paulo, lakini Stefana na wengine wawili walifanya kazi ambayo Kanisa lote lilipaswa kufanya (1 Wakorintho 16:17). Shauku yao ya kumsaidia Paulo na huduma yake ilikuwa kupaumbele chao cha kwanza. Kanisa ni la ngapi katika orodha ya vipaumbele vyako?

Uraibu unakulazimisha kufanya kitu. Inakuwa kitu kinachokutawala. waraibu mara nyingi husema wanataka kuacha, lakini uraibu wao unawathibiti. Vivyo hivyo, upendo wa Kristo unapaswa kututawala. ***"Maana, upendo wa Kristo watubidiisha, maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote***" (2 Wakorintho 5:14). Paulo alisema alikuwa mdaiwa/mdeni kwa Wagiriki, kwa wasio Wayunani, kwa wenye hekima na wasio na hekima (Warumi 1:14). Tunapaswa kuongozwa na Roho. ***"Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi, bali mjazwe na Roho"*** (Waefeso 5:18). Tunapojiweka chini ya uongozi wa Roho, Neno Lake, ndipo tutalazimika kufanya vitu vinavyoweza kuonekana ujinga kwa ulimwengu. Tutakuwa ni watu tuliojikita zaidi katika kazi ya Bwana.

Mungu na Kanisa lake wanahitaji watu wengi zaidi wa kujitoa katika huduma. Mraibu hamsubiri mtu amsaidie ili kutosheleza uraibu wake. Anatafuta yeye mwenyewe. Hivyo, mtu aliyejitoa kwa huduma ya Mungu hasubiri kuombwa kufanya kitu. Mungu alijitolea. Mungu kwa hiari alimtoa Mwanawe Msalabani. Yesu kwa hiari alitoa maisha yake. Wakati Mungu alipohitaji Mjumbe au Nabii, Isaya alisema ***"mimi hapa, nitume mimi".*** Daudi alijitoa kupigana na Goliathi. Nehemia alijitolea kurudi na kujenga ukuta wa Yerusalemu. Watu hawa wote, na wengine pia, walilichukua hili juu yao kufanya yale waliyojua kuwa ni wajibu wao. Walilichukulia hili kuwa ni fursa na hawakuiyumbisha kazi. Bado, Wakristo wengi hawafanyi jambo lolote isipokuwa wameambiwa kufanya, na hata wakiambiwa wanafanya kana kwamba

wanakufanyia msaada. Tunahitaji kukumbuka kuwa hatumfanyii kazi mtu ye yote, badala yake, tunamfanyia Mungu.

Kazi ya Kanisa ni kwa kila mshirika si kwa "watu fulani tu" (ni kwa mtu ye yote yule). Wasiookoka daima wanahitaji kufundishwa. Wagonjwa, waombolezaji na wazee daima wanahitaji msaada na kutiwa moyo. Lazima tufanye wajibu wetu bila kungojea kupanga "programu". Tunaweza kuwa na uhakika ya kwamba Mungu atatupa thawabu. ***"Maana Mungu si dhalimu hata aisahau kazi yenu, na pendo lile mlilolidhihirisha kwa jina lake, kwa kuwa mmewahudumia Watakatifu, na hata hivi sasa mngali mkiwahudumia"*** (Waebrania 6:10). Alvin York, shujaa mkuu wa kijeshi, wa vita kuu ya kwanza ya dunia (WWI), aliwai kuulizwa kwa nini alifanya matendo ya ushujaa aliyoyafanya, alisema tu katika kiingereza chake cha Mountain, Tennesse "nikaona wajibu wangu na kuufanya". Je, unaweza kutoa kauli hiyo hiyo kuhusu kazi katika kusanyika lako?.



# AMANI YA KWELI

**Byron Nichols**

Shauku ya kuwa na amani ni tamaa ya ulimwengu kama watu ulimwenguni pote wanavyoomba amani na kuitamani. Biblia inayo mengi ya kuzungumza kuhusu amani, basi acha tuangalie pamoja baadhi ya Maandiko jinsi yanavyofunua kuhusu somo hili la muhimu sana.

**Biblia inasema Pambana au Tafuta Amani**

Zaburi 34:14 inatuambia ***"uache mabaya ukatende mema, utafute amani ukaifuatie"***. Msisitizo huu unarudiwa kwa Kanisa katika Agano Jipya kama Paulo alivyohimiza ***"Basi kama ni hivyo, na mfuate mambo ya amani na mambo yafaayo kwa kujengana"*** (Warumi 14:19). Paulo alitambua thamani ya amani kama alivyoonesha kwa kiwango ambacho juhudi zetu zinavyopaswa kuwa ili tuwe na amani. Angalia alichoandika Paulo katika Warumi 12:18 ***"kama yamkini, kwa upande wenu, mkae katika amani na watu wote"*** alikuwa anazungumzia nini? Alikuwa anasema "Amani ni ya muhimu na ya thamani kana kwamba kila Mkristo lazima afanye kazi kwa bidii ili amani iwepo ambayo kama itakosekana, haiwezi kuwa kwa sababu ya ukosefu wa jitihada za mtu.

Paulo aliendeleza msisitizo huu wakati akihitimisha katika 2 Wakorintho 13:11 ***"hatimaye ndugu, kwaherini, mtimilike, mfarijike, nieni mamoja, mkae katika amani, na Mungu wa upendo na amani atakuwa pamoja nanyi".*** Njia mojawapo ya kugundua thamani ya kitu fulani ni kiwango cha jitihada inayohitajika ili kukipata. Hivyo, tunaweza kuona kwamba amani ina thamani kubwa sana iliyowekwa na Maandiko.

## Kwa hiyo, Amani ni muhimu, lakini Chanzo chake ni nini; Tunawezaje kuipata?

Tunasoma katika Luka 2 juu ya kuzaliwa kwa Yesu, inafurahisha kuona kwamba umati mkubwa wa Jeshi la Mbinguni likimsifu Mungu na kusema ***"Atukuzwe Mungu juu Mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu waliowaridhia"*** (mstari wa 14). Hakika ijulikane kuwa kuja kwake Kristo kulihusishwa kwa karibu na amani. Luka pia aliandika kitabu cha Matendo ya mitume, na katika sura ya 10:36 alisema kwamba Amani inahubiriwa kupitia Yesu Kristo. Hivyo, pasipo Kristo, hakuna amani ya kweli. Katika Waefeso 2:14 Paulo alithibitisha kwa uwazi kwamba Yesu ni "Amani yetu", kwa kuifanya amani ipatikane kwa kuimwaga damu Msalabani. Kwa kufanya hivyo aliharibu utengano wa Wayahudi na watu wa Mataifa, akawafanya kuwa mmoja. Hebu tuangalie maoni ya Paulo katika Wakolosai 1:19-20; "***Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae; na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni."*** Kwa hiyo, tunaona kwamba amani inatokana na dhabihu ya upatanisho ya Mwana wa Mungu kwa ajili ya dhambi za ulimwengu mzima!

## Hatimaye Tumefika katika Amani Kuu – Amani ya moyo – Amani ya Kweli.

Kama ambavyo amani ya dunia inavyothaminiwa, bado amani iliyo kuu ni ile tunayoweza kuwa nayo ndani yetu kwa njia ya imani kwa Mungu na uhusiano sahihi tulionao pamoja naye. Si amani wala machafuko katika taifa letu au katika ulimwengu kwa jumla, inayoamua ikiwa tuna amani ya kibinafsi au la! Ikiwa kitu chochote, hata uwepo wa machafuko yanayotuznguka ambayo yanaweza kumsababisha mtoto wa Mungu mwaminifu kuuthamini uhusiano wake na Mungu kwa kiwango cha juu ni ukweli kwamba hakuna jambo wala mtu atakayeweza kuondoa amani kutoka kwake.

Wale waliojitoa kumtumikia Yesu wamebarikiwa na maneno yaliyo katika Warumi 8:6 ***“Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani”*** Paulo alisema kwa wote wanaojitahidi kumtumikia Bwana leo, ***“Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu, ndiyo mliyoitiwa katika mwilimmoja; tena iweni wote wa shukrani”*** (Wakolosai 3:15).

Kwa bahati mbaya, inawezekana kwetu kuwa amani bila kujua kwamba hiyo ni ya kupotosha na ni ya muda tu. Tunaweza kujiidanganya kwa kuamini kwamba tutapata amani ya milele ya mbinguni kwa sababu tu **tunatamani** matokeo hayo. Pamoja na hayo, tunasoma Agano jipya lote juu ya watu wazuri ambao walikuwa wanajaribu kwa dhati kumtumikia Bwana, lakini hawakuwa sehemu ya Kanisa ambalo Yesu aliahidi kulijenga (Mathayo 16:18). Baada ya kufundishwa, wengi walitii matakwa ya Kristo na **kumwamini** yeye kama Mwana wa Mungu (Yohana 8:24) **walitubu** dhambi zao (Matendo 2:38), **walikiri** imani yao katika Kristo, **kubatizwa** kwa kuzamishwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao (Matendo 2:38, 1 Petro 3:21) na kutumika kwa **uaminifu** mpaka kufa. (Ufunuo 2:10).

Tafadhali usicheze kamari na nafsi yako na fursa yako ya amani hiyo ya milele. Mtii Bwana kama wale waliofungwa katika karne ya kwanza. **Amri na faida bado ni zilezile hata leo.**





1932 - 2008

# Kamwe Usilidunishe Kanisa

**J.C Choate**

Umewahi kusikia mtu yeyote akisema "Kanisa moja ni zuri kama linguine" au "hupaswi kuwa mshirika wa Kanisa lolote ili uokoke. Rudia tu, sala ya mwenye dhambi na utakuwa sawa?" au mbaya zaidi, Je! Umewasikia watu wenye kudunisha na kudhihaki "dini iliyopangiliwa vizuri" kama kichekesho, kwa sababu ya mgawanyiko na kuchanganyikiwa katika mafundisho na mazoea ya Ulimwengu wa kidini?

Kabla hujazama sana kupinga wazo la "Kanisa" fikiria kwa **muda: Je! Unajua kuwa Kanisa linaitwa Bibi – arusi wa Kristo?** Ndoa ni kitu kinachojulikana na kueleweka vizuri sana karibu Ulimwengu mzima. Mwanaume anamchagua mwanamke mmoja maalum ili awe bibi arusi wake. **Anamuoa**, anampa **jina lake**, anaishi kwa ajili ya ***kumlinda***, **kumpatia** mahitaji yake, **kumpenda**, na ikiwa anampenda vya kutosha, na ikiwa uhitaji utatokea, **atakufa ili kumwokoa.** Ikiwa uhitaji unawatenganisha kwa muda, wazo lake kubwa ni **kurudi kwake**.

Kama bibi arusi wa Kristo, **Kanisa la Kristo** na watoto wa muungano ni Wakristo. Kama ilivyo katika ndoa ya kiwmili, hakuna mume atakayeruhusu mke wake kuvaa jina la mwanaume mwingine. Bibi arusi, Kanisa la Kristo, anapaswa kuvaa au kuitwa kwa jina la mume wake. ***"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya Mbingu walipopewa wanadamu litupasalo sis kuokolewa kwalo"*** (Matendo 4:12. ***"Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia"*** (Matendo 11:26).

Bibi arusi anatakiwa kumpenda na kumtii mume wake. ***"Mkinipenda, mtazishika amri zangu".*** (Yohana 14:15) ufafanuzi umesisitizwa zaidi katika Wagalatia 1:8 ***"Ijapokuwa sisi, au Malaika wa Mbinguni, atawahubiri ninyi Injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe"*** Mafundisho mengi na miongozo ya imani zilizoundwa na watu huendesha makanisa waliyoyaanzisha wako katika ukiukaji wa moja kwa moja wa andiko hili.

Mahusiano ya ndoa ya kibinadamu sambamba na ndoa ya Kristo na kanisa lake yameelezwa vizuri katika Waefeso 5:22-23, ambapo upendo na utunzaji wa Kristo kwa Bibi arusi wake unafanywa kama mfano wa wanandoa na ambapo mapenzi ya Kristo kuyatoa maisha yake kwa ajili ya bibi arusi wake, kwa sababu ya upendo wake mkubwa kwa Kanisa umeelezwa. Uhusiano umewekwa kwa njia hii.

> ***"…Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji*** [ubatizo], ***katika neno*** [kwa mujibu wa maandiko] ***kwamba aweze kumsogeza kwake*** [atakuja tena, kumpokea bibi arusi wake] ***Kanisa Tukufu*** [Umoja, mwili mmoja ulioungana, sio maelfu ya madhehebu] ***lisilokuwa na doa wala kunyanzi au kitu kama hicho, lakini kwamba liwe Takatifu na lisilo na ila".***

Kutokana na ulinganifu huu kati ya Kristo na Kanisa lake, na mume na mke, tunaweza kuona kwamba kuna uhusiano maalum sana kati ya Kanisa na mume wake. Atakasirika sana ikiwa mtu yeyote atamdhihaki au kumdharau bibi arusi wake, kundi kubwa la watu ambao aliyatoa maisha yake pale msalabani kwa ajili yao. Hiyo damu inalifanya Kanisa kuwa taasisi Takatifu, inayopendwa na kuheshimiwa kama mwili wa Kiroho ambapo Kristo ni kichwa cha Kiroho cha mwili huo.

Bado, kuna wengi katika Ulimwengu wa dini wanajaribu kulidunisha Kanisa kuwa si kitu chochote zaidi ya shirika lililofanywa na wanadamu ambalo halina umuhumiu. Watakwambia kwamba sio lazima uwe mshirikawake ili kwenda Mbinguni – kuhalalisha madhehebu yote haya. Wengine wanaelezea hilo kwa kuweka madhehebu yote pamoja chini ya "Mwamvuli" mkubwa unaishia kuwa

na Kanisa ambalo tunaweza kulisoma katika Biblia. Wengine huenda kwa Yohana 15 na kusema kwamba Kristo ni mzabihu na kwamba matawi ya mzabihu huo ndio haya madhehebu tofauti ya Makanisa.

Baadhi ya Makanisa haya yanavaa majina ya waanzilishi wao; baadhi yana majina ya siku ambazo wanaabudu au baada ya imani au mazoea fulani ambayo ni ya kawaida kwao. Makanisa haya yana kila namna ya masharti ya uanachama, wanaabudu katika njia tofauti tofauti (Baadhi yao zinashikamana zaidi na burudani kuliko kumwabudu Mungu) na karibu kila kitu kinachofikirika hufundishwa na kufanywa nao. Jambo la kushangaza ni kwamba yote haya yanafanywa katika "Jina" la Kristo na kila mmoja anatarajia Bwana atoe kibali chake kwa aina nyingi za mafundisho na mazoea ya dini, wengi wao hawana msingi wowote katika maandiko, inasikitisha jinsi gani Ulimwengu unaojulikana wa Kristo kugawanyika vibaya na kuchanganyikana, kufanyia mzaha Bwana na njia yake, kupunguza umuhimu wa fundisho lake na kudharau ili sadaka yake aliyojitoa yeye mwenyewe kwa ajili ya Kanisa, kwa sababu ya njia ambayo Binadamu amebadilisha mambo na akayageuza karibu, "dini iliyopangwa haina kitu zaidi ya utani mkubwa katika mawazo ya wengi. Matokeo ya mgawanyiko mkubwa, kuchanganyikiwa na utatanishio ni kwamba idadi kubwa ya watu Ulimwenguni wamekataa dini kabisa na wamekuwa makafiri au watu wasiomwamini Mungu na maneno yake.

Walakini, hakuna kitu kuhusu rushwa ya dini iliyopangwa ni ya kuchekesha unapoacha kutambua kwamba watu wote wenye makosa ya dini watapotea kwa sababu wameongeza katika neno la Mungu au kupunguza kutoka katika neno.

> ***"Namshuhudia kila mtu ayasikiye maneno ya unabii wa kitabi hiki, mtu yeyote akiyaongeza Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu yeyote akiomba lolote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa mzima na katika ule mji Mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki"*** (Ufunuo 22:18-19).

Wale wote wanaothubutu kubadilisha ujumbe wa Mungu pia watasababisha wengine kupotea kwa sabau wafuasi wao wamedanganywa na mafundisho ya uongo, Yesu mwenyewe alionya katika Mathayo 7:21-23.

> ***"Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana atakayeingia katika Ufalme wa Mbinguni, bali ni yeye ayafanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye Mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwaba, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe, ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu".***


Wale ambao wangepata kosa pamoja na Bwana na Kanisa lake na chochote alichokifundisha ataishi kwa majuto, hakika watakufa kwa majuto na hakuna kitu cha kuchekesha katika hilo.

# *Shiriki katika Vita*

**Raymond A. Leonard**

**Tuko katika mapambano haya pamoja**
**Katika huduma ya Bwana**
**Tunapambana na nguvu ya uovu kwa kutumia**
**Neno la Mungu, upanga wa Roho.**

**Mungu ametuita katika huduma yake**
**Bendera yake kuinua juu,**
**Tunapohubiri na kufundisha Injili**
**Kwamba wenye dhambi hawatakiwi kufa.**



**Wakati tunapovaa mavazi yetu ya huduma,**
**Tumejitoa kwa Mungu,**
**Kwamba tutii amri zake**
**Na mapenzi yake tusiyavunje.**

**Kwa hiyo tunapojihusisha katika vita,**
**Ambayo Mungu ametuita kupambana,**
**Tutafanya kama watu wa heshima,**
**Kuangaza nuru ya Injili ya Kristo.**

**Hatuna mamlaka nyingine zaidi ya,**
**Nguvu zilizomo katika Neno la Mungu,**
**Ambayo ina nguvu ya kubadilisha maisha tu**
**Wakati wale wanaohitaji wanaposikia.**

**Lazima tudumu katika vita,**
**Wajibu wetu hatuwezi kuacha.**
**Tunapigania nafsi za milele,**
**Na uovu umekula kila mahali.**

**Mungu ametuweka katika vita hii,**
**Tumehusika katika njia ya haki**
**Omba ili usife moyo kamwe**
**Kwamba tunataka kuacha au kusitisha.**

### MUNGU

Unaweza kumwona Yesu ……………………Glenn Colley ………………………..24
Ukamilifu katika Kristo ……………………David Deffenbaugh …………………26


### USHAHIDI

Ndege jamii ya Kipanga ……………………Brett Petrillo ………………………….28
Ukweli wa kisayansi katika Neno lake………..David Everson ……………..32


### NENO LA MUNGU

Biblia …………………………………………… Chalres Cash …………………….......36
Kuna nini katikati?………………………Edward Anderson ……………………39


### WOKOVU

Usiende Pamoja na Mbuzi……………………Perry N. Hall……………….........45
Yatazameni Mashamba ……………….Dayton Keesee …………………………47
Kama ningekuwa na makala moja zaidi……….Bob Prichard ………………50


### KANISA

Kanisa lililoteswa …………………………..Gary C. Hampton …………………..53
Ni kweli Kanisa lina umuhimu hivyo? …………Patrick Morrison ………...56


### FUNDISHO LA KUISHI KWALO

Mpya ……………………………………...… Royce Fredrick ………………………….59
John Calvin na Neema ………………….. Wayne Jackson ………………………..61


### UKRISTO KATIKA VITENDO

Ulimwenguni pote ………………….. Paul Holland ……………………………….66
Ukimya usiowezekana ……………..John Gipson …………………………………70
Wakristo wote ni watumishi wa Bwana……….Dale Grisson ……………..72
Chapa za Yesu ……………………………….. Jim R. Everett ……………………..73
Kupanua uzio ……………………………. Olden Cook ………………………………74


### IBADA

Ibada inayokubalika ………………………John Thiesen …………………………76
Tabia nne kuelekea utoaji……………..Wade websiter …………………………79

Kunyanyua mikono iliyotakata ……………..Kevin Moore……………………..81

## MAISHA YA MKRISTO KILA SIKU

Jengo juu ya msingi wa mwamba……..Wayne Barrier ……….……………..87
Changamoto yetu ……………………..Greg Tridwell ……………….……………..89
Hayo Ndiyo Maisha……………………..Carroll Sites ……………………………..91
Shetani – Je, unamtambua………..Betty Burton Choate …………….……..93

## NYUMBA YA MKRISTO

Umuhimu wa malezi ya nyumbani…………Ferman Carpenter …………..97
Urithi bora ………………………………………. Dwight Fungua ………………...100

## MASOMO KATIKA MAANDIKO

Waefeso; Kristo na Kanisa lake …………… Jim Laws ………………….. …..103
Injili ya Marko ………………………………… David Shannon………………….107

## WAHUSIKA KATIKA BIBLIA

Jifunze kwa mtu mwema …………Maxie B. Boren ……………………………110
Mwuaji wa jitu karibia auawe……Steve Higginbotham……………………111
Shetani alikutana na ukuta wa tofali………Dalton Key ……………………..114

## MASWALI YA BIBLIA

Mungu aliwaacha kivipi? ………………..Dennis Gulledge ………………..….116
Amri kumi za Agano jipya ……………….. Russel Bell ………………………...118

## CHATI NA MIHTASARI

Nini kilichosahihi kwa Kanisa ………………… Mark N. Posey ……………….121
Kumsahau Mungu …………………………….Bobby Dockery …………………123


## HISTORIA YA KANISA

Theolojia ya marejesho ……………………Cecil May, Jr ……………………125

## VIPENGELE, MASHARTI NA VIJAZO

Kama hujawahi kamwe….Marry Kelly Oler ……(upande wa ndani wa gamba la mbele)
Biblia, Mungu amesema …………………Dannie S. Barnes …………………...3

Mifano ya wongofu ……………………….Donni S. Barnes ……………………….4
Jaribio la kusikitisha ………………….. Laws Ruskwore ………………………….6
Familia ya Waraibu …………………… Jerry Bates ………………………………..9
Amani ya kweli ……………………………. Byron Nichols ……………………….13
Kamwe usilidunishe Kanisa…………………J.C. Choate ……………………….16
Shiriki katika vita ………………… Raymond A. Leonard ……………………20
Je, ulijia……………Rebecca Rushmore……………..25,31,46,51,106,108,104
Tafuta Aya ……………………………. Jerry Bates ………………………………….42
Jipime na Biblia …………………….. Martha Rushmore ……………………….52
Wazo la haraka katika Aya ya msingi………Betty Burton Choate ……….65
Kupanda mbegu ya Ufalme …………Eddie Copper …………………………….69
Unapimaje? ……………………… Betty Burton Choate ………………………..75
Ucheshi (Mithali 17:22)……………Byron Nichols ………………………………..84
Dakika 5 za kujifunza Biblia ………….. Paula Bates …………………………102
Mwokoteza mawindo ……………… Rebecca Rushmore ……………………109
Tafuta Aya, jipime na Biblia na, Mwokoteza mawindo (majibu; upande wa ndani wa gamba la nyuma).



# Unaweza Kumwona Kristo

**Glenn Colley**

Kwamba wangine wangeona ni vigumu kumfuata Mwokozi ambaye hawakuweza kumwona imeonyeshwa katika 1 Petro 1:8 ***"Naye mwampenda, ijapokuwa hamkumwona; ambaye ijapokuwa hamwoni sasa, unamwamini; na kufurahi sana, kwa furaha isiyoneneka, yenye Utukufu.*** Anatuongoza na kututawala kwa Agano jipya, ambalo alituachia tulifuate. (Waebrania 9: 1-17).

Lakini ifahamike kwamba kuna namna ambayo tunaweza kumwona Kristo leo. Katika Matendo 9:4, Yesu alipomtokea Paulo wa Tarso alipokuwa akielekea Dameski, Alimuuliza, ***"Sauli, Sauli, mbona waniudhi?"*** Je, Sauli angewezaje kumtesa/kumuudhi Kristo? Yesu alishakufa na kufufuka kwenda kwa Baba yake Mbinguni katika Matendo 1, na bado Yesu anamuuliza Sauli kwanini **anamuudhi**. Jibu la hili ni rahisi, linapatikana katika Matendo 8:3 ambapo tunasoma ***"Sauli <u>akaliharibu Kanisa</u>, akiingia kila nyumba na kuwaburuta wanaume na wanawake na kuwatupa gerezani".*** Ukweli ni, wakati Sauli au mtu mwingine yeyote kwa jambo kama hilo, la kuumiza watu wanaovaa jina la Kristo anamuumiza Kristo.

Sisi pia tunaweza kumwona Yesu tunapowajali na kuwapenda Wakristo. Dhana itafafanuliwa katika hukumu,

***"Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia. Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu tukakunywesha? Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi, tukakuvika? Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia? Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi."*** (Mathayo 25:34 – 40)

Fundisho liko wazi sana kukosa kuuona uso wa Bwana wetu ni lazima tu tuangalie mbali kama ndugu yetu au dada yetu waliokaa karibu nasi. Aina yoyote ya ukarimu tunaoonyesha kwao inapokelewa na Kristo. Tunapoona nyuso zao, sura za ndugu zetu zikihitaji, kuna maana ambayo tunaona sura ya kupendeza ya Yesu. Haishangazi kwamba linaitwa mwili wa Kristo (Waefeso 1: 22 -23). Sisi sio marafiki wake tu, lakini sisi ndio mwili wake. Tunaweza kumwona leo, kama wimbo wa zamani unaosema, "Je, Yesu anajali? ……………Najua anajali.

**Gleen Colley ni mhubiri wa Kanisa la Kristo huko Hustsville Magharibi, Alabama, Marekani**

Kuuona uso wa Bwana wetu ni lazima tu tuangalie mbali kama ndugu yetu au dada yetu waliokaa karibu nasi. Aina yoyote ya ukarimu tunaoonesha kwao inapokewa na kristo. Tunapoona nyuso zao, sura za ndugu zetu zinahitaji, kuna maana ambayo twaona sura ya kupendeza ya Yesu.



# Ukamilifu katika Kristo

**David Deffenbaugh**

Mtu yeyote ambaye amewahi kucheza mchezo wa fumbo wa kuunganisha (picha, herufi au namba) ili kupata kipande kimoja anajua jinsi tunavyojali ukamilifu. Haijalishi vipande 499 kati ya vipande 500 viko pale na ni mahali pake. Haijalishi kwamba mtu anaweza kusema hasa picha inayotengenezwa na puzzle na anaweza kupenda uzuri wake. Ikiwa kipande kimoja kitakosekana, kutokukamilika kwake ndiko kutaonekana zaidi.

Watu wanahitaji ukamilifu pia. Ingawa miili yetu ya nyama ni mkusanyiko wa ajabu wa mifumo na mchakato wa ajabu (zaburi 139:14), kuna kitu cha zaidi kwetu kuliko utu wetu wa nje. Mwanadamu amekuwa akitafuta kitu kikubwa na muhimu zaidi kuliko yeye mwenyewe kilicho nje ya mwili wake. Kutafuta kwake ni kwa asili ya ukamilifu. Hata kwa wanafalsafa na wasosomi wa Athene, Paulo alishuhudia shauku hii kama ilivyojidhihirisha katika jaribio la upotoshaji la kuabudu miungu isiyojulikana. (Matendo 17). Ingawaje kukamilika kwa mwanadamu, kunapatikana kwa Yesu Kristo pekee.

***"Maana katika Yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili. Na ninyi mmetimilika katika Yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka*"** (Wakolosai 2:9-10).

Yesu tu ndiye awezaye kutukamilisha, kwa sababu ni katika Yesu tu ukamilifu wote wa Uungu unapatikana. Soma maelezo mazuri na ya ajabu yanayomwelezea Yesu kuwa ni nani, yanapatikana katika Wakolosai 1:15-19. Hakuna mtu anayeweza kulinganisha. Hakika, Jitihada nyingi za mwanadamu haziwezi kumpa mwanadamu, ukamilifu unaopatikana ndani ya Kristo pekee. Sio falsafa, tamaduni, ibada ya malaika, maono, wala dini iliyobuniwa (Wakolosai 2:8, 18, 23). Badala yake, ukamilifu unapatikana katika wokovu unaopatikana ndani ya Kristo. Maelezo ya wokovu huo hutumika kama kitabu kwa picha hiyo Tukufu ya Kristo katika Wakolosai 1:15-19 (1:13-14, 1:20-23). Pia inapatikana katika kuendelea kwa mtu kukua Kiroho.

Maombi ya Paulo kwa Wakristo ni kuwa wapate "Mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa, (Wakolosai 1:10). Anaendelea kueleza ni kwa jinsi gani hii inaweza kutokea; kwa kuzaa matunda, kuongezeka katika maarifa ya Mungu, kuimarishwa na nguvu na kumshukuru Baba (Wakolosai 1:10 – 12).

Ukamilifu ni muhimu bila shaka na unapatikana katika Kristo tu.

**David Deffenbaugh anahubiri katika kanisa la Bwana Kusini Magharibi katika mji wa Oklahoma, Marekani.**

## Je, ulijua?

**Ardhi ya Biblia imenyooka maili zipatazo 2200 kutoka Mashariki mpaka Magharibi (Rumi mpaka Ghuba ya Uajemi) na maili 900 kutoka Kaskazini mpaka Kusini (Mlima Ararati hadi mlima Sinai). Sehemu kubwa ya upeo huo ni maji (Mfano: Bahari ya Mediterania, Bahari nyeusi, Bahari ya Caspian, Bahari nyekundu, Ghuba ya Uajemi, Bahari mfu, Bahari ya Galilaya, Ghuba ya Suez, Ghuba ya Aqaba).**





# Ndege jamii ya Kipanga

**Brett Petrillo**

Uzito wake ni pauni mbili tu (sawa na gramu 907.185, kilo moja kasolo) lakini wakati macho yake yanapotazama mawindo, anaweza kwenda kasi maili 242 kwa saa, na kuwa mnyama mwenye kasi zaidi kwenye sayari, the kozi kipanga hana shaka wala mashaka kwa kuwa ni moja ya viumbe vya kushangaza. Ili kufikia kasi kama hiyo, lazima awe na uwezo fulani.

**1. Umbo la mwili;** wakati ambapo kozi kipangaanapoanza kushuka, kwa kawaida ananyumbua mwili wake ili uwe katika umbo kamili la angani, ambalo linawezekana kuwa kama kichwa cha mshale. Mara tu anapokuwa katika nafasi hii, ni risasi kuelekea mawindo yake kwa zaidi ya maili 200 kwa saa. Cha kushangaza, upimaji umebaini kuwa katika hewa ya juu, kozi kipanga anaweza kinadharia kufika kasi ya mita 174 kwa sekunde, amabyo ni sawa na maili 389 kwa saa. ni jambo moja la kasi sana, lakini kudhibiti mwendo ni jambo lingine. Hakuna tatizo hapa. Lazima vipanga wote wapate kidogo kubadilisha

umbo la mwili kutembea upande upande, kupunguza mwendo, kuongeza mwendo au chochote kinachohitajika kufikia lengo na kujiweka salama.

**2. Manyoya;** wakati unapoifikia kasi hiyo, isingechukui muda mrefu baadhi ya manyoya yake kung'oka. Kwa ndege huyu, manyoya yake ni marefu sana kwa ajili ya kumfanya awe na uwezo wa kwenda angani zaidi, lakini pia ni magumu kiasi cha kuweza kukabiliana na upepo, lakini, kinachovutia zaidi. Katika kipindi kifupi kilichopita wanasanyansi wamegundua kuwa ndege huyu anachomoza manyoya mengine madogo katikati ya mgongo wake wakati wa kuruka. Manyoya haya madogo kimsingi humsaidia kukabiliana na upinzani, ambapo kwa kawaida angekutana na upinzani mkali zaidi wa hewa ambao ungepunguza kasi yake. Kwa umbo lake na manyoya yaliyopangwa vizuri, ndege huyu ameumbwa kuwa mwenye kasi.

**3. Kupumua;** ikiwa umewai kupata upepo mkali unaovuma usoni mwako wakati unakimbia, labda umegundua kuwa inakuwa ngumu sana kupumua. Sasa fikiria kujaribu kupumua kwenye upepo wakati unapokuwa kwenye kasi ya maili 200 kwa saa katika uso wako. Kwa karibu ndege wengine wote, ingekuwa haiwezekeni kwao kupumua, na inawezekana kusababisha uharibifu wa mapafu kutokana na mgandamizo wa hewa, lakini ndege huyu ameumbwa kikamilifu kwa kuwekewa kitu kinachoitwa tubercle (kinundu), ambacho ni kidogo kwa muundo… wa koni katika kitundu cha pua yake. Wakati wa kushuka, muundo huu mdogo hupunguza hewa inayoingia puani na kumrahishia huyu ndege kupumua kwa urahisi, katika mwendo wa maili 200 kwa saa.

**4. Macho;** kasi hii yote haina maana ikiwa ndege huyu hawezi kuona mawindo yake kutoka umbali mrefu sana. Ndege huyu ana macho makubwa sana na uwezo wake wa kuona ni mara nane bora kuliko waonavyo binadamu. Wanaweza kugundua mawindo yao karibu umbali wa maili sita kabla hawajaenda kwenye mashambulio. Macho yetu ili yafanane na macho ya kozi kipanga, tungehitaji kuwa na macho

yenye upana wa inchi tatu na uzito wa pauni 4 (sawa na gramu 1814.369 au kilo 1.814).

Sifa hizi kwa pamoja ndizo zinazomfanya ndege huyu kuwa wa ajabu zaidi miongoni mwa wanyama wanaokula nyama, mwenye uhakika na, kasi zaidi. Kila moja ya uwezo huu lazima uwepo mahali husika kwa ndege huyu ili aweze kuwinda na kuishi. Kila ninapomfikiria mnyama aliye na uwezo wa hali ya juu kama huu, daima anaibua pingamizi akilini mwangu dhidi ya mageuzi (evolution). Kwa mfano, Je, kipanga alijuaje kugeuza uwezo huu wote? Zaidi ya hayo, hata kama angeweza kufanya hivyo kwa mamilioni ya miaka ya mabadiliko kidogo. Je! Uko wapi uthibitisho usioweza kukanushwa, ulio na kumbukumbu ya kuthibitisha matukio haya?

Bado, kumtazama mnyama kama huyu kunaibua maswali makubwa zaidi. Kwa kuwa wananadamu wako juu ya kiwango cha mageuzi, kwa nini hatuna uwezo huu wa kushangaza? Ingefaa kuwa na uwezo wa kipanga kuruka, na uwezo wa macho yake. Litakuwa jambo la ajabu kuwa na uwezo wa kupumua chini ya maji kama Papa. Ingekuwa vizuri sana kuwa na uwezo wa kuotesha viungo vyote kama wafanyavyo baadhi yawanyama watambaao. Itakuwa jambo la kushangaza kunusa vilevile kama mbwa awezavyo, kusikia kama tembo au agalau uwe na nguvu za sokwe, amabye anasemekana kuwa ni ndugu wa karibu “sana” wa mageuzi. Lakini hatuna hata mojawapo ya uwezo huu, wala ushahidi wowote wa maandishi unaoonyesha jinsi gani na kwa nini tuliwapoteza kwa haraka hivi.

Mapengo ni makubwa sana na ni mengi mno kuvumilia katika mageuzi, wakati hakika kuna kiwango cha imani inayohitajika, wingi wa ushahidi unaotuzunguka unaendeleza yote kwa Muumba. Hatujawahi kuona mnyama yeyote akibadilisha aina yake (Mwanzo 1:24-25). Kila mahali tunapofunua, tunaona ubunifu, mipangilio na usawa wa uzazi. Zaburi 104:24 inasema ***“Ee Bwana, jinsi yalivyo mengi matendo yako! Kwa hekima yako umevifanya vyote pia. Dunia imejaa mali zako”.***

# Ushahidi

Mungu ametuzunguka kwa ushahidi wa nguvu zake na uweza wake. Tupate macho ya kuona, ulaini wa moyo wa kuikubali na mdomo wa kumsifia.

**Brett Petrillo ni waziri wa vijana na familia wa Kanisa la Bear Valley huko Deaver, Colorado, Marekani.**

**Bahari ya Galilaya (pia inaitwa Kinereti, Genezareti na Tiberio) ilikuwa mahali ambapo pa miujiza 10 iliyowekwa kwenye kumbukumbu iliyofanywa na Yesu. Eneo hili la maji liko takribani maili 12.5 Urefu, kwa 7.5 upana. Wastani wa kina chake ni futi 12, lakini sehemu yenye kina kirefu zaidi ni futi 165.. Uso wa nchi ya bahari ya Galilay ni futi 700 kutoka usawa wa Bahari.**

## Ushahidi

# Ukweli wa Kisayansi katika Neno Lake

**David Everson**

Hakia hakuna mtu kati yetu lwo anayeweza kusema kwamba Neno la Mungu lililovuviwa, Biblia, lilitolewa kwetu/tulipewa sisi kama kitabu cha kiada juu ya kanuni za kisayansi. Ni kumbukumbu inayoonesha namna Mungu anavyoshughulika na mwanadamu na kitabu chetu cha mwongozo kwa ajili ya uzima wa milele. Bado, pia hatupaswi kupunguza hiyo kama Muumba wa Ulimwengu, Mungu anapozungumza kuhusu Ulimwengu wa kimwili, hakika, kile alichokisema kikithibitishwa kuwa kweli kwa viwango vya kisayansi sehemu kubwa. Sehemu kubwa ya ukweli huu inaenda kinyume na mawazo na mitazamo maarufu ya kisayansi juu ya muda na haikuthibitishwa kuwa ni kweli na mtu asiye na makosa kwa karne nyingi baada ya Mungu kuziandika kwanza. Ninegependa kuorodhesha kwa uchache baadhi ya kweli hizi ambazo zimefunuliwa katika maneno ya Mungu. Ukweli huu unapaswa kusaidia kutia nguvu imani yetu na kutusaidia kushawishi wengine kwamba, hakika, kuna Mungu.

Tunaanza katika kitabu cha Mwanzo, sura ya kwanza, wakati ambapo Mungu aliamuru viumbe hai vyote kuwa wanapaswa "Kuzaliana … kwa jinsi yake". Lulu hii ya ajabu ya hekima na ukweli wa kisayansi haukutambuliwa na mtu wa kisasa mpaka miaka ya 1850 wakati ambapo mtaalamu mkuu wa maumbile Gregor Mendel alisomea uzazi katika baazi ya bustani. Hata wakati kazi hii ilipokuwa imekamilika na kuthibitishwa kwamba vitu vyote vinaweza kuzaa viumbe hai kama vyenyewe, jambo kubwa la wanasayansi katika siku zake walipinga au kukataa umuhimu wa ukweli huu mkubwa. Gregor Mendel alikufa akiwa hajui kuwa ataitwa "Baba wa maumbile ya kisasa". Gregor Mendel inawezekana ameelezea njia hiyo, lakini Mungu aliiumba na akaifunua miaka elfu kadhaa kabla yake.

# Ushahidi

Tukirudi katika kitabu cha Mambo ya Walawi, tunaona mambo mawili ya ajabu. Katika 17:11 inasema "kwa kuwa uhai wa mwili uko katika damu". Damu ni muhimu kwa ajili ya uzima. Madaktari na wanasayansi leo wanakisoma kitu hiki cha kushangaza na cha ajabu kwa upana ili kujifunza vizuri jinsi gani inafanya kazi na kumfanya mtu aonekane mwenye afya. Walakini, hekima ya mwanadamu, siku zote haikubaliani na Mungu katika mambo ya muhimu. Damu ilifikiriwa kuwa, mara nyingi kuliko tatizo pindi ugonjwa ulipotokea. Kwa hiyo mara nyingi, ilitolewa, kwa sababu "ilikuwa nyingi" au ilikuwa "mabya". Utoaji wa damu kama njia ya tiba karibu chochote uliendelea mpaka miaka ya 1900. Leo, ukweli wa muhimu uliofunuliwa na Mungu kwa muda mrefu uliopita unaonekana sasa ni hekima ya mwanadamu.

Kisha, katika nukuu nyingi katika Kitabu cha Mambo ya Walawi, Mungu alitoa maelezo na maonyo kuhusu ukweli mwingine wa kisayansi uliopuuzwa kwa muda mrefu: maambukizi ya Bacteria na usafi wa mazingira.sheria za Mungu kwa Waisrael kuhusu wanyama safi na wasio safi, jinsi gani ya kujikinga na maradhi kwa kujitenga na kujiosha, iliwasaidia kuwa wenye afya na kwa hivyo kufanya mapenzi ya Mungu. Ukweli huu muhimu unaojulikana na watu wote wastaarabu ni mambo ya muhimu katika muda mrefu wa kuishi na ustawi wa jumla. Hekima ya kisayansi ya Mungu Muumba aliyowaambia wanadamu kwa muda mrefu sana inawezekana kupatikana katika hospitali za kisasa zinazotoa huduma katika karne ya 21 baada ya kupuuzwa na kuchekwa kwa miaka mia moja na wanasayansi.

Zaidi na zaidi tena, tunaona ukweli wa kisayansi uliofunuliwa na Mungu Muumbaji. Nafasi haitaruhusu kutoa maelezo kwa kina. Hapa kuna mengine machahe ambayo yataimarisha imani yetu kwa Mungu na Muumba wa Ulimwengu.

1. Mduara wa dunia (Isaya 40:22) dhidi ya imani ya kwamba dunia ilikuwa tambarare.
2. Nyota zisizohesabika (Mwanzo 15:5, Yeremia 33:32) dhidi ya fikra ya kwamba kuna nyota 1024 tu.



3. Njia katika bahari (Zaburi 8:8) dhidi ya mtu kutofikiria juu ya jambo hilo kamwe.
4. Radi (umeme) na mvua vimeunganishwa (Ayubu 38:25-26) dhidi ya kupuuza muunganiko wowote.
5. Utupu katika anga la Kaskazini (Ayubu 26:7) dhidi ya kufikiria kwamba nyota ziko katika anga lote.
6. Mvutano unasaidia dunia (Ayubu 26:7) dhidi ya kuamini kwamba Atlasi inashikilia dunia.
7. Mbegu ya mtu ndani ya mwanaume na mwanamke (Mwanzo 3:15) dhidi ya mawazo kwamba mwanamke alikuwa tu kiangulio cha vifaranga.
8. Pembe nne za dunia (isaya 11:12) dhidi ya fikra za kutokuwepo kwa mvutano wa sumaku.
9. Kuwezekana kwa upasuaji (Mwanzo 2:21) dhidi ya kudhani kwamba kukata mwili ni jambo ovu.
10. Upambanuzi wa tabia ya uzazi (vizazi), (kutoka 30:27++) dhidi ya imani kwamba hakukuwa na njia ya kuthibiti tabia.
11. Misingi ya dunia (Isaya 51:13) dhidi ya dhana rahisi ya muundo wa dunia.

## Ushahidi

Hakika, tungeweza zaidi na zaidi kuendelea lakini haya machache yananapaswa kutosha kuona kwamba Mungu ndiye Muumba. Kama ambavyo mwandishi wa Zaburi alisema, ***"Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, na anga laitangaza kazi ya mikono yake"*** (Zaburi 19:1).

**David Everson ni mzee wa Kansia la Kristo huko Belington, Virginia Mashariki na ana miaka mingi ya Elimu katika Bailojia.**



# BIBLIA

**Charles Cash**

***"Kila andiko, lenye pumnzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema"*** (2Timotheo 3:16-17).

Kuna Biblia ya kiebrania huko Vatican ambayo ina uzito wa Pauni 325 (sawa na kilogramu 147.418), uzito wake mkubwa ni katika dhahabu. Ni wakala pekee sahihi ya Biblia katika lugha ya Kiebrania, ambayo thamani yake ni kubwa sana. Ikiwa ingekuwa nakala pekee sahihi katika lugha yeyote, thamani yake itakuwa haiwezi kuhesabiwa.

Biblia ya kwanza kuchapishwa iliyoweza kubebeka ilimalizika mwaka 1456 huko Mainz, Ujeruman ilichapishwa na Johhan Gutenberg, mvumbuzi wa vyombo vya habari vya uchapishaji. Inaitwa Biblia ya Gutenberg. Ni Biblia 20 tu zilizobakia, mojawapo kati ya hizo iliuzwa mwaka 1978 kwa shs. $ 2,000,000.00. kutoka kwa Gutenberg mpaka mwanzoni mwa karne ya 19 jumla ya idadi ya Biblia zilizochapishwa na kusambazwa haijulikani kwa sababu rekodi sahihi haikutunzwa. Walakini, makadirio sahihi yanapatikana, kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1800. Idadi ya Biblia zilizochapishwa kati ya mwaka 1816 hadi 1975 imefuatiliwa na chama cha Biblia cha Marekani kuwa ni 2,458,000.000. Makadirio hayo yalipanda karibu Billioni sita mwaka 1992. Mauzo ya Ulimwnegu ya Biblia ni zaidi ya milioni 100 kila mwaka inauzwa zaidi kuliko kitabu kingine chochote. Bila shaka yeyote, Biblia ni kitabu kilichouzwa zaidi kwa miaka yote. Kama ilivyo leo, inakadiriwa Biblia Bilion 8 zimesambazwa Ulimwengu mzima. Hesabu

hii haihusishi matoleo mbalimbali ya kidigitali ya Biblia ambayo hutumiwa leo ni mamilioni ya watu katika Kompyuta, Simu mahiri (simu janja) na Tablet.

Biblia nzima imechapishwa kwa lugha zaidi 450. Agano jipya pekee limechapishwa karibu kwa lugha 1400. Injili ya Marko imechapishwa katika lugha zaidi ya 2370. Hata hivyo takwimu hizi zinawakilisha chini ya nusu ya lugha na lahaja zilizopo katika matumizi Ulimwenguni. Walakini, ni pamoja na magari ya mawasiliano ya zaidi ya 90% ya idadi ya watu Ulimwenguni. Katika Ulimwengu ambao sasa una zaidi ya wakazi Biliono saba, kuna makadirio ya Biblia moja kwa kila mtu aliye hai katika dunia. Kwa bahati mbaya, kuna mgawanyo wa Biblia kati ya Mataifa ya Ulimwengu, hasa katika Asia na Mashariki ya kati. Baadhi ya Nchi katika Ulimwengu wa Magharibi wanaweza kuwa na Biblia zaidi ya idadi ya watu, kama vile huko Marekani. Kulingana na katalogi ya kitabu cha Harper San Francisco, Wamarekani wanatumia dola $425 million kwa mwaka kwa ajili ya Biblia, na wastani wa kaya ya Marekani (kila famila) wanamiliki nakala nne za Biblia.

Angalia nyaraka za uvumbuzi wa Marekani, kama vile katiba na miswada ya haki, ni ushahidi kwamba Taifa hili, tangu kuanzishwa kwake, liliundwa juu ya imani kwa Mungu na Biblia. Kama tujuavyo sote, kuna watu katika nchi hii, wachache, ambao wanafanikiwa polepole na kwa njia mbalimbali wanaharibu. Msingi huo inasikitisha kwa kweli.

Biblia ni nyingi, iwe ni ile ya nadra Biblia ya Kiebrania ya kizamani au aina ya kawaida inayopatikana katika duka lolote la punguzo au duka la vitabu, thamani halisi iko kwenye ujumbe. Biblia yako inaweza kufungwa na gamba laini, ngozi inayofaa ya Moroko na kuchapishwa kwenye karatasi nzuri ya India, lakini ni zaidi ya hiyo. Kupitia hiyo Mungu amesema **Ni neno la Mungu!** ukijitoa kwa ajili ya hazina kubwa katika Neno la Mungu na kupima thamani yake kwa ushawishi wake juu ya maisha yako na maisha ya wale wanaokuzunguka, kwa kweli ni zaidi ya bei yote. Biblia imekuwa, ikabaki na itakuwa siku zote kitabu cha vitabu.

Yesu alituhakikishia kuwa, ***"Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe"*** (Marko 13:31). Maneno yake yamepita katika Mithali, ahadi, mafundisho na njia kwa Mungu na ***"Maisha tele"*** lakini hayajawai kupita, na hayatapita kamwe.

"Hapa kuna kitabu, Biblia, kina thamani zaidi kuliko vyote vilivyowahi kuchapishwa," Patrick Henry alisema hivyo. Bado ni bahati mbaya kwangu kwa kutopata muda wa kuisoma." Hmmmmmm! Je! Tunapata muda wa kuisoma?

**Charles Cash anafanya kazi pamoja na Kanisa la Bwana huko Bella Vista, Arkansas, Marekani.**

# KUNA NINI KATIKATI?

**Edward Anderson**

Wakati wa kujadili sanaa za upishi – kwa kweli tulikuwa tunazungumza tu juu ya vitafunwa vya shule. Mwalimu wa shule ya Sekondari aliuliza ikiwa nimewahi kuwa na silesi za mkate zilizopakwa siagi. Nilimuhakikishia mara nyingi nilikuwa nikieleza jam ya mama yangu ya kusafishia mdomo kati ya Nusu mbili za Biskuti za moto, mpya kutoka kwenyeoveni, kusambaza kwa uaminifu kwa wema siage "iliyoikwa" kwa siku kuu ya Kimungu! Walakini, alikuwa na kitu kingine akilini. Alikumbuka wakati nyakati zilikuwa ngumu sana kwamba



angeoka vipande viwili vya mkate pamoja na kula vipande hivyo pasipo kitu katikati.

# Neno la Mungu

Neno la Mungu ni chakula kwa ajili ya roho, ***"mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwakila neno litokalo katika kinywa cha Mungu"*** (Mathayo 4:4). Lina vitu na utoshelevu wa kutukamilisha kabisa katika huduma ya Mungu (2 Timotheo 3:16 – 17). Maneno ya Mungu hayatamkatisha tamaa mtu mwenye ***"moyo mzuri na mnyoofu"*** (Luka 8:15). Huiridhisha nafsi yenye njaa inayotafuta ukweli (Yohana 8:32, 17:17). Ni rahisi na inayoweza kubadilika kama mtoto mchanga ayataminivyo "Maziwa halisi ya Neno" (1Petro 2:2) au litatumika kama "chakula kigumu" kwa wale ambao "wana umri mkubwa" (Waebrania 5:12 – 14).

Kabati la neno la Mungu siku zote limejaa. Ni kama pipa la mjane la chakula na chupa ya mafuta ambavyo vilidumu kipindi chote cha ukame (1Wafalme 17:14). Ni kama viatu vya Waisrael ambavyo havikuchakaa kwa miaka 40 ya kutembea walipokuwa jangwani (Kumbukumbu 29:5). Ni kama mikate na samaki katika mikono ya Bwana walipolishwa makutano wenye njaa (Yohana 6). Neno la Mungu ni chakula cha kutosha kwa kila hali na majaliwa katika maisha. Baba wa Mbinguni amehidhi vizuri kila kitu tunachohitaji kwa ajili ya afya ya kiroho, kwa utaratibu na kwa uzuri. Neno la Mungu litatufanya kuwa wanyenyekevu na watu wa toba, kamwe haliwezi kuturuhusu tupate kiburi na kujidai. Litatubadilisha daima kuwa na upendo zaidi, wapole, wanaojidai na wazuri (wema) (1Wakorintho 13).

Ikiwa umekuwa mtu wa kula vyakula vinavyochakaa vya Ibilisi na vimevimba na kulemewa na dhambi, ni wakati wa kubadilisha mlo wako. ***"Sheria ya Bwana ni kamilifu, huiburudisha nafsi"*** (Zaburi 19:7). Kristo tu "***ndiye mwenye maneno ya uzima wa milele"*** (Yohana 6:68). Agano lake jipya linatuelekeza namna ya **kumwamini Mungu** katika Mungu na mwana. (Waebrania 11:6, Yohana 8:24), **kutubu** kwa ajili ya dhambi zetu zote (Matendo 3:19), na **kumkiri Kristo kama Mwana na Mungu** (Matendo 8:38, Warumi 10:9 – 10), **kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi** (Matendo 2:38, Marko 16:16) na siku zote kuwa waaminifu katika huduma ya Bwana na kazi (1Wakorintho 15:58).

**Edward Anderson ni mhubiri wa Kanisa la Kristo huko Cathage, Tennese, Marekani.**

**Ikiwa umekuwa unakula vyakula vinavyochakaa vya Ibilisi na vimevimba na kulemewa na dhambi ni wakati wako wa kubadilisha mlo.**




1. Kwa nini kila mwanaume awe na mke na kila mwanamke awe na mume? (7:2)
2. Ni nani mwenye mamlaka juu ya mwili wa mtu anapooa au kuolewa? (7:4)
3. Kwa nini Paulo anasema wanandoa wasinyimane isipokuwa wamepatana kwa muda? (7:5)
4. Kwanini Paulo anasema kwamba alitamani wanaume wote wawe katika mahusiano na ndoa? (7:7)
5. Je! Hii ilikuwa amri kwa Bwana au ushauri wake ulioongozwa na Roho? (7:6)
6. Ni kwa sababu gani Paulo anasema watu wanapaswa kuona? (7:6)
7. “Maana ni afadhali _____ kuliko ______ tama” (7:9)
8. Mkristo anapaswa kumfanyia nini mwenza wake asiyeamini? (7:12-13)
9. Je! Mtu anapaswa kufanya nini ikiwa mwenzi wake asiyeamini akiondoka? (7:15)
10. “Maana Mungu ametuita katika ____________ (7:15)
11. Je! Muumini anaweza kufanya nini kwa mwenzi wake asiyeamini? (7:16)

(Angalia kwenye gamba la nyuma ya kitabu kwa ajili ya majibu)

“1 Basi kwa habari ya mambo yale mliyoandika, ni heri mwanamume asimguse mwanamke. 2 Lakini kwa sababu ya zinaa kila mwanamume na awe na mke wake mwenyewe, na kila mwanamke na awe na mume wake mwenyewe. 3 Mume na ampe mkewe haki yake, na vivyo hivyo mke na ampe mumewe haki yake. 4 Mke hana amri juu ya mwili wake, bali mumewe; vivyo hivyo mume hana amri juu ya mwili wake, bali mkewe. 5 Msinyimane isipokuwa mmepatana kwa muda, ili mpate faragha kwa kusali; mkajiane tena, Shetani asije akawajaribu kwa kutokuwa na kiasi kwenu. 6 Lakini nasema hayo, kwa kutoa idhini yangu, si kwa amri. 7 Ila nipendalo ni kwamba watu wote wawe kama mimi nilivyo; walakini kila mtu ana karama yake mwenyewe itokayo kwa Mungu, huyu hivi, na huyu hivi.

8 Lakini nawaambia wale wasiooa bado, na wajane, Ni heri wakae kama mimi nilivyo. 9 Lakini ikiwa hawawezi kujizuia, na waoe; maana ni afadhali kuoa kuliko kuwaka tamaa.

10 Lakini wale waliokwisha kuoana nawaagiza; wala hapo si mimi, ila Bwana; mke asiachane na mumewe;

11 lakini, ikiwa ameachana naye, na akae asiolewe, au apatane na mumewe; tena mume asimwache mkewe.

12 Lakini watu wengine nawaambia mimi, wala si Bwana, ya kwamba iwapo ndugu mmoja ana mke asiyeamini, na mke huyo anakubali kukaa naye asimwache. 13 Na mwanamke, ambaye ana mume asiyeamini, na mume huyo anakubali kukaa naye, asimwache mumewe. 14 Kwa maana yule mume asiyeamini hutakaswa katika mkewe; na yule mke asiyeamini hutakaswa katika mumewe; kama isingekuwa hivyo, watoto wenu wangekuwa si safi; bali sasa ni watakatifu. 15 Lakini yule asiyeamini akiondoka, na aondoke. Hapo huyo ndugu mume au ndugu mke hafungiki. Lakini Mungu ametuita katika amani. 16 Kwa maana wajuaje, wewe mwanamke, kama utamwokoa mumeo? Au wajuaje, wewe mwanamume, kama utamwokoa mkeo?”

**KUMBUKA:** Kifungu hiki kina maelezo ya Paulo kuhusu ndoa kwa Mkristo. Katika utamaduni wa Wakorintho, uasherati, uzinzi na ushoga vilifanywa kawaida, kwa hivyo Paulo alitambulisha tatizo hili. Paulo alifikiria kwamba ni vizuri kubaki bila ndoa; walakini, useja hakika haikuwa hali ya lazima au bora kimaadili kuliko ndoa. Pia anatambua watu wengi hawastahili/hawawezi kubaki wasiooana kwa sababu ya tamaa.

Majadiliano kamili ya masuala yote kuhusu ndoa na talaka haiwezekani. Mungu anafundisha kila mara kuwa anachukia talaka na anataka waume na wake wote waishi pamoja katika mapenzi (Upendo) na maelewano. Bila shaka, hivyo sio mara zote inawezekana, walakini, sababu pekee ya kimaandiko iliyotolewa kwa talaka ni uasherati (Mathayo 19:8-9).

# Usiende Pamoja na Mbuzi!

**Perry N. Hall**



Pamoja na maelezo ya wazi sana, Muumba wetu, Mwokozi wetu, na hakimu wetu aliyetufunulia katika Mathayo 25:31-46 ya kushangaza sana, hukumu kubwa na ya mwisho ya wanadamu wote. Alionesha kwamba katika hukumu inayokuja kwamba kila mtu atahukumiwa siku hiyo kuu na uongozi wake wa kutoa ujira umetolewa na Baba kwa mwanae (Matendo 17:31). Wakati ambapo Kristo atakuja katika Utukufu wake kuhukumu Ulimwengu,

atawaleta Malaika wake Watakatifu wote na kukaa katika enzi yake ya Utukufu. Hivi sasa ameketi juu ya kiti cha Enzi cha Baba yake wa Mbinguni, katika mkono wake wa kuume. Ni kiti cha Enzi cha Neema, ambayo tunaweza kuja kwa ujasiri. Pia ni kiti cha enzi cha Serikali, Enzi ya Baba yake, Daudi, kutoka kwa yeye anatawala kwa Mamlaka yote Kanisa lake au Ufalme. Yeye ni Kuhani juu ya kiti cha Enzi.

Kiti cha Enzi cha Utukufu atakachokalia siku ya mwisho ni kiti chake cha hukumu. Huko, atawatenganisha wanadamu watiifu na wasiowatiifu. Kwa sasa wanakaa pamoja katika Mataifa, majimbo, nchi, miji, makanisa na familia. Yesu anasema atawatenganisha mmoja kutoka kwa mwingine kama Mchungaji anavyowagawa kondoo na mbuzi. Atawaweka kondoo katika mkono wake wa kuume, lakini mbuzi atawaweka katika mkono wale kushoto. Baadaye alitangaza katika muktadha huo huo kuwa wale wa kushoto wataenda mbali katika adhabu ya milele.

Ndugu, hatupaswi kwenda pamoja na mbuzi sasa ikiwa hatutaki kwenda pamoja nao katika umilele. Yesu alijifunua kwamba yeye ni Mchungaji mwema na kwamba atautoa muhai wake kwa ajili ya kondoo. Vilevile alitangaza kwamba kondoo wake wanaisikia sauti yake na kumfuata. Hao anawapa uzima wa milele.

Kondoo ni wapole, wanyenyekevu, wavumilivu, wasiolalamika, wanafaa na hawana hatia. Pia wanamfuata Mchungaji wao. Mbuzi hawana utaratibu na hawaongozeki na wafuasi, kwenda kinyume na mapenzi ya Mchungaji na wale wote wanaoingia katika njia yao ya uasi. Mbuzi, wasiotii, wasiojali wa Ulimwengu huu hawana wasiwasi kumhusu Mungu, mapenzi yake, nafsi zao na mahitaji au ustawi wa wenzao. **Usiende Pamoja na Mbuzi**.

**Perry N. Hall ni mhubiri wa Injili anayeishi huko Tyler, Texas, Marekani**

**Adamu alikufa akiwa na miaka 930. Kulingana na nasaba ya vizazi vilivyoorodheshwa katika Mwanzo, Adamu angekuwa hai wakati mzao wake Lameki ambaye alizaliwa (miaka 61 baadaye)! Adamu alikufa miaka 121 kabla ya Nuhu kuzaliwa.**

# Yatazameni Mashamba

**Dayton Keesee**

Ni msingi kwamba ujumbe wa Kristo miononi mwa watu ulikuwa ***"Kutafuta na kuokoa kilichopotea"*** (Luka 19:10). Kutafuta huko ni mchakato wa kujitolea. Neno la asili (Kigiriki; Zeteo) linamaanisha "Kutafuta (ili kujua) kwa kufikiri, kutafakari, kutoa hoja …ili kuuliza… lengo, jitihada baada… shauku au tamaa … Uhitaji, mahitaji (Thayer 272).

Je! Umekuwa ukifikiria, kutafakari, kujadili, kuuliza, kulenga kujitahidi baada, kutamani "Nafsi iliyopotea" hivi karibuni?. Ikiwa tunapanga kufuata nyayo za Kristo (1Petro 2:21), tunapaswa kufikiria, kutafakari, kuuliza, kujitahidi baada ya baadhi ya roho au nafsi zilizopotea? Je! Kweli Kristo alitimiza na kuonesha kazi yake?.

Mfano halisi (unaothibitisha "Ndiyo alifanya) unapatikana katika Yohana 4. Inapendeza kwamba kielelezo chake kilitokea (1) Katika anga la mgeni miongoni mwa Wasamaria, (2) wakati wale mitume wake walipokuwa wakitumia wakati wao kufikiria, kutenda na kuzungumzia kimsingi kuhusu chakula na kula (Yohana 4:8,31,33), (3) walikuwa wanafikiria zaidi kuhusu mwenendo wa sahihi wa kitamaduni kuliko kuziongoa roho zilizopotea (4:27), (4) walikuwa wakifikiria ni wakati usiofaa kutafuta roho, (walichukulia kuwa ni mahali pasipo sahihi, watu wasiofaa, na wakati usio sahihi.

Aliwapa karipio aliposema ***"Inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno"*** (Yohana 4:35). Muktadha wa Yohana 4 unathibitisha kwamba Yesu alikuwa anajua nini alikiongea kuhusu haki, basi mbele ya macho yao, miongoni mwa Wasamaria hao. Mwanamke huyo aliyekuwa akiishi na mwanaume asiye mume wake (Yohana 4:17) na ***"wengi wakaamini kwa sababu ya maneno yake"*** (41: Yohana 4:14). Kristo alikuwa na vyote viwili lengo na imani katika huduma yake, wakati mitume wake walijali zaidi **chakula** kuliko **iman**i, na **ukawiaji** kuliko **kutumika**!.

Je! Unadhani Kristo anaweza kuwa anasema kwako au kwangu ***"Inua macho yako utazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno"*** (mstari wa 35)? Kutazama huko ni katika hali ya agizo (Kigiriki. Theasthe ya theaomai) inamaanisha "kuangalia kwa makini, kwa kutafakari, kujifunza kwa kuangalia, kutambua (Thayer 284). Je! Unatazama kama hivyo sasa kama inahusiana na roho zilizopotea? Je, unatambua shamba au mashamba kwamba ni "meupe tayari kwa kuvuna?"

Ndugu Norman Gipson alionekana kutojali wakati alipokua miongoni mwa walimu_katika shule ya kuhubiri ya Sunset mwaka 1978, akielezea kwamba ulikuwa umeshakuwa usiku zaidi. Baada ya kusoma pamoja na mtu, alirudi nyumbani na kuandika wimbo ufuatao kuhusu uzoefu wake katika jioni hiuo.

**Ulikuwa Wapi kwa Muda Wote Huu?**

Niliongea na mtu kuhusu Yesu;
Alisikiliza kwa mshangao wa ajabu;
Kisha nikahisi mwanzo wa maumivu moyoni mwangu
Alipouliza na machozi katika macho yake;

**Kiitikio**

Ulikuwa wapi kwa muda wote huu?
Kwa nini hukuja katika mlango wangu?
Nimeishi katika dhambi kwa muda mrefu?
Kwa nini hukuniambia kabla?

**Ubeti wa pili**

Nilimwambia Bwana alikuja kutoka kwenye Utukufu
Kuleta chini wokovu kwa watu;
Alisikia kwa furaha ya ajabu,
Kisha alilia aliponiuliza tena

**Kiitikio**

Umekuwa wapi kwa muda mrefu?
Kwa nini hukuja katika mlango wangu?
Nimeishi katika dhambi kwa muda mrefu?

Kwa nini hukuniambia kabla?

**Ubeti wa tatu**

Kwa Ulimwengu wote waambie habari kuu
Kwamba Kristo ndiye uzima, kweli na njia;
Kwa hiyo wakati utakapofika na hukumu itakapokuja,
Hakuna mtu katika umati huo anaweza kuhitaji kusema;

**Kiitikio**

Umekuwa wapi kwa muda mrefu?
Kwa nini hukuja katika mlango wangu?
Nimeishi katika dhambi kwa muda mrefu?
Kwa nini hukuniambia kabla?

**Kiitikio**

Je! Kuna mtu anakusubiri wewe uje kwenye mlango wake?

**Dayton Keesee ni mzee katika Kanisa la Bwana huko Choctaw, Oktahoma, Marekani.**

# Kama Ningekuwa na Makala Moja Zaidi

**Bob Prichard**

kwa miaka kadhaa nimekuwa nikiandika mamia ya makala rasmi na makala katika magazeti. Kama mambo yakienda kama nilivyopanga,



nitaandika mamia kadhaa zaidi, lakini siku inakuja ambayo nitaandika ya mwisho. Nitataka kukuambia nini ikiwa hili ni jambo langu la mwisho?

Kama moja ya nyimbo zangu pendwa inavyosema “Ikiwa huwezi kuimba kama Malaika, Ikiwa huwezi kuhubiri kama Paulo, basi waambie Upendo wa Yesu, na useme alikufa kwa ajili ya wote” hapo ndipo ninapopaswa kuanzia “wakati ninachunguza msalaba wa ajabu amabao mwana wa Mfalme wa Utukufu alikufa”, siwezi kusaidia lakini

nashangaa kuhusu upendo wake. Ninataka kukumbusha kwamba unaweza kuwa na masamaha kama nilionao. Ingawa hatukustahili, Yesu anatupenda vya kutosha  hadi kufa kwa ajili yetu.

***"Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu, kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema. Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi"*** (Warumi 5:6-8).

Ikiwa unakubali kile alichokifanya kwa ajili yako, haitakuwa vigumu kufanya yale anayotuagiza tuyafanye kama wajibu. ***"Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuikoa nafsi yake, ataipoteza, na mtu atakayepoteza nafsi yake kwa ajili yangu, ataiona. Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata Ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake, au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake"?*** (Mathayo 16:24-26).

Kujikana mwenyewe ni rahisi sana kusema kuliko kufanya, bila shaka, lakini ikiwa unaelewa na kuthamini kile alichofanya kwa ajili yako, hakika utataka kumtii. Pasipo yeye umepotea, lakini pamoja na yeye utakuwa na Mbingu kama nyumbani kwako (Marko 16:15 – 16). ***"Amin, amin, nawaambia, mtu akilishika neno langu, hataona mauti milele"*** (Yohana 8:51). ***"Mkinipenda, mtazishika amri zangu.***" (Yohana 14:15). Je! Unamtii Yesu. ***"Naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu, wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote"*** )1Yohana 2:2).

**Bob Prichard anahubiri katika Kanisa la Bwana huko Oxford, Mississippi, Marekani.**

**Je! Ulijua?** Katika nyakati za Agano jipya, Korintho ulikuwa ni mji wa michezo ya Isthmian  (sawa na Olimpiki) iliyofanyika kila baada ya miaka 5. Matukio yaliyojumuishwa ni mbio, kuruka, kurusha mshale, ndondi na mieleka. Hata vita vingeweza kusimamishwa kwa ajili ya matukio ya michezo.



# JIPIME NA BIBLIA

Martha Rushmore

## Ndoa

6. Kwa utiifu alifuatana na Ibrahimu  Mwanzo 12:1-5
7. Mapambo ya harusi. Isaya 62:10-19
9. Wanandoa hawapaswi kufanya hii. Mathayo 10:9
11. Uhusiano wa mke kwa mumewe. Mithali 12:4
12. Mke wa pili wa Abraham. Mwanzo 25:1
15. Alikuwa na mamia ya wake na wake za pili. 1Wafalme 11
16. Alioa mwanamke mbaya. Mwanzo 29:15-30
17. Mzina aliyemuua mume wa mwanamke. 2 Samwel 11



**Chini**

1. Mapambo ya harusi. Isaya 62:10
2. Amri wanaume. Waefeso %;25
3. Mke ampende nani. Tito 2:4
4. Mji ambao Yesu alihudhuria shere ya ndoa. Yohana 2:1-5
5. Neno la Biblia kuhusu uchumba. Mathayo 1:18
8. Kuhusu wazazi wake, mwanaume anapaswa kufanya hivi.  Mwanzo 2:24
10. Katika ukoo wa Yesu Kristo. Ruth 4:9-10, Mathayo 1:5
13. Amri kwa wanaume. Mithali 5:18
14. Talaka kwa sababu ya unyenyekevu wake. Esther 1



# Kanisa Lililoteswa

**Gary C. Hampton**

Barua ya Bwana kwa Kanisa la Samaria imejaa maneno ya uhakika kwa wale wote wanaoishi katika nyakati ambazo watu kusimama katika imani ya mtu lilikuwa jambo linalodhihakiwa. Smirnaa ilipakana maili 40 Kaskazini mwa Efeso. Smirna ulikua ni mji ambao kwa asili uliundwa na Iskanda Mkuu. Kulikuwa na maktaba kubwa huko ambayo baadaye ilihamishiwa Iskandria. Smirnaa pia ilikuwa eneo la michezo ya Olimpiki. Mapema mnamo mwaka 23 baada ya Kristo (B.K), mji huu ulijenga hekalu kwa Tiberia, Mfalme na kuongoza njia huko Asia kwa ajili ya ibada ya Mfalme chini ya Domitiani. Kulikuwa na idadi kubwa ya Wayahudi katika mji huo. Kanisa, liliteswa kupitia mateso na kifo,

lazima uwe umehakikishiwa kujua kwamba Yesu ni wa milele na ameshinda kaburi (Ufunuo 2:8).

Ni rahisi sana kwa wanaoteseka kujisikia wanapata tabu kama vile hakuna mtu anayewajali. Yesu anajua mambo ya kila mtu yaliyopo na yajayo, na aliahidi kuwasaidia kubeba matatizo yote (Waebrania 2:17 – 18, 4:15-16, 1Wakorintho 10:13). Vile vile Bwana alijua kuhusu umaskini wao; kwa kweli, aliwahi kupitia hali kama hizo. (Mathayo 8:20). Wakristo hawapaswi kutegemea juhudi zao wenyewe katika kupata utajari wa mali (Mathayo 6:19-20). Kanisa la Smirna kimwili lilikuwa maskini lakini Kiroho tajiri. Mfalme Yesu pia alijua kuhusu kufuru au kusema dhidi ya hiyo, ilikuwa ikitokea kwa wale waliosema wao ni Wayahudi. Kulikuwa na Sinagogi kule, lakini Bwana anasema lilikuwa la Shetani sio lake. Waisrael wa Mungu wa kweli katika kipindi cha Kristo ni wale wote ambao wametahiriwa katika moyo (Ufunuo 2:9, Warumi 2:28-29, Wafilipi 3:3).

Ingawa majaribu makali yalikuwa bado yanakuja, na yangeweza kudumu kipindi kamili, Kanisa lilihakikishiwa kuwa saa hiyo siku moja itakwisha (2Timotheo 3:12, Wafilipi 1:29). Adui wa kweli wa Kanisa ni Shetani, jina Ibilisi linayomaanisha Mshitaki au mchongezi (cf Yohana 8:44, 1Petro 5:8, Luka 22:31). Anawajaribu au kuwapima wafanye dhambi kwa njia kamili inayowezekana, kifungo, uhamisho au kifo. Wakristo hawapaswi kuogopa juu ya mambo haya, kwa kuwa ikiwa watabaki katika imani ya kweli, hata kama itaathiri maisha yako, uzima wa milele itakuwa thawabu yao (Luka 12:4-5, Yakobo 1:12, 2Timotheo 4:6-8, 1Petro 5:4, 1Wakorintho 9:25).

Kumbuka, huku ni nyumbani kwa michezo ya Olimpiki, kwa hiyo kuwa na uzima wa milele, inaelezwa kama taji ya ushindi ingekuwa ya maana kabisa. Ndugu walihimizwa kusikiliza maneno ya barua hii, na kama wangefanya hivyo, wangekuwa kinga hadi mauti ya pili (Ufunuo 2:10 – 11, 20:14, Warumi 6:23). Kinga hiyo iliahidiwa kwa wale wote walioshinda.

Kanisa la Mungu huko Smirna walipitia majaribu makubwa zaidi kuliko wengi wetu ambavyo tunajua au tumewahi kufikiria, lakini

walibaki waaminifu licha ya mateso yao na waliahidiwa taji ikiwa wangebaki waaminifu. Mkristo wa leo anapaswa kutiwa moyo na mfano wa Wakristo hao ili kubaki wakweli kwa Bwana ambaye hutoa uzima wa milele kama shada la ushindi.

**Gary C. Hampton anahubiri katika kusanyika la barabara ya Siwell huko Jackson, Mississipi, Marekani.**

# Ni kweli Kanisa linaumuhimu hivyo?

**Patrick Morrison**

Kukua kwa idadi ya watu kumekuwa kukipoteza imani juu ya dhana nzima ya "Kanisa" au "Dini iliyoundwa". Maelfu kwa maelfu yanaacha madhehebu makubwa ili kufuata Ukristo wa aina ya Mfalme Burger (katika hili unajiuliza, kauli mbiu ya Burger ni, "shika njia yako". Wazo maarufu ni kwamba Kanisa si la muhimu hivyo, kwamba ni sehemu isiyokuwa ya lazima ya uhusiano wa kweli na Kristo, au si kitu zaidi ya kikwazo kwa "hali halisi" ya kiroho.

Ni kweli kwamba, kwa wakati fulani, tumefanya udhalimu mkubwa Ulimwenguni katika njia tunayoishi na matendo yetu katika Kanisa, wakati mwingine kulibadilisha kuwa si kitu chochote isipokuwa biashara au shirika la kijamii. Wakati mwingine tuna hatia ya kumtazama Kristo kwa njia "tunayolifanya Kanisa". Kuna wakati njia zetu na msukumo wetu sio kama vile unavyotakiwa kuwa. Ni wa kinafiki, kuna watu maalumu, kuna wamiliki wa biashara wasio waaminifu na kuna mawazo ya kidunia, wanaotafuta raha ya anasa katika Kanisa. Bado, kuna waaminifu pia, waliojitolea, wanafanya kazi kwa bidii, wafuasi wa Kristo, wanyenyekevu, watu wa toba, wanaopenda kweli, wanaomtafuta Mungu, wavumilivu, washirika wanaosamehe katika Kanisa.

Kwa sababu tu tunashindwa kuishi kwa picha bora ya namna Kanisa linapaswa kuwa haimaanishi kwamba hakuna ubora wa kanisa kama huo au haipaswi kuwepo. Haijalishi ni kiasi gani tunaweza kulichanganya, hakuna kitu tunachoweza kufanya au kusema kinachoweza kulifanya Kanisa lionekane halina maana. Limekuwapo daima na daima litakuwa kamilifu kwa wokovu wa nafsi zetu. Kwa sababu kadhaa zinazolifanya Kanisa lionekane kuwa ni la muhimu, nazo ni:-

**Kanisa ni la muhimu kwa sababu LIMEZALIWA MBINGUNI**. Dharau nyingi juu ya wazo la Kanisa leo ni kwa sababu wengi wako chini ya maoni kwamba ni bidhaa ya asili ya Binadamu. Ikiwa hiyo

ndivyo ilivyo, basi sisi sote twapaswa kusimama tukipinga! Walakini, Kanisa kama tulionavyo katika maandiko (linalotakiwa kuwepo leo) ni lenye asili ya kimungu. Kanisa ni kusudi la milele la Mungu, lililotimizwa katika Yesu Kristo. (Waefeso 3:10-11). Jaribio lolote la kuliona Kanisa kama halina maana ni kutangaza kwamba mpango wa Mungu wa milele wa ukombozi katika Kristo Yesu una mapungufu. Mwenyezi alidhamiria kwamba mara tu Kanisa litakapoanzishwa atamweka kila mtu aliyeokolewa (okoka) ndani ya Kanisa la Mwanawe mpendwa (Matendo 2:47). Kulitangaza Kanisa kama lisilo na thamani, au kuudharau Ukristo wa kweli, ni tusi kwa hekima ya BWANA.

**Kanisa ni la muhimu, LIMENUNULIWA KWA DAMU.** Ni vigumu kwangu kuelewa jinsi gani wengi wanaweza kusema Kanisa sio la muhimu wakati lilikuwa la muhimu sana kwa Yesu. Kuna wale wote wanaodai kumpenda Yesu na kutaka kumtafuta lakini wanakataa kushikilia hicho alichokipenda na kuamua kukifia (Matendo 20:28). Yesu alilipenda sana Kanisa kiasi kwamba alikufa kwa ajili yake. (Waefeso 5:25). Tunawezaje kumdharau bibi arusi mtukufu wa Bwana wetu! Ikiwa tutamuiga Yesu, basi tunapaswa kulipenda Kanisa kama alivyofanya yeye.

**Kanisa ni la muhimu kwa sababu LINAKIFUNGO CHA UTUKUFU.** Yesu ni bwana arusi, na Kanisa ni bibi arusi wake (Waefeso 5:22). Ameenda kuandaa nyumba ya milele ya bibi arusi wake wa thamani (Yohana 14:1-6), na atarudi siku moja kumchukua ampeleke nyumbani kwenda naye mahali palipoandaliwa. Wakati mwisho utakapokuja, atamkabidhi Mungu ufalme (1Wakorontho 15:24). Wote walio katika ufalme huo, ambao ndio Kanisa (mathayo 16:18-19), ambao wameishi kwa uaminifu katika kumtumikia Bwana wataishi kwa uaminifu katika kumtumikia Bwana wataishi milele mbele ya Baba, Mwana, Roho Mtakatifu na wale waliokombolewa katika zama zote. Yesu hawezi kuliangalia Kanisa kama kitu kisicho na maana ikiwa atalipeleka kwa Baba katika siku ya mwisho.

**Patrick Morrison anahubiri katika Kanisa la Kristo “The Six Avenue” huko Jasper, Alabama Marekani.**

**Kanisa**

**Limezaliwa Mbinguni – limenunuliwa kwa damu – lina kifungo cha utukufu**

# MPYA

Royce Fredrick

Mara nyingi tunapenda kuwa na vitu vipya. Mungu ana vitu vipya muhimu sana kwetu.

**KUZALIWA UPYA**

***"Amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu. Nikodemo akamwambia, awezaje mtu kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? Yesu akajibu, Amin, amin nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho hawezi kuinia ufalme wa Mungu"*** (Yohana 3:3 – 5). Mtoto huzaliwa wakati anapotoka tumboni mwa mama yake. Mwenye dhambi anakuwa mwana wa Mungu pale anapotoka ndani ya maji ya ubatizo. Wakati mwenye dhambi ***"anapobatizwa katika Kristo Yesu"***, ***"anazikwa"*** katika maji, na baadaye, anatoka nje ya maji na kuanza kutembea katika ***"Upya wa uzima"*** (Warumi 6:3 – 4, Matendo 8:36 – 39). Huku ni kuzaliwa upya. ***"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya".*** (2 wakorintho 5:17).



## AGANO JIPYA

Mungu alitabiri kupitia nabii Yeremia. ***"Angalia, siku zitakuja, asema Bwana, nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda. Si kwa mfano wa Agano lile nililolifanya na baba zao, katika siku ile nilipowashika mkono, ili kuwatoa katika nchi ya Misisri, ambalo agano langu hilo walilivunja, ingawa nalikuwa mume kwao, asema Bwana"*** (Yeremia 31:31 – 32). Yesu alipokufa msalabani, alitimiliza Agano la kale, akaliondoa na kulirudishia mahala pake Agano jipya (mathayo 5:17 – 18, Wakolosai 2:14, Warumi 7: 4 – 7, Waebrania 8:6 – 13, 9:15 – 17, Luka 22:20).

## MBINGU MPYA NA NCHI MPYA

Hakuna hata mmoja anayejua wakati Kristo atakaporudi. ***"lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi, katika siku hiyo Mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufunuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea. Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafanuliwa, hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa ..? Lakini kama ilivyo ahadi yake, manatazmia Mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake."*** (2Petro 3:10 – 13). Mtume Yohana alipewa maono ya makazi ya milele ya Wakristo waaminifu. ***"Kisha nikaona Mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana Mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwishapita, wala hapana habari tena. Nami nikauona mji ule Mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka Mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi – arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe, … Na Mungu atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwako tena; wala maombolezo; wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza, yamekwisha kupita."*** (Ufunuo 21:1,4). Dunia hii itaharibiwa kabisa, lakini Utukufu wa ajabu, makazi ya milele yanatusubiri katika nchi mpya.

**Royce Fredrick ni mhariri wa waalimu wa Injili Kimataifa na anaishi huko Fort Worth, Texas, Marekani.**

# John Calvin na Neema

**Wayne Jackson**

Mmoja kati ya watu wenye ushawishi mkubwa wa kidini katika millennia yake alikuwa John Calvin wa Uswisi. Alizaliwa mwaka 1509. Akiwa na miaka 14, alienda Paris kusomea ya viwango vya juu. Alikuwa Austere Sava hivi kwamba wanafunzi wenzanke walimpa jina la utani "Kasha la mashtaka". Mwaka 1529, alianza utafiti wa sheria za kiraia. Wakati huu, ingawa Calvin alivutiwa mafundisho ya wanamageuzi wajerumani na kwa hivyo akajitosa kwenye utafiti wa Dini au kusomea mambo ya dini. Alivunja ushirika na Kanisa Katoliki (Roman Katoliki) mwaka 1533 baada ya uzoefu "wa kidini" wakati ambapo aliamini amepokea agizo kutoka kwa Mungu kulirudisha Kanisa katika usafi wake wa asili. Mnamo mwaka wa 1536, akiwa na umri wa miaka 26 tu, alikuwa amekamilisha toleo la kwanza taasisi yake maarugu ya dini ya Kikristo. Toleo la awali lilikuwa na ujazo mdogo wa sura 6. Toleo la mwisho (1560) lilirudiwa zaidi ya miaka kadhaa, na liliongezeka kwa sura themanini. Kiwango cha juu, muonekano wa Calvin, ambao uliendelea katika Afrika Kaskazini (353 – 430 B.K). umeunda misingi ya mafundisho mengi ya waprotestanti wa kisasa.

Katika somo hili, tunategemea kueleza kwa ufupi juu ya ushawishi wa John Calvin juu ya jamii ya kidini kuhusu somo la "Neema". Mawazo yake yanasambazwa katika madhehebu mbalimbali, na kwa kusikitisha, yanaonekana kutafuta njia yao kwa mawazo ya baadhi ya watu wetu wenyewe.

Moja ya makosa maarufu ya Calvin ilikuwa ni dhana ya kuwa mtu amezaliwa akiwa amepotoshwa kabisa, akiwa amerithi athari zote na hatia ya asili ya Adamu. Hata watoto wachanga, kwa hivyo, ndani yao

wana mbegu ya dhambi, hakika, asili yao yote ni aina ya mbegu ya dhambi. Kwa hiyo, hawawezi kuwa kitu chochote zaidi ya ufisadi mbele za Mungu. (Institutes ii.1.8). Kwa hivyo, watu wote wamesimama wanahitaji neema ya Bwana. Kutokana na kosa hili la msingi mengine yanajitokeza.

**Neema isiyo na ukomo**

Moja ya jiwe la pembeni la theolojia ya Calvin ilikuwa ni fundisho la imani (ambayo watu wanatakiwa kukubari bila kusaili), na nadharia ya kwamba yote yatokeayo ni maamuzi ya Mungu na binadamu hana utashi nayo; nadharia ya kwamba Mungu ameamua kuwa wengine watakwenda na wengine motoni. Dhana hii ni kwamba. Sambamba na enzi yake mwenyewe, Mungu, kabla ya misingi ya dunia, alitambua ni nani atayeokolewa mapema na ni nani atakayepotea. "Kwa muonekano wa hili, wakati Kristo alipokufa, kifo chake kilikuwa na ufaulu kwa "wateule tu". Dhana hii ya "Upatanisho wenye ukomo". Na kwa hivyo, Neema yenye ukomo, ni mpya kwa mafundisho ya kimaandiko kwamba ni vigumu kwa yeyote aliye na maarifa ya msingi wa Agano Jipya kuikubali.

Sikia ushuhuda wa Paulo, ***"Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa"*** (Tito 2:11). Kwa sababu Mungu aliupenda Ulimwengu mzima (Yohana 3:16), anataka watu wote waokolewe (1Timotheo 2:4) na hataki mtu yeyote apotee (2Petro 3:9), Kristo alikufa kuwa mptanishi wa Dhambi, **sio tu kwa "wateule"** lakini kwa Ulimwengu wote pia (1Yohana 2:2)

**Neema isiyozuilika**

Mafundisho ya Calvin yanahimiza kwamba kwa siri na uendeshaji maalumu wa Roho Mtakatifu, Neema ya Mungu imemwagwa juu ya wateul;r. kwa kuwa kupanuliwa kwa neema hii ni kitendo cha nguvu za Kimungu, haiwezi kuzuiliwa zaidi kuliko uumbaji asili ungeweza kupinga uwezo wa ubunifu wa Bwana.

Walakini, ukweli ni kwamba ingawa neema ya Mungu imetolewa kwa ukarimu, inatakiwa ipokelewe na wenye dhambi. ***"…Twawasihi***

***msiipokee neema ya Mungu bure…"*** (2Wakorintho 6:1). Hakika inawezekana kutokupokea kile kilichotolewa (Yohana 1:11).

**Neema isiyo na masharti**

Wafuasi wa mafundisho wa John Calvin wanahimiza kwamba neema ilitolewa kwa wateule Bila masharti. Ikiwa iko hivyo, basi hakuna kitu chochote zaidi ambacho mtu anapaswa kufanya ili aweze kupokea wokovu. Hakuna hata kuamini. Mwandishi mmoja anasema "tunaamini kwamba hakuna kibali chochote kwa mtazamo wa Yohana 3:16 unaoweka imani kama hali ya kufanywa na waliopotea ili waweze kupata maisha ya milele ya Kiroho". Tena tunasoma, "Mungu, pasipo kutumia Injili yoyote ya kibinadamu, ataweza kuwaokoa wapendwa wake wote waliokombolewa katika kila nchi na katika kila zama.

Paulo alisema kwamba ***"Tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii"*** (Warumi 5:2). Katika mjadala wake juu ya Neema katika Tito 3, Mtume aliyevuviwa alisema kwamba Mungu, kutokana na rehema zake, alituokoa kupitia ***"kuoshwa kwa kuzaliwa mara ya pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu… ili kuhesabiwa haki kwa neema yake" (5-7).*** Paulo analinganisha kuwa ***"kuokolewa kwa kuoshwa kwa kuzaliwa mara ya pili pamoja na kuthibitishwa kwa neema"***. Pamoja na ***"kuhesabiwa haki kwa neema."*** Kuoshwa ni dokezo la mwitikio wa mtu kwa Mungu kukubali kubatizwa. Neema inetolewa na Bwana, kujitegemea kwa ustahili kwa sehemu yetu. Ni wazi, ingawa, "***kuoshwa kwa kuzaliwa mara ya pili"*** ni **sharti** la ukombozi wetu. Bado, Je, hiyo ndio dokezo la ubatizo? Hata Calvin alikubali kwamba hakuwa na shaka kwamba Paulo alikuwa akidokeza kuhusu ubatizo, ingawa alipinga muunganiko kati ya ubatizo na wokovu.

**Neema isiotenguka**

Calvin alishikilia kwamba wateule wangekuwa na hakika kwamba Mungu kamwe atawaruhusu waanguke kutoka kwenye imani. Hivi wangevumilia mpaka mwisho. Sehemu kubwa ya Uprotestanti imepitisha mafundisho hayo kwa kiwango Fulani au nyingine.

Walakini, Agano jipya linafundisha vinginevyo. Mwana wa Mungu anaweza kuanguka kutoka kwenye Neema. (Wagalatia 5:4) au aklashindwa (kurudi nyuma) mbali ni upendeleo wa bwana (Waebrania 12:15). Inawezekana kumkataa kiongozi aliyekununua, na hivyo kuharibiwa (2Petro 2:1). Kwa hivyo, tunapaswa kujiweka sisi wenyewe ndani ya upendo wa Mungu (Yuda 21) kujitahidi zaidi kufanya imara kuitwa kwetu na uteule wetu (2Petro 1:10), isije ikawa mapokezi yetu ya Neema ya Kimungu yamekuwa bure. (2 Wakorintho 6:1).

**Hitimisho**

Wakati tunapopongeza kwamba John Calvin alifndisha ukweli baadhi, pia tnapaswa kutambua kwamba, alitetea makosa mengi. Makosa hayo lazima yakataliwe.

**Wayne Jackson ni mhariri wa Christian Courier na anaishi huko Stockton, Califonia, Marekani.**

# Wazo la Haraka katika Aya ya Msingi

## 2 Wakorintho 6:11 - 18

**11 Vinywa vyetu vimefumbuliwa kwenu, enyi Wakorintho; mioyo yetu imekunjuliwa.**
**12 Hamsongwi ndani yetu, bali mwasongwa katika mioyo yenu.**
**13 Basi, ili mlipe kadiri ile mliyopewa (nasema nanyi kama na watoto), nanyi pia mkunjuliwe mioyo.**
**14 Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza?**
**15 Tena pana ulinganifu gani kati ya Kristo na Beliari? Au yeye aaminiye ana sehemu gani pamoja na yeye asiyeamini?**
**16 Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, ya kwamba, Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu.**
**17 Kwa hiyo, Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha.**
**18 Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike,**

### Maandiko yanasema nini kuhusu Wakristo na wasio Wakristo kuchangamana?

Wakati fulani mtu anatii Injili, na mume au mke hafichwi. Kama 1 Petro 3:1 anavyosema, ndoa na itunzwe, na kuomba ili kielelezo cha uaminifu kiweze kumpata yeye asiyeamini.

**Maneno haya** ni kwa wale wasio wanandoa, wanaotafuta wenza. **Mst. 12** ni onyo kwamba mapenzi yetu yanaweza kuleta vikwazo katika maisha yetu. **Mst. 13** unatuambia tuwe na akili zilizofunguka kwa yafuatayo:

Ndoa iliundwa ili iwe muungano wa nusu kwa nusu wa kitu kizima: **mwanaume + mwanamke = binadamu kamili – kimaumbile, kihisia, kiakili, kijamii, na KIROHO.** Kama hakuna muungano wa kiroho, hakuna muungano wowote unaoweza kukamilika. Hakutakuwa na kufanana kwa mawazo, thamani, hakuna umoja katika vipaumbele vya muungano, na bila shaka hakutakuwa na umoja wa kiroho. Utofauti umeoneshwa katika **mst. 14** baina ya haki na uasi, baina ya nuru na giza, na katika **mst. 15** inaweka wazi utofauti baina ya Kristo na Shetani, baina ya aaminiye na asiyeamini.

Kwanini ni muhimu sana kwamba kuwe na umoja wa kiroho katika ndoa? Kwa sababu *miili yetu* ni hekalu la Mungu aliye hai, na ameahidi kuishi ndani yetu na kuwa Baba yetu. ***Pindi mke na mume wanapukwa wameungana vizuri na Mungu, ndoa yao hubarikiwa sana.***




**Paul Holland**

Adoniram Judson alikuwa mmisionari wa madhehebu ya Wabaptisti kwa miaka kadhaa iliyopita. Alisema, “Ni makosa kudhani kuwa goigoi na mtu wa kiwango cha pili anafaa sana kwa upagani. Aliye dhaifu zaidi ndiye anayetuhitaji zaidi. Mungu alitoa kilicho bora, Mwanawe wa pekee, ili kwamba auokoe ulimwengu uliopotea. Roho zilizotiwa giza na kudhalilika ndizo zinazohitaji kufikiriwa zaidi.”

Ulimwengu umepotea. Wanaume na wanawake, familia, watoto wadogo na vijana kote ulimwenguni wako katika dhambi na, wamepofushwa na dini zao wenyewe, hatima yao ni maangamizi ya milele. Msaada mkubwa tunaoweza kuwapa unatoka katika Injili ya Yesu Kristo.

Wakati tunapanga na kuomba kwa ajili ya uongofu wa roho zilizopotea, tusiache kutazama eneo kubwa la kazi. Kuna mtu hivi karibuni aliniambia, **“Wewe kama si mmisionari basi ni shamba la kazi.”** Uinjilisti ni Ukristo katika vitendo. Vance Havner alisema, “Uinjilisti katika Ukristo ni mishipa ya miili yetu. **Ukiukata Ukristo popote pale basi utavuja Uinjilisti.** Uinjilisti ni mishipa ya damu; ni kazi yetu. Ukizungumzia uinjilisti ni suala kuu, kama ambavyo unaweza kusema kuhusu uponyaji lilivyo jambo kuu kwa Daktari, hiyo ndiyo kazi yetu.”

Takribani 95% ya wahubiri wa makanisa ya Kristo wanaishi Marekani [hii ni sawa na kusema wahubiri wengi hupenda kuishi mjini], lakini kuna nchi 190 katika ulimwengu wanaohitaji waalimu wa Injili. Vikundi vingine vya kidini ambavyo vinaeneza uongo wanaona hii kama fursa ya kupata wanafunzi. Kanisa la Bwana ni lazima liwafikishie ukweli watu hao. Dunia inahitaji uwazi. Hifadhi ya taarifa za Kikristo Ulimwenguni (WCD) inakadiria kuwa kuna madhehebu ya "kikristo" 9,000 katika ulimwengu [kwa sasa ni zaidi ya hapo]. Hiyo ni aibu kwa kukosa utauwa.

Bila shaka watu wengine wa kidini wanatuangalia na kusema, "Unawezaje kutarajia niwe Mkristo wakati ninyi Wakristo hamwezi hata kukutana na kuamua juu ya nini hasa Ukristo uhusike nacho?" Miguu yetu inahitajika ijikite katika Neno la Mungu na tujue ya kwamba tunajua kile tukijuacho. Halafu tunapaswa kupeleka Injili katika ardhi za kigeni. "Yu tayari kwenda au tayari kukaa, tayari kuijaza nafasi yangu. Tayari kwa huduma, duni au kuu. Tayari kufanya mapenzi Yake." Je, tuko tayari?

Inawezekana kujifunza lugha ya kigeni. Hakuna miungoni mwetu katika timu yetu ya kazi aliozaliwa na ufahamu wa lugha. Ilituchukua masaa na masaa kujifunza. Upendo wa Kristo na upendo kwa watu hatukujua ya kwamba ulitusukuma. Inawezekana kujifunza utamaduni wa kigeni. Ndiyo, wanafanya vitu kwa njia tofauti huko, lakini kwa kawaida kuna sababu ambayo mara nyingi hatuelewi mwanzoni.

Katika kipindi hiki cha teknolojia ya leo, ni rahisi sana kuwasiliana na familia na marafiki kuliko ilivyokuwa katika miaka iliyopita. Kamera zinatufanya tuweze kuonana hata kama tumetengana kwa maelfu ya maili. Mambo mengi tunayoyafurahia kwetu yanapatikana kwa mtindo fulani maeneo mengine ya dunia. Inawezekana kuishi na kustawi nje na nyumbani!

Tafakari kifungu maarufu kuhusu Yesu akifanya kazi ya umisheni na dhabihu aliyoitoa kwa ajili yetu, ***"ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana***

***utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba."*** (Wafilipi 2:6-8).

Unapaswa kufanya kazi ya umisheni. Unaweza kufanya kazi ya umisheni. Je, utafanya kazi ya umisheni?

**Paul Holland anafanya kazi na Kanisa la Kristo Swartz Creek huko Swartz Creek, Michigan, Marekani**

# Kupanda Mbegu ya Ufalme

**Eddie Cooper**

Huenda umewahi kusikia hadithi ya kijana mmoja aliyetaka kuimba wimbo wa kaka yake mjinga. Mama yake alimwuliza kuwa wimbo ulikuwa na kitu gani kuhusiana na hilo. Akajibu, "je, wewe unapanda mbegu ya kaka mfalme mjinga." Hicho sicho kilichonifanya nilete makala hii. Nilidhani kwamba wengine wanadhani kwamba kupanda mbegu ya ufalme si muhimu sana, lakini kupanda mbegu ndiyo kazi kuu kuliko kazi zote.

Soma katika Mathayo 13:24-30. Katika muhtasari wa mithali hii, Yesu anauita ulimwengu kuwa ni shamba ambalo ndani yake mbegu njema zimepandwa. Hata hivyo, wakati watu walipolala, adui akaja na kupanda magugu miungoni mwa ngano kisha akaenda zake. Hivyo ndivyo Shetani anavyofanya kazi. Mambo yote mazuri tunayoyafanya Shetani analeta upinzani ili kuyashinda. Angalia katika mfano hata ingawa mbegu njema zilikwisha pandwa, lakini Shetani bado alifanya kazi yake chafu. Swali linalokuja akilini mwangu ni hili, "Je, tumeacha kupanda mbegu ya ufalme? Je, tumesahau kazi yetu katika kanisa?"

Hivi punde nilikumbushwa, sikiliza hotuba ya Injili, ambayo mara nyingi tunadharau mafundisho ya Kristo. Mafundisho yake ni halisi, matakatifu na mema. Maneno yake yanaleta uzima, tabia njema, heshima na kufanana na Mwalimu. Nguvu ya mbegu inaonekana katika ukweli kwamba maisha ya watu yamebadilika kuwa mazuri. Watu wanaweza kuwa wanyenyekevu, wakweli, wenye upendo, wasaidiaji, wanaosanehe na wema. Wanapaswa kuwa, kulingana na mafundisho ya Yesu, ***"Nuru ya ulimwengu"*** (Mathayo 5:16) na ***"chumvi ya ulimwengu"*** (Mathayo 5:13).

# Ukimya Usiowezekana

John Gipson

Je, mtu anapaswa kubaki na dini yake? Je, unadhani ni "jambo baya" kuzungumzia dini?

Wengi wetu wakati mmoja au mwingine tumejikuta tukitakiwa kushughulika na mtu fulani ambaye alitumia busara kidogo katika ushawishi wake. Kulifanya jambo hili kuwa jepesi, wakasababisha machukizo zaidi. Kwa hiyo huenda tangu hapo tuliamua kwamba tangu sasa tutakuwa kimya kuhusu Ukristo wetu.

Kama huo ndio umekuwa uchaguzi wetu, basi tumefanya kosa kubwa. Kwanini? Kwa sababu hilo ni kinyume cha kuwa Mkristo. Tunayo amri kutoka kwa Yesu kusonga mbele, na hiyo inahusisha kufundisha mataifa yote jambo ambalo Wakristo wa awali walilifanya kwa shauku. Kuwa kimya hakukuwa, na hata sasa halina mjadala (Mathayo 28:18-20).

Mitume iliwabidi kupambana na mamlaka zilizowaambia ***"…wasiseme kabisa wala kufundisha kwa jina la Yesu."*** Tumtii Mungu au mwanadamu? Hilo ndilo lilikuwa swali. Mungu alisema nena; mwanadamu alisema kaa kimya. Unakumbuka jibu lao? ***"Petro na Yohana wakawajibu wakawaambia, Kwamba ni haki mbele za Mungu kuwasikiliza ninyi kuliko Mungu, hukumuni ninyi wenyewe; maana sisi hatuwezi kuacha kuyanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia."*** (Mdo 4:19-20).

Tunatakiwa kushukuru kwa uamuzi wao. Kama vile bwana As H.G. Wells aliwahi kusema, "Shida ya watu wengi sana ni kwamba sauti za majirani zao zinasikika sana katika masikio yao kuliko sauti ya Mungu."

Kumbuka mwenendo wa Wakristo wa awali wakati walipokuwa wakiteswa kwa sababu ya imani yao. Walitawanyika, lakini hawakubaki kimya. ***"…wakaenda huko na huko wakihubiri neno."*** (Mdo 8:4). Sisi pia, tunatakiwa kuelewa kwamba tumeungana na Mungu katika kusudio la kiungu na ***"…hatuwezi kuacha kuyanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia."***

**John Gipson anafanya kazi na Kanisa la Kristo Windsong huko Little Rock, Arkansas, Marekani.**

# Wakristo Wote ni Watumishi wa Bwana

**Dale Grissom**

Inaonekana kuwa ni vigumu kwa baadhi ya Wakristo kujifikiria wenyewe kama ni watumishi wa Mungu. Wakristo wote ni watumishi; hivyo ni wahudumu. Tumefanya tofauti kubwa baina ya watumishi wanaohubiri Injili na kupokea posho kutoka katika kanisa, na ndugu wasiopokea posho kutoka katika kanisa. Nadhani hii ni moja ya sababu ambayo wengi hawakubari jukumu la kuwa wavunaji wa roho.

Uinjilisti binafsi ni kazi iliyokuja yenyewe katika kipindi ambacho kanisa la awali kanisa la Yerusalemu lilipokuwa likiteswa. Tunasoma kuhusu hili katika Mdo 8:3-4. ***"Sauli akaliharibu kanisa, akiingia kila nyumba, na kuwaburuta wanaume na wanawake na kuwatupa gerezani. Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno."*** hii ndiyo sababu kanisa la awali lilikua kwa haraka sana.

Kipindi cha miaka 30 ya mwisho [hivi karibuni, tumekuwa kama kanisa la awali katika kuzileta roho kwa Kristo. Kwa miaka mingi nyuma ya kipindi hiki, tulikuwa na mazungumzo machache sana hisipokuwa katika mikutano ya Injili, katika wakati ambao watu kadhaa waliitii Injili. Shukrani, kwa sababu sasa tunafanya uinjilisti kipindi chote cha mwaka, tukitambua umuhimu wa utii.

Paulo, akiongea na wazee wa Efeso kabla hajaondoka kwenda Yerusalemu, alisema katika Mdo 20:20, ***" ya kuwa sikujiepusha katika kuwatangazia neno lo lote liwezalo kuwafaa bali naliwafundisha waziwazi, na nyumba kwa nyumba,"*** Paulo aliweka kielelezo kwa sisi kukifuata. Lazima tufundishe katika jumuiya na nyumba kwa nyumba ikiwa tunatarajia kuwafikia watu katika jamii zetu kwa Injili. Kazi binafsi ndiyo njia yenye ufanisi zaidi ya kuzifikia roho zilizopotea. Wengi wangeweza kufanya kazi kwa njia hii kwa ajili ya Bwana kama tu wangeamini kuwa wanaweza.

**Dale Grissom (1927-2014) alijitoa kwa uinjilisti binafsi na alikuwa akifanya kazi na kanisa la Kristo huko Dexter, Missouri, Marekani.**

# Chapa za Yesu

**Jim R. Everett**

Mwili ulipigwa kwa mawe na kuachwa, kwa muonekano wote wa nje ni kama ulikuwa mfu katika kiunga cha mji wa Listra. Muda mfupi kabla ya kupigwa kwa mawe, mtu huyu alitukuzwa na kutangazwa kama mungu, lakini alikataa kuabudiwa na wenyeji. Yeye pamoja na Barnaba waliwazuia kwa shida kwa jambo ambalo halikutakiwa wala kustahili kuabudiwa kama miungu. Badala ya kukubari kuinuliwa kama mungu, alijaribu kuwaongoza kwa Mungu mmoja pekee na wa kweli, ***"Lakini hakujiacha pasipo ushuhuda,.."*** (Mdo 14:17).

Wayahudi ambao Paulo aliwaghadhabisha kule Antiokia walifanya hili kuwa jukumu lao kusafiri kwa maili 130, pamoja na Wayahudi waliokasirishwa, wa Ikonia kuwachochea watu wa Listra. Hawakujisikia kutosheka kwa Paulo na Barnaba kufukuzwa kutoka ndani ya miji yao , ila walitaka Paulo "atiwe alama" kuhubiri juu ya Yesu.

Baadaye, Paulo alielezea makovu yake ***"…kwa maana ninachukua mwilini mwangu chapa zake Yesu."*** (Wagalatia 6:17). Uzoefu wa Paulo haukuwa tofauti na mtu mwingine ambaye alivumilia maumivu na kuidharau aibu, lakini akitazama mbari zaidi ya mateso ya msalaba ambayo ili wanadamu waweze kupatanishwa na Mungu (Waebrania 12:1-2). Mwili wa Yesu alibeba alama za misumali katika mikono na miguu yake, na mkuki wa Kirumi katika ubavu wake uliochomwa. Sababu ya Paulo kuyaita makovu aliyoyabeba ***"chapa za Yesu"*** ni kwa sababu zilikuwa zinatambulika kama alama za haki zilizotokana na Yesu; kwa njia fulani ndogo alishiriki aina ya mateso yale ambayo Yesu aliyastahimili.

Kama wewe ni mwenye haki, mateso yatakuja (2 Timotheo 3:12). Kwa mtindo wowote yatakayochukua, usitishwe na adui. Badala yake, vaa ***"chapa za Yesu"*** kama askari mwenye kujivuna akionesha medali zake; makovu, huchukuliwa na ulimwengu kama kitu cha aibu, kwa kweli yanatakiwa kuchukuliwa na Wakristo kama ushahidi wa ushujaa.

**Jim R. Everett alikuwa mzee na mhubiri katika kusanyiko la Cedar Park, Texas**

# Kupanua Uzio

**Olden Cook**




Alipoulizwa kuhusu uamuzi wake katika suala lenye utata mwanasiasa aliwahi kujibu, “Sawa, nina marafiki wanaounga mkono hilo, na ninao marafiki ambao wako kinyume na hilo, na daima usimama na marafiki zangu!” Hivyo, alipanua uzio vizuri.

Watu wengi wapo kama hivi linapokuja suala la Ukristo. Wanasimama kinyume kwa jambo la bure na wako kwa kila kilicho maarufu. Wanajihisi kwamba kwa kupanua uzio hivyo wanaweza kuwa “pande zote mbili”, bila ya kutambua kwamba ***“…kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu…”*** (Yakobo 4:4). Wakristo wanatakiwa waufahamishe ulimwengu kuwa wako upande gani, na kuwa mstari wa mbele kuikabili dhambi, ulimwengu na upotofu.

Kiroho, hakuna nafasi ya katikati. Musa aliwauliza, ***“Nani yuko upande wa BWANA?”*** (Kutoka 32:26). Yoshua aliwapa watu changamoto ***“…chagueni hivi leo mtakayemtumikia…”*** (Yoshua 24:15).

Hauwezi kupanua uzio! Wakati kanisa la Laodikia lilipojaribu, Yesu alisema kwamba angewatapika watoke katika kinywa chake (Ufunuo 3:16).

**Olden Cook alikuwamhubiri kwa miaka kadhaa.**



# Unapimaje?

**Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu. Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi; siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu. Kwa maana sisi tulio hai, siku zote twatolewa kufe kwa ajili ya Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu ipatikananyo na mauti. Basi hapo mauti hufanya kazi ndani yetu, bali uzima ndani yenu. Lakini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani; kama ilivyoandikwa, Naliamini, na kwa sababu hiyo nalinena; sisi nasi twaamini, na kwa sababu hiyo twanena; tukijua ya kwamba yeye aliyemfufua Bwana Yesu atatufufua sisi nasi pamoja na Yesu, na kutuhudhurisha pamoja nanyi. Kwa maana mambo yote ni kwa ajili yenu, ili neema hiyo ikiongezwa sana, kwa hao walio wengi shukrani izidishwe, na Mungu atukuzwe. Kwa hiyo hatulegei, bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku. Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele.**

**2 Wakorintho 4 : 7 – 18**

# Ibada Inayokubalika

**John Thiesen**

Ni aina gani ya ibada inayokubalika kwa Mungu? Au, inaleta badiliko lolote kwa Mungu kwa namna tunavyomwabudu? Yesu, akiwa katika mazungumzo na mwanamke wa Samaria, alifafanua aina ya ibada inayompendeza Mungu na hivyo anatafuta hilo katika watu: ***"Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli."*** (Yohana 4:24).

## Ibada Ambayo Ni Halisi na Kweli

Miungoni mwa mambo mengine ambayo inawezekana kujifunza kutoka katika maneno ya Yesua hapo juu, iko wazi sana: ibada, ili ikubalike na Mungu, ni lazima iwe halisi, ikitoka katika roho (au moyo) wa aabuduye, na ni lazima itokane na kweli ya Mungu. Waabuduo wa jinsi hiyo ni wa ***"tohara"*** ya kweli (watoto wa Ibrahimu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu). Mtume Paulo alisema, "***Maana sisi tu tohara, tumwabuduo Mungu kwa Roho, na kuona fahari juu ya Kristo Yesu, wala hatuutumainii mwili."*** (Wafilipi 3:3).

## Kwa Unyenyekevu na Uchaji wa Mungu

Kwa Mungu kuisikia ibada yetu, lazima tumsogelee kwa unyenyekevu. ***"Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa, na mwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho; maana Mungu wetu ni moto ulao."*** (Waebrania 12:28-29). Hii inamaanisha kwamba tunatakiwa kumwabudu Mungu huku tukitambua kwamba tuko kwenye uwepo wa Mwenyezi, Bwana Mungu. Wakati wa kumwabudu, akili zetu ni lazima zimwelekee yeye pekee. Mambo yote yasiyo na maana katika maisha ya kila siku, biashara, na starehe lazima tuziweke kando wakati mioyo yetu iko chini ya uangalizi wa Mwenyezi. Kama Musa, alivyovua viatu katika kichaka kilichokuwa kikiwaka moto kwa sababu alikuwa katika ardhi takatifu, sisi pia tupo katika ***"ardhi takatifu"*** tunapojihudhurisha mbele za Mungu pamoja na tunda la dhabihu ya midomo yetu. Lazima tuyaache mambo ya kidunia ya kuharibu na ya kuangusha mioyo yetu na akili mbele za uwepo wa Bwana wa milele.

# Uzuri na kwa Utaratibu

Utaratibu ni kipengele kingine cha ibada ambacho kinakubalika na Mungu ***"Lakini mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu."*** (1 Wakorintho 14:40). Haipaswi kuwe na mkanganyiko wo wote unaotokana na kelele, mwingiliano au watu kuzungumza kwa muda mmoja, kwa kuwa dhumuni moja la kukusanyika ni kujengana (kufundishana) kwa kanisa (Aya ya 26).

# Unyenyekevu

Kipengele kingine muhimu cha kufanya ibada inayokubalika na Mungu ni unyenyekevu ***"…Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema."*** (1 Petro 5:5). Kielelezo cha hili kimetolewa na Yesu katika mfano wake juu ya Mfarisayo na Mtoza ushuru waliokwenda Hekaluni kusali. Farisayo, katika sala yake kwa Mungu, aliorodhesha mambo yake yote yenye ubora mzuri, akishukuru kwamba yeye si mtenda dhambi kama watu wengine, na alijipongeza kwa kufunga kwake na kuwa mwangalifu kwa kutoa zaka ya vitu vyote

alivykuwa navyo (Luka 18:11-12). Mtoza ushuru, kwa upande mwingine, aliinamisha kichwa chake kwa aibu, akijipigapiga kifuani mwake na kuomba ***"…Ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi."*** (Aya ya 13).

Yesu alisema kwa mtoza ushuru, "***…huyu alishuka kwenda nyumbani kwake amehesabiwa haki kuliko yule; kwa maana kila ajikwezaye atadhiliwa, naye ajidhiliye atakwezwa."*** (Aya ya 14).

### Ibada

## Utekelezaji

Na tupambane kumwabudu Mungu kwa uhalisia na kwa moyo wote, tukimnyenyekea kwa hofu ya kimungu, katika utaratibu na unyenyekevu, roho ya toba. Kama tukifanya hivi, tunaweza kuwa na ujasiri kwamba Mungu atasikia maombi yetu na kuikubali ibada yetu.

**John Thiesen (1934-2000) alijihusisha na kutafsiri kwa Kiispania The Voice of Truth International na alitumika kama mmisionari kwa miaka mingi nchini Malawi.**

## Ibada

# Tabia Nne Kuelekea Utoaji

**Wade Webster**

Nilipokuwa mwanafunzi katika Shule ya Mahubiri ya Memphis. James Dearman, mmoja wa wakufunzi wangu, alitoa muhtasari darasani kwetu juu ya kutoa ambao nimeutumia kwa miaka kadhaa. Muhtasari ulitokana na maelezo ya Daudi aliyoyasema kwa Arauna pindi alipojitolea kumpatia mfalme kiwanja cha kupuria na vyote vilivyohitajika kwa ajili ya mfalme kutoa dhabihu kwa BWANA. Kifungu kinasomeka, "***Lakini mfalme akamwambia Arauna, La, sivyo; lakini kweli nitavinunua kwako kwa thamani yake; wala sitamtolea Bwana, Mungu wangu, sadaka za kuteketezwa nisizozigharimia. Hivyo Daudi akakinunua hicho kiwanja cha kupuria na wale ng'ombe kwa shekeli hamsini za fedha."*** (2 Samweli 24:24). Kutoka katika kifungu hiki, ndugu Dearman alitoa tabia nne ambazo mtu mmoja mmoja mara nyingi huonesha kuelekea utoaji.

**Tabia ya kwanza - "Sita toa."** Jamaa wengi kirahisi tu hawako tayari kutoa. Wao ni bahili wa kiroho.


**Tabia ya pili – "Sita mtolea Bwana."** Marafiki wengine wako tayari kutoa, lakini hawako tayari kumtolea Bwana. Wako tayari kutoa

kwenye klabu hii na kwa jambo lile, lakini hawako tayari kutoa kwa ajili ya Bwana.

**Tabia ya tatu – "Sita toa kwa Bwana kile ambacho kitanigharimu."** Baadhi ya marafiki, wako tayari kumtolea Bwana, lakini hawako tayari kumtolea kitu cho chote ambacho kitawagharimu. Watampa chakavu, lakini si kilicho bora.

**Tabia ya nne – "Sitamtolea Bwana kitu ambacho hakinigharimu kitu."** Kuna wale wanaojitoa dhabihu katika kutoa. Wanatoa vitu ambavyo wengine wanafurahia ili kwamba waweze kumtoloa zaidi kwa Bwana.

Tabia gani inayokuwakilisha wewe vizuri na utoaji wako? Je, unagoma kabisa kutoa, au **IBADA** je, kirahisi tu unagoma kumtolea Bwana? Je, unatoa vilivyochakaa, au unatoa vile vinavyokugharimu? Ninakutia moyo uwe kama Daudi na kutoa kile tu kinachokugharimu.




***"Basi, nataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata pasipo hasira wala majadiliano."*** (1 Timotheo 2:8). Katika aya hii, ilimaanishwa nini kwa kusema ***"..huku wakiinua mikono iliyotakata.."?*** watu wengi wanaweka mkazo katika neno ***"mikono"*** na kuwa na fikra kwamba Paulo anaelezea mkao wa mtu pindi anaposali. Hata hivyo, si kile ambacho watu wanafanya kwa mikono yao ambacho Paulo alikuwa akizungumzia katika aya hii, bali ni hali ya mioyo na maisha yao.

Katika Biblia yote, imeelezwa mikao mbali mbali wakati wa kuomba: kusimama (1 Wafalme 8:22), kupiga magoti (Danieli 6:10), kukaa (Luka 22:14,17), kulala chini (2 Samweli 12:16), kunyanyua mikono (Nehemia 8:6), bila kunyanyua mikono (Mathayo 26:39), kuukabili ukuta (2 Wafalme 20:2), kuinamisha kichwa (Kutoka 4:31), kutazama juu (Yohana 17:1) n.k. Ni hakika ya kwamba hakuna maelekezo yo yote ya mkao kwa ajili ya sala. Mkao wa mwili wa mtu haujalishi kwa Mungu, bali ni hali ya moyo wa mtu ndicho kinachojalisha Kwake "***Na aache mabaya, atende mema; Atafute amani, aifuate sana. Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, Na masikio yake husikiliza maombi yao; Bali uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya."*** (1 Petro 3:11,12).

Kwa kuwa mtu anatumia mikono yake kwa karibu shughuli zote za kimwili (**kazi**, 1 Wathesalonike 4:11; **kupigana,** Zaburi 144:1; n.k.), mikono inaashiria vitendo vya mtu (Mwanzo 16:2; Mathayo 6:3; Marko 9:43). Matendo ya mtu (mazuri au mabaya) moja kwa moja yanahusishwa na hali ya moyo wake (Mathayo 12:34-35; Marko 7:20-23). Wenye hatia ya dhambi wanasemwa kuwa wana mikono iliyochafuka (Isaya 1:15; Ezekieli 3:18,20; Yakobo 4:8), na hivyo kuondoa dhambi kutoka katika moyo/maisha ya mtu mmoja mmoja inaashiliwa kama kuosha "**mikono"** (Kumbukumbu la Torati 21:6-9; Zaburi 26:2; Yakobo 4:8). Wakati Pilato alipotaka kutangaza kuwa hana hatia katika kumhukumu Yesu ***"…akanawa mikono…"*** (Mathayo 27:24). Daudi aliandika, "***Bwana alinitendea sawasawa na haki yangu, Sawasawa na usafi wa mikono yangu akanilipa."*** (Zaburi 18:20).

Katika Biblia, mtindo wa kunyanyua mikono katika maombi kunaashiria ukweli kwamba mtu huyo alikuwa akimtolea Mungu maisha safi, na hivyo maombi yake hayapaswi kuzuiliwa. Mikono ya mtu inyanyuliwe au isinyanyuliwe, michafu au safi, haihusiani kwa lo lote na kukubalika kwa maombi yake. Ni hali ya moyo na maisha ya mtu mmoja mmoja ndivyo vinavyojalisha kwa Mungu. Dhambi (uchafu wa roho) ndiyo inayofanya maombi ya mtu kuzuiliwa (Isaya 59:1,2; Zaburi 66:18), na sio hali au mkao wa mikono ya mtu. Mungu alimwongoza Isaya kuandika, ***"Nanyi mkunjuapo mikono yenu, nitaficha macho yangu nisiwaone; naam, mwombapo maombi mengi, sitasikia; mikono yenu imejaa damu. Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho yangu; acheni kutenda mabaya;"*** (Isaya 1:15-16). Hivyo, kunyanyua mikono katika sala ni kunyanyua na kuuweka moyo wa mtu, roho na maisha kwa Mungu (Zaburi 63:4; 86:4; Maombolezo 3:41). Kama "mikono" yako ya kiroho imetiwa doa kwa dhambi, Mungu hatasikia maombi yako (Zaburi 66:18). Hata hivyo, kama mikono ya kiroho ya mtu imesafishwa na dhambi (Zaburi 18:20,24: 24:4), maombi yake yatakubaliwa na Mungu (1 Petro 3:12).

Katika 1 Timotheo 2:8 mkazo haupo katika “mikono”, bali ni ***“mikono iliyotakata”*** Wakati wanaume wakiomba, Mungu anataka mioyo yao na maisha yao kuwa na utakatifu (Warumi 12:1; Waeeso 1:4), bila ya kujali mkao wao wa kimwili. Mwanamume asiye na mikono bado anaweza kukubalika kumwomba Mungu maadamu “mikono” yake ya kiroho ni safi.

**Kevin L. Moore ni Profesa Mshiriki wa Bible & Missions katika Chuo kikuu cha Freed-Hardeman, Marekani na afanya kazi za umisionari huko Porirua, New Zealand.**

## MITHALI 17:22



Ndugu, kama mkeo hajisikii vizuri, fanya kile ninachofanya kumweka sawa mke wangu kwa haraka; mpe msaada wa kufanya kazi za nyumbani. Kama haudhani kuna jambo kama miujiza ya kuweka sawa, basi unaweza kumwona mke wangu akiwa sawa tena kila wakati ninapoanza kusafisha madirisha.



Mwishowe nilipata majibu kwanini nanenepa! Nilitakiwa kujua hili mapema.

Ni sabuni ya nywele ninayoitumia kwenye bomba la mvua. Ninapoosha nywele zangu, sabuni inatelemka mwili mzima. Nembo ya sabuni iko wazi inasomeka, **“Kwa ujazo zaidi na mwili.”**

Nimeachana na sabuni hiyo, na ninaenda kutumia sabuni ya vyombo *Dawn*. Katika nembo yake inasomeka, **“Inaondoa mafuta ambayo vinginevyo ni vigumu kuondoa.”** Tatizo limetatuliwa!



Mtu mmoja alienda kumwona mhubiri. “Mhubiri, kunajambo baya linaendelea, na ninapaswa kuzungumza nawe kuhusu hili.”

Mhubiri akauliza, “Kuna shida gani?” Mtu Yule akajibu, “Mke wangu anaelekea kunipa sumu.”

Mhubiri akishangazwa sana na hili, akauliza, “Hilo linawezekanaje?” Mwanaume akasihi, “Ninakuambia, nina hakika anaelekea kunipa sumu. Nini napaswa kufanya?”

Mhubiri akasema, “Nikwambie nini? Ngoja nizungumze naye na nitaona

nitakachokigundua na kisha nitakufahamisha."

Wiki moja baadaye mhubiri alimwita yule mwanaume na kumwambia, "Nimeongea na mke wako kwa simu kwa masaa matatu. Unataka ushauri wangu?" Mwanaume akasema, "Ndiyo," na mhubiri akajibu, "Ikubali sumu."

Hata sifikiri kulifunua jina lake, lakini mhubiri alilazimishwa kusimama na askari wa barabarani kwa sababu ya mwendo kasi. Askari alipokuwa akimwandikia cheti, mhubiri alimwambia, "Heri wenye rehema; maana hao watapata rehema." Askari akampa cheti mhubiri na kusema, "Enenda zako; wala usitende dhambi tena."

Daktari wa upasuaji alikuwa akimkagua mgonjwa aliyefanyiwa upasuaji wa ngiri siku tatu zilizopita. Daktari alimwuliza, yule mtu kwanini hajaondoka kitandani. "Nina maumivu," yule mwanaume alisema, "Haujui jinsi inavyokuwa."

"Ninajua hasa jinsi inavyokuwa" daktari alisema, "Mwezi uliopita nilipitia hatua hiyo hiyo, na nikarudi kazini siku mbili baadaye. Hakuna utofauti katika upasuaji wetu."

"Ah ndiyo upo," alisema mgonjwa. "Ulikuwa na daktari wa upasuaji tofauti."

Mvulana wa miaka mitano alikuwa na wazazi wake walipokuwa wakishuhudia sherehe ya harusi ya rafiki wa familia.

"Mama," alimnong'oneza, "Kwanini mwanamke amevaa nyeupe?" Mama yake akatabasamu na kumnong'oneza, "Kwa sababu anafuraha sana ya kuolewa."

Kijana akatafakari kwa muda, "Sasa kwanini mwanaume amevaa nyeusi?"


Mtu na mkewe walikuwa na matatizo nyumbani na

walinyamaziana. Wiki iliyofuata, mwanaume aligundua kuwa alikuwa anamuhitaji mkewe amwamshe saa 11:00 asubuhi, awahi ndege kwa ajili ya safari ya kibiashara kuelekea Chicago. Huku akitaka kutokuwa wa kwanza kuvunja ukimya (na kupoteza), akaandika kwenye kikaratasi, "Tafadhali niamshe saa 11:00 asubuhi."

Asubuhi yake mume aliamka, na kugundua kuwa ilikuwa saa 3:00 asubuhi, na hivyo aliikosa ndege yake. Akaghadhabika, alitaka kunyanyuka na aone kwanini mke wake hakumwamsha akaona kikaratasi kitandani. Karatasi ilisema, "Ni saa 11:00 asubuhi. Amka."



Kulikuwa na mwungwana katika kitanda hospitalini kando yangu.alikuwa amefunikwa kwa bandeji kutoka kichwani hadi kidole cha mguu. Nikasema naye, "Unashughulika na nini katika maisha?" Akasema, "Awali nilikuwa mwosha madirisha." Nikauliza, "Lini uliiacha?" Akajibu, "Nusu kushuka chini."




**Wayne Barrier**

Umbo la nje si imara kama msingi wake. Tunakumbushwa ukweli huu pindi matetemeko ya ardhi yanapotetemesha ardhi na majengo kupolomoka. Kanuni hii pia inatumika katika maisha yetu. Yesu alifundisha katika Mathayo 7:24-27,

> ***"Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa."***

Yesu alikuwa akihitimisha Hotuba yake nzuri ya Mlimani, iliyorekodiwa katika Mathayo 5-7. Sura hizi zinarekodi ya muhtasari wa nguvu wenye mafundisho pacha ya Ukristo. Yesu alitoa mwongozo muhimu na amri ambazo zikifuatwa huleta matokeo ya maisha ya

utauwa ambayo yanahakikisha ustawi wetu wa kiroho na utiifu kwa Mungu. Paulo akirejea mafundisho ya Kristo kama msingi wa maisha aliandika katika 1 Wakorintho 3:11, ***"Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani Yesu Kristo."*** Baadhi ya vipengele muhimu vya hotuba hii nzuri ambavyo vinaunda msingi wa mwamba ikijumuisha yafuatayo;

- **Mathayo 5:1-12** Maskini wa roho, wenye huzuni, wenye upole, wenye njaa na kiu ya haki, wenye rehema, wenye moyo safi, wapatanishi na watumishi wa Mungu huko ni kuudhiwa kwa ajili ya haki wana heri na kibali.
- **Mathayo 5:21-30** Dhambi huja kutoka katika mioyo yetu, tabia zina akisi mioyo yetu.
- **Mathayo 65-13** Mungu atajibu maombi ya watoto wake.
- **Mathayo 6:19-21** Hazina ya mtu katika maisha haiwekwi duniani, badala yake, inakusanywa mbinguni.
- **Mathayo 6:33-34** Ni lazima tutafute kwanza ufalme wa mbinguni na haki ya Kristo. Tunapofanya hivi, Mungu atatupatia mahitaji yetu ya kila siku.
- **Mathayo 7:13-14** Njia ya mbinguni ni nyembamba na ngumu, na njia ya maangamizi ya milele ni pana na rahisi.
- **Mathayo 7:15-20** Iweni waangalifu na waalimu wa uongo.
- **Mathayo 7:21-23** Ni wale pekee wanaojua na kufanya mapenzi ya Baba watakaookoka.

Kuna mafundisho mengine mengi katika hotuba hii. Soma na ujifunze kila mstari wa Mathayo 5-7 ujifunze jinsi ya kujenga maisha yako juu ya msingi imara. Ulimwengu umejazwa kwa mabilioni ya watu na maisha yaliyoshikana. Kushindwa kwa mwisho ni kifo pindi unapokuwa nje ya mwili wa Kristo. Je, umejenga maisha yako juu ya msingi wa aina gani?

**Wayne Barrier anaishi huko Florence, Alabama, Marekani, na anafanya kazi za umisionari katika nchi mbali mbali.**

# Changamoto Yetu

**Greg Tidwell**

> ***"Na kwa malaika wa kanisa lililoko Thiatira andika; Haya ndiyo anenayo Mwana wa Mungu, yeye aliye na macho yake kama mwali wa moto, na miguu yake mfano wa shaba iliyosuguliwa sana. Nayajua matendo yako na upendo na imani na huduma na subira yako; tena kwamba matendo yako ya mwisho yamezidi yale ya kwanza."*** (Ufunuo 2:18-19).

Wakati Bwana wetu akiendelea kulionya kanisa lililoko Thiatira kuongeza imani, hongera ambazo alianza nazo katika sehemu hii ni kubwa. Akiwasifu kwa bidii na mshikamano wao, Aliyavisha taji mafanikio yao kwa kusema kirai hiki; ***"matendo yako ya mwisho yamezidi yale ya kwanza."*** Kusanyiko la Thiatira lazima lilikuwa na nguvu. Hawakutosheka kukumbatia raha kupita kiasi ya mambo yaliyofanikishwa zamani, walisonga mbele, kufanikisha zaidi kwa ajili ya Kristo.

Nguvu kubwa iliyowekwa zamani kwa ajili ya wakati wa sasa. Uzoefu wetu unaweza kutupatia changamoto ya kufika mbali na kufanikisha zaidi kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Kwa bahati mbaya, mara nyingi tunaruhusu zamani iwe kizuwizi badala ya kuwa msaada. Mazoea ya zamani yanaweza kutumika kama kikwazo cha maendeleo. Hatupaswi kuishi katika ushindi au kuanguka kwa zamani katika namna ambayo inaweka ukomo katika ufanisi wetu wa sasa na uwezekano wa baadaye. Badala yake, fuata mfano wa kanisa la Thiatira, tunapaswa kuendeleza tabia ya upendo, imani na huduma ambayo inajenga siku zijazo kuliko kustarehe katika mambo ya zamani.

Sisi ni warithi wa urithi mkuu. Matendo ya wanaume na wanawake waliotutangulia yanapaswa kuheshimiwa na kuenziwa kama kumbukumbu ya mafanikio yenye nguvu. Yanapaswa kutusongesha mbele. Changamoto yetu ni kujenga juu ya urithi ili kwamba matendo ya mwisho yazidi ya kwanza.

**Greg Tidwell ni mhubiri wa Kanisa la Kristo Fishinger na Kenny huko Columbus, Ohio, Marekani, hali kadhalika anahudumu kama Mhariri Wakili wa Injili.**

# Hayo ndiyo Maisha

**Carroll Sites**

***"Haya basi, ninyi msemao, Leo au kesho tutaingia katika mji fulani na kukaa humo mwaka mzima, na kufanya biashara na kupata faida; walakini hamjui yatakayokuwako kesho. Uzima wenu ni nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo, kisha hutoweka. Badala ya kusema, Bwana akipenda, tutakuwa hai na kufanya hivi au hivi. Lakini sasa mwajisifu katika majivuno yenu; kujisifu kote kwa namna hii ni kubaya. Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi."*** (Yakobo 4:13-17).

Hatukuwa na lo lote la kusema pindi tulipozaliwa katika maisha haya. Hatujui muda ambao tutayaacha maisha haya katika kifo. Kwa hiyo, kipaumbele cha kwanza ni muda uliopo baina ya kuzaliwa na kifo.

Sehemu fulani nilisoma, "Maisha ni sanaa ya uchoraji bila ya kifutio." Makosa yaliyofanywa zamani, vitu tulivyovifanya ambavyo hatukupaswa kuvifanya na vitu tulivyoacha kuvifanya ambavyo tulipaswa kuvifanya haviwezi kubadilishwa. Hatuna ufutio, kwa hiyo tufanye nini? Mweke Kristo katika maisha yako, mweke hapo. Pamoja Naye hapo, tunaweza kupata suluhisho la kufanya vizuri kesho na tutafanya.

Peter Marshall aliweka maelezo ya msisitizo mkubwa, "Kama Mungu haingii jikoni kwako, kuna jambo lisilo sawa jikoni kwako. Kama hauko na Mungu katika ubunifu wako, kuna kitu hakipo sawa katika mchezo wako…" Wote tunamwamini Mungu wa ushujaa. Tunachokihitaji zaidi katika siku hizi ni Mungu wa kawaida "mtu wa kawaida" "mtu wa kazi" "mke wa kila siku" "mwenye elimu ya juu," na "asiye na elimu." Pamoja Naye katika maisha yetu, tunaweza kufanikiwa bila kujali nini. Kama Philips Brooks aliwahi kuandika, "Ukristo unatusaidia kuukabili muziki, hata kama hatuipendi tuni yake."

Kwa hiyo, unafanya nini katika maisha? Unaruhusu maisha yafanye nini kwako? Mweke Kristo katika maisha yako leo, na itakuwa tofauti.

**Carroll Sites ni mwinjilisti wa Kanisa la Kristo Higden huko Higden, Arkansas, Marekani.**



# SHETANI

## Je, Unamtambua?

Betty Burton Choate

***"huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu. Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze. Nanyi mpingeni huyo, mkiwa thabiti katika imani, mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani."*** (1 Petro 5:7-9).

Mungu anatuonya kwamba tunaye adui wa mauti ambaye anatafuta kwa bidii kutuangamiza. Katika Maandiko, amefafanuliwa kama "Ibilisi", "Shetani," "Joka," n.k. orodha inaendelea, na tunaelewa hata katika majina ambayo yanaonesha alivyo mwovu. Wasanii, wanachora mawazo yao juu ya mwonekano wake, mara zote anaelezewa kama jitu jekundu la kutisha lenye mapembe, meno ya mnyama na mwenye uma wa kutisha. Ni wazi, wanatumia mchoro na mawazo kutusaidia kuelewa uovu wake wa ndani.

Kutangulia kuonywa kunapaswa kuwe ni utayari, lakini tatizo ni kwamba hakuna mtu anayeliona hilo jitu jekundu, kwa hiyo anauwezo wa kunyata na kuingia na kujificha vizuri na kutengeneza maangamizi katika maisha ya wasioshuku.

Tena, Baba yetu anatuonya; "***Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa-mwitu wakali."*** (Mathayo 7:15). Maneno yanatutahadhalisha katika

ukweli kwamba Shetani sio tu kwamba baba wa uongo (Yohana 8:44), lakini pia ni bwana wa udanganyifu. Anajua kwamba sisi sote tunaweza kumkimbia mbwa mwitu au jitu, lakini ni nani anayeweza kumkimbia kondoo asiye na madhara? Kwa hiyo, nini baadhi vitu zaidi vya kawaida ambavyo Shetani hujificha?

- Mara nyingi huwaendea watu kupitia hamu zao na starehe; bia na pombe nyingine, na madawa ya kulevya yanaleta starehe kubwa kwa watu wengi, na ni pale tu baada ya kupata athari au afya kualibiwa ndipo hutambua ukweli ya kwamba Shetani alikuwa akijificha katika mambo hayo ya kufurahisha. Kwa masikitiko, hata ulafi ni moja ya vifaa vyake. Vyakula, inaonekana ni vigumu sana kuviepuka, na matokeo yake ni kitambi kinachoharibu afya na kupunguza maisha ndiyo gharama Shetani anayoitoza.
- Shetani anaweza akaja katika umbo la tamaa ya kufanikisha lengo kwa njia ya uongo na mambo mengine yasiyo ya kimaadili. Baadhi ya tamaduni zinajiendesha katika mhimili kwamba hakuna mtu awezaye kuaminiwa, ushahidi mkubwa wa udhibiti wa Shetani kwa umma.
- Shetani anaweza kuwatega wahanga katika matope ya tamaa kupitia urembo wa mwanamke fulani au muonekano wa mahaba wa mwanaume fulani, wote wakiweka mikogo katika miili yao kwa lengo moja la kuwavuta watu dhaifu katika uharamu na mazingira yasiyo ya kimaadili.
- Shetabi anatumia “makanisa” bandia na “injili” bandia kuwapofusha watu wasione ukweli. Baadhi ya waalimu wake wengi wenye weledi sio wale wanaohubiri kutoamini katika Mungu bali ni wale wanaodai kuwa ni wahubiri na viongozi, lakini wapo katika dini potofu. Shetani anajua kwamba uhitaji wa Mungu umezikwa katika kina cha kila nafsi, na kwa hiyo, anajaza huo uwazi kwa uongo. Roho iliyodanganywa kwa ujasiri hutembea katika njia pana kuelekea katika mwisho wake ulioahidiwa.

❖ Shetani pia ni mwizi mwenye hila. Anawajaribu Wakristo wamtolee Mungu mabaki ya vipato vyao baada ya kulipia ada mbali mbali na kufunika kujiendekeza kwa mtu. Hulijaribu Kanisa kutumia takribani 95% ya fedha ya Mungu kwa kila hitaji la kawaida {mambo madogo madogo}, kudekeza na ubadhilifu, kuliko katika uinjilisti na kusaidia wahitaji.

❖ Shetani huaribu roho kwa njia ya kutengeneza ugomvi na uadui baina ya ndugu. Wakati mwingine, anatumia utofauti wa haiba kama kabari yake; wakati mwingine hutumia shauku ya ufahari, au tatizo linaweza hata kugeuka kutoka katika Neno la Kweli la Mungu. Lo lote kati ya haya yanaweza kuligawa kanisa, na matokeo yake roho hizo zinaweza kuangamia milele.

❖ Kutumia muda kwenye burudani inaweza kusababisha mauti ya kiroho. Hapana, jaribu la Shetani katika hili si dhambi kwa kitendo chenyewe. Dhambi inakuja kwa sababu burudani inaweza kumwondoa mtu kutoka kwa Mungu na kupoteza muda. Masaa yanatolewa dhabihu kila siku katika runinga, michezo au burudani nyingine yo yote ile inapoiba nafasi ya Mungu. Wakristo watafanya vema kuweka ratiba, kuweka muhtasari wa muda unaotumika katika sala, kusoma, kuabudu na kuwashirikisha Injili wengine katika safu moja, na masaa yaliyotumika katika burudani katika safu inayofuata. Baada ya wiki, linganisha uone kuna uwiano gani?

❖ Moja ya silaha ya Shetani yenye ufanisi ni "kutingwa na shughuli". Wakristo wameachwa ulimwenguni wawe vyombo vya kupeleka Injili kwa waliopotea. Wanajua dhima yao, na wanakusudia kuwa vyombo katika mikono ya Mungu. Hata hivyo, kwanza, vitu elfu vya ulazima vinatakiwa kufanyika, na hivyo siku na majuma yanapita bila ya kubakiwa na muda wa kufanya kazi ya Mungu. Kwa sababu watu wanatingwa katika majaribu haya mengi kwamba hawafanyi dhambi, wanaweza kuendelea na maisha bila ya kutambua ujanja wa Shetani **kuwafanya Wakristo kutingwa na wageni, michezo, usafi, TV, n.k. kwamba kusiwe na muda utakaobaki wa kusoma Neno la Mungu au kuwashirikisha wengine.** Wakati dhamiri inapotingwa, Shetani

anaipoza kwa matarajio ya kesho…

❖ Hatimaye, kila angamizi au kujitoa kokote kwa mtu ambako huchukua nafasi ya kwanza ya cheo cha Mungu katika moyo wa Mkristo ni silaha ya Shetani. Kweli, yeye angependa kila mtu awe mwovu kama yeye alivyo, lakini anajua kwamba wengi wanataka kuwa wema; kwa hiyo, anatosheka na mafanikio yake maadamu ametuliza hali ya watu kujitoa kwa Mungu na kuwa **vuguvugu.** Bado, anashinda.

Ndiyo, Shetani huja kwa njia nyingi, Wakristo wanaweza kujilinda wenyewe dhidi ya shambulio lake kwa kuwa waangalifu, wakivaa silaha zote za Mungu.

> ***"Basi simameni, hali mmejifunga <u>kweli</u> viunoni, na kuvaa dirii ya <u>haki</u> kifuani, na kufungiwa miguu <u>utayari tupatao kwa Injili ya amani</u>; zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya <u>imani</u>, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya <u>wokovu</u>, na upanga wa Roho ambao ni <u>neno la Mungu</u>; kwa <u>sala zote na maombi mkisali</u> kila wakati katika Roho, <u>mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote;</u>"*** (Waefeso 6:14-18).

**Betty Burton Choate ni mjane wa J.C. Choate, mfanya kazi mwenza katika uandishi na katika kazi za umisionari kwa muda wote wa ndoa yao.**

# Umuhimu wa Malezi ya Nyumbani

**Ferman Carpenter**



**Ni nyumbani ambapo watoto wanapaswa kupokea malezi ambayo yatawajengea msingi wa maisha haya na ya uzima wa milele.** Watoto wetu hawakuomba kuwepo hapa; ndiyomaana wazazi wanawajibika kwa uwepo wao hapa duniani. Kwa hiyo, nyumbani na ushawishi wake utachangia pakubwa kwamba watakuwa na furaha wakati huu na wapi wataishi kwa umilele. Ukweli, kuwa mzazi ni wajibu mzuri.

Ili kufanya kazi ambayo Mungu anataka ifanyike, wazazi lazima waanze mwanzoni kabisa mwamalezi ya maisha kwa watoto wao. Mara nyingi zaidi wazazi husubiri mpaka wakati ambao watakuwa wamechelewa sana, na baadaye wanashangaa kwanini wameshindwa. Somo zuri lililofundishwa na Manoa, baba wa Samsoni, pindi alipojua kwamba yeye na mkewe watapata mwana. Alisema, ***"…Basi sasa hayo***

***nayo maneno yako yatakapotimia, je! Huyo mtoto atakuwa wa namna gani, na kazi yake itakuwa ni nini?"*** (Waamuzi 13:12). Alitafakari maisha ya baadaye ya mwanawe hata kabla hajazaliwa.

Mungu anawaambia wazazi, ***"Mlee mtoto katika njia impasayo"*** na ***"…waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana."*** (Mithali 22:6; Waefeso 6:4). Ni jambo lenye maana kwamba Biblia inakazia ukweli kwamba wazazi, na si wengine, wanawajibu wa ***"kulea"*** *na* ***"kuwaadabisha"*** watoto wao katika njia sahihi. Hawawezi kugawa majukumu yao kwa wengine, wala kuanza kuwafundisha watoto wao wakati wamepevuka. Tangu wakiwa wadogo, na maadamu wako chini ya uangalizi wa wazazi, wazazi wanawajibika. **Ni mchakato endelevu.** Wazazi hawawezi **kuwatenga** watoto wao na majaribu, lakini wanaweza kuwasaidia **kuwahami** na dhambi. Hiyo ndiyo sababu majukumu ya wazazi yanaanza wakati watoto wakiwa wadogo.

Ili kuwa na uhakika, ni muhimu wazazi wakachukua uangalifu wa mahitaji ya kimwili ya watoto, lakini si hadi katika anga za roho zao. Je, mtoto anaona ni wapi wazazi wake wanapoweka mkazo zaidi? Je, ni katika mambo ya kimwili, au katika mambo ya kiroho? Kile mzazi anachomfundisha mtoto, kwa maneno na vitendo, ndivyo hasa mtoto atakavyokuwa na kufundisha watoto wake mwenyewe. Kama mkazo upo katika mwili, basi tusitarajie mtoto huyo kupigana ***"vita vizuri vya imani"*** atakapokabiliana na majaribu. Kristo alisema, ***"Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu;.."*** na "***Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake?.."*** (Mathayo 6:24; 16:26).

Wazazi,hakuna kilichomuhimu kuliko roho ya mtoto wako, **kwa maana yenyewe ndiyo pekee ya umilele.** Ikiwa watoto wako wamekufa kwa njaa na kupata uzima wa milele, utakuwa umefanikiwa sana. Kwa maneno mengine, kama watoto wako wanakilakitu ambavyo vinapatikana katika maisha haya na wakaangamia katika Siku ya Hukumu, maisha yao yatakuwa yameshindwa kwa huzuni.

Hiyo ndiyo sababu **wazazi hawapaswi kusahau umuhimu wa malezi ya nyumbani.**

**Ferman Carpenter ni mhubiri wa Kanisa la Kristo Westside huko Round Rock, Texas, Marekani.**

# Urithi Bora!

**Dwight Fuqua**

Zakaria na Elisabeti, wazazi wa Yohana Mbatizaji, walielezewa namna hii, (Luka 1:5). Yohana alibarikiwa kuwapata wazazi watauwa namna ile!



Wazazi watauwa kweli ni baraka! Wale walio na wazazi ambao wamewalea ***"katika adabu na maonyo ya Bwana"*** (Waefeso 6:4) wamepata mengi ambayo kwayo wanapaswa kushukuru! urithi mzuri kiasi gani!

Unatamani mzazi mtauwa? Neno la Mungu linafanya hivyo kwa ajili yetu.

- Wazazi watauwa wanatembea katika njia ya Bwana na ***"kuwaamuru"*** watoto wao wawafuate (Mwanzo 18:19).
- Wazazi watauwa ***"wanawajulisha watoto wao kweli ya Mungu"*** (Isaya 38:19).
- Wazazi watauwa ***"huwaonya"*** watoto wao (1 Wathesalonike 2:11).
- Wazazi watauwa ***"huwarudi"*** watoto wao katika njia iwapasayo kwenda (Waebrania 12:7).

- Wazazi watauwa ***"wanawalea"*** watoto wao katika njia iwapasayo (Mithali 22:6).

Baadhi ya maelekezo yenye utajiri sana katika Biblia kwa wazazi yanapatikana katika maonyo ya Musa katika Kumbukumbu la Torati 6:4-9. Musa aliandika:

> ***"Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja. Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako. Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako."***

Ngoja tufupishe.

- Wazazi watauwa wanampenda Mungu kwa uhalisia (mist 4-6).
- Wazazi watauwa wanajitoa kwa watoto wao na kuwafundisha kwa ***"bidii"*** njia ya Bwana (mst 7).
- Wazazi watauwa wanailinda imani kwa uwazi na kuiishi (mist 8-9).

Sulemani aliandika ***"Mtu mwema huawaachia wana wa wanawe urithi;.."*** (Mithali 13:22). Sio urithi wa kimwili. Ni urithi wa imani. Ah, ni urithi mzuri kiasi gani!

**Dwight Fuqua anahubiri katika kanisa la Kristo Findlay huko Sparta, Tennessee, Marekani.**



# Dakika - 5 Za Kujifunza Biblia

**Paula Bates**

# Ukiri

1. Kwa maana kwa………..mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa…………..hata kupata……………. Warumi 10:10.
2. Ungameni…………………zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa………….. Yakobo 5:16.
3. Walakini hata katika wakuu walikuwamo wengi…………………..; lakini kwa sababu ya……………………., ……………………., wasije wakatengwa na sinagogi.. Yohana 12:42.
4. Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe, wala………………. kamwe jina lake katika………….. cha uzima, nami………………. jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika zake. Ufunuo 3:5
5. na kila…………..ukiri ya kuwa..........................NI …………., kwa utukufu wa Mungu Baba. Wafilipi 2:11.
6. Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni……………………….na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu……….. 1 Yohana 1:9.

Majibu:

1. Moyo, ukiri, wokovu
2. Dhambi, bidii
3. Waliomwamini, Mafarisayo, hawakumkir
4. Sitalifuta, kitabu, nitalikiri
5. Ulimi, Yesu Kristo, Bwana
6. mwaminifu, wote

# Waefeso: Kristo na Kanisa Lake

**Jim Laws**



Efeso ulikuwa mji muhimu, ambao ulijigamba kwa kuwa mlinzi wa Hekalu la Diana, moja kati ya maajabu saba ya ulimwengu wa kale. Mji ulijitoa katika ibada za sanamu. Katika kipindi cha safari yake ya pili ya umisheni, Paulo alitembelea Efeso na kuwaacha huko Akila na Prisila (Mdo 18:19-21). Alirudi Efeso miaka miwili baadaye na kuhudumu kwa miaka mitatu, akiyafikia majimbo yote ya Asia kwa Injli (Mdo 19). Miaka kadhaa baadaye, akiwa mfungwa kule Rumi, Paulo aliandika waraka kwa ndugu wa Efeso (Warumi 3:1; 4:1). Kwa kweli, kuna nyaraka nne za gerezani; Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, na Filemoni.

Soma pamoja nami katika kitabu hiki kizuri cha Agano Jipya, Waefeso, angalia jinsi Paulo alivyoandika kuhusiana na, fundisho (sura 1-3) na, wajibu (sura 4-6). Waefeso inajulikana kama waraka mkuu katika nyaraka za Paulo; wengine wameenda mbali zaidi hata kusema “Korongo Kuu la Maandiko”.

# Waefeso 1

Paulo anapanua fundisho la wokovu kwa neema ya Mungu, ambao Baba aliupanga (1:1-4), Mwana alinunua (1:7-12) na Roho alifunua (1:13-114). Maombi yake (1:15-23) akielezea shauku yake kwamba watakatifu wafikie kujua jambo fulani la kiwango cha baraka zetu katika Kristo. Ni kweli wokovu unatoka kwa Mungu na unapatikana kwa watu wote ambao wanamtii Yeye (Waebrania 5:8-9).

# Waefeso 2

Paulo aliandika kwamba Wakristo wa Efeso kwanza walikuwa wamekufa katika dhambi zao, lakini kwa sababu ya utiifu wao wa imani, walikuwa hai katika Kristo. Maisha haya mapya katika Kristo yanamweka mtu huru mbali na kifungo cha dhambi (2:1-3). Katika Yesu Kristo, wote Wayahudi na Mataifa sasa ni mmoja tangu kiambaza kilipoondolewa. Waamini ni washirika wa mwili mmoja, raia wa taifa moja takatifu na mawe yaliyo hai katika hekalu moja (1 Petro 2:1-10). Baraka hizi zote ni matokeo ya rehema na upendo wa Mungu.

# Waefeso 3

Kwa sababu hii, Kristo alijenga kanisa lake (Mathayo 16:18). Kanisa lake ni kwa ajili ya wote watakaomgeukia kwa kutii ujumbe wa Injili yake. Mungu aliipa kibali kazi kubwa ya Paulo kuhubiri habari njema kwa Wayahudi na kwa Mataifa ili kwamba makundi yote mawili yaweze kuwa sehemu ya kanisa moja, kutimiza mpango wa Mungu wa umilele.

# Waefeso 4

Wakristo wote ni mmoja katika Kristo Yesu (Wagalatia 3:28), lakini ni lazima tufanye kazi kuunda umoja wa roho katika uhalisia wa maisha yetu ya kila siku. Umoja utajenga kanisa; utengano, ni kazi ya Shetani, utaliharibu kanisa (4:1-13). Paulo anakazia kwamba kama ilivyo kuna ulazima wa kuzaliwa kiroho, hapo pia, lazima kuwe na ukuaji kama tunataka kufanana na Yesu (1 Petro 1:22-2:3). Kwa sababu tunakua

kiroho, tunaelewa uhitaji wa kuongea ukweli katika upendo (4:15) na kuishi maisha ya uwajibikaji kwa wengine (4:17-32).

## Waefeso 5

Katika sura hii, Paulo anakumbusha kuhusu dhabihu ya Yesu, ambayo inapaswa itusukume kuishi vizuri mbele zake (5:1-7). Anatupeleka katika shamba na kutukumbusha kwamba kutembea nuruni kutazaa tunda la Roho (5:8-14; Wagalatia 6:14-18). Anatuchukua hadi katika maeneo ya sokoni, akituambia tuwe wafanyabiashara wazuri kwa kununua kila fursa kutenda wema na kutembea kwa hekima (5:15-17). Mwisho, anatupeleka nyumbani, ambapo anatumia ndoa kama picha ya mahusiano yetu na Kristo (5:23-32).

## Waefeso 6

Mtoto wa Mungu ambaye anauishi ujumbe wa Agano Jipya katika maisha yake ataonesha "Taswira ya Kristo" nyumbani, kazini, shuleni na hata katika uwanja wa mapambano katika maisha. Kama watoto hawajifunzi kutii nyumbani, hawawezi kuitii mamlaka nyingine yo yote ya nje. Wazazi Wakristo lazima wawaandae watoto wao kukabiliana na adui yetu wa siku zote Shetani. katika uwanja wo wote wa vita katika maisha. Kama sisi sote tutamzingatia adui yetu, wala hatuthubutu kupuuzia ***"kuzivaa silaha zote za Mungu"*** katika maandalizi ya vita vya kiroho vilivyo mbele yetu. Kwa hiyo, ilinde nafsi yako kwa Neno la Mungu, na umshinde adui yako.

**Jim Laws ni mhubiri wa Kanisa la Kristo Broadway huko Tyler, Texas, Marekani.**

**Je, Ulijua?** Tunapaswa kuvaa silaha zote za Mungu (Waefeso 6:11), sio baadhi. Neno la Kigiriki silaha ni *panoply.* Neno "simama" linaashiria kusimama wima. Tunatakiwa kusimama wima dhidi ya Shetani. ***"Hila za Shetani"*** inamaanisha njia anazotumia kutujaribu ili tumfuate yeye na kumwacha Mungu. 1 Yohana 2:16 anazungumzia kuhusu tamaa ya mwili, tamaa ya macho na kiburi cha uzima. Hizi ndizo njia tatu Shetani anazotumia kutunasa ili tumwache Mungu. Kila jaribu tunalokabiliana nalo linaangukia katika moja ya njia hizo. Yakobo 1:13-15 inaelezea zaidi jinsi hili linavyotendeka. Shetani anatuwekea mbele yetu vitu vya ulimwengu huu tunavyovitaka. Tunapoingia na kushiriki, jaribu linabadilika na kuwa tendo la dhambi na dhambi isiyotubiwa inapelekea mauti ya kiroho. Silaha tunazotakiwa kuzivaa zinatusaidia kutulinda dhidi ya mbinu za Shetani.

# *Injili ya Marko*

**David Shannon**

Katika Injili ya Marko, neno ***"Mara"*** linaonekana likitumiwa na Marko mara nyingi. Tuangalie mifano michache.

**Marko 1:20** "***Mara akawaita, wakamwacha baba yao Zebedayo ndani ya chombo pamoja na watu wa mshahara, wakaenda, wakamfuata."*** Yesu anashauku tumfuate Yeye maramoja (haraka).



**Marko 1:21 "*Wakashika njia mpaka Kapernaumu, na mara siku ya sabato akaingia katika sinagogi, akafundish."*** .Wakati Yesu alipopata fursa ya kufundisha, maramoja aliitumia fursa hiyo.

**Marko 2:8** "***Mara Yesu akafahamu rohoni mwake kwamba wanafikiri hivyo nafsini mwao, akawaambia, Mbona mnafikiri hivi mioyoni mwenu?"*** Yesu anajua mioyo yetu kwa haraka. Wengi hujua pekee matendo yetu au maneno, lakini Yesu anajua moyo (mawazo)! Je, anauonaje moyo wako?

**Marko 3:6** "***Mara** wakatoka wale Mafarisayo, wakawa wakifanya shauri juu yake pamoja na Maherodi, jinsi ya kumwangamiza."* Mafarisayo walichukia uvunjaji wa Yesu wa utamaduni wao wa Sabato. Walimwona akiponya katika siku ya Sababto na mara wakaamua kumwua! Wakati mafundisho ya Yesu yanapohalifu matendo yetu, mawazo au tamaduni, nini itakuwa mwitikio wetu wa haraka?

**Marko 4:15** "***Hawa ndio walio kando ya njia lipandwapo neno; nao, wakiisha kusikia, mara huja Shetani, akaliondoa lile neno lililopandwa mioyoni mwao."*** Baadhi wanasikia hotuba na kusoma kifungu cha Maandiko, lakini wanasahau kwa haraka sana badala ya kuweka katika moyo na kulitumia (Marko 4:24). Wengine wanalikubali Neno la Mungu, lakini wanaruhusu mali kulitoa nje Neno hilo na ***"mara wanajikwaa"*** (Marko 4:17).

**Marko 9:24** "***Mara babaye yule kijana akapaza sauti, akasema, Naamini, nisaidie kutokuamini kwangu."*** Baba wa kijana mwenye kifafa alitafuta uponyaji wa Yesu. Yesu alielezea umuhimu wa imani. Unyenyekevu wa baba na shauku yake kwa Bwana ili amsaidie kukua akajibu kwa haraka ***"nisaidie kutokuamini kwangu!"*** tulifanye hili kuwa maombi yetu kwa bidii.

Je, matendo yako ya haraka, maneno na mawazo ya moyo yanamtegemea Mungu? **Na tumtumikie Yeye haraka! Usisubiri!**

**David Shannon ni mhubiri wa Kanisa la Kristo Mt. Juliet huko Mt. Juliet, Tennessee, Marekani.**

## Je, Ulijua?

Ustaarabu wa Sumer (eneo lililopo kusini mwa Babeli au Iraq ya leo), lipo baina ya mito Tigris na Frati karibu na Ghuba ya Umedi takribani km 3000, ndilo lililowajibika kwa kutoa nambari za mfumo tunaotumia kwa muda, na kwa kupimia mzunguko (sexagesimal system). Mfumo huu unategemea namba 60.




# Mwokoteza Mawindo

**kitabu cha Yakobo**

**(Majibu ndani ya gamba la nyuma)**

1. Kitabu cha Yakobo waliandikiwa wakina nani?
2. Hisia gani wanayopaswa Wakristo kuwa nayo wakati wanapoyakabili majiribu?
3. Nini kinachofanya dini ya mtu isiwe na maana?
4. Nini kinacholeta furaha juu ya hukumu?
5. Ni nani aliyeitwa rafiki wa Mungu?
6. Taja vitu viwili vikubwa ambavyo Yakobo anasema vinatawaliwa na kitu kidogo.
7. Ni yupi ambaye Mungu anampa neema?
8. Maisha yanalinganishwa na kitu gani?
9. Aina gani ya maombi yanayofaa sana?
10. Wataje watu wanne katika Agano la Kale waliotumiwa kama mfano na Yakobo.

# Jifunze kwa Mtu Mwema.



**Maxie B. Boren**

Inafurahisha kutoka muda hadi muda kusisitiza umuhimu na kuzungumza kuhusu marafiki wema na mambo mazuri waliyoyafanya. Inaonekana kana kwamba tunasikia sana kuhusu ubaya lakini si sana kuhusu wema. Tunahitaji kubadili hilo.

Mtu mmoja tangu muda mrefu uliopita ambaye daima amekuwa chati ya kielelezo cha juu alikuwa ni mvulana mfalme Yosia. Alianza utawala wake akiwa na umri wa miaka 8 na akaendelea katika mamlaka hayo kwa miaka 31. Alikuwa mfalme wa 16 wa Yuda, kutoka takribani mwaka wa 640 hadi 610 K.K. Biblia inatuambia "***Akafanya yaliyo mema machoni pa Bwana, akaziendea njia za Daudi babaye, asigeuke kwa kuume wala kwa kushoto.***" (2 Mambo ya nyakati 34:2). **Moyo wake ulikuwa mnyenyekevu,** na alikuwa mnyenyekevu mbele za Mungu (aya ya 19). Nakumbushwa na vifungu viwili; ***"Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako,.."*** (Mhubiri 12:1) na "***Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari,.."*** (1 Petro 5:6).

Kwa sababu ya unyenyekevu wake wa kumtafuta Mungu, (1) alirudisha upya sharti la kushika agano la Mungu, (2) alitokomeza sanamu, (3) alizivunja nyumba za wasodoma na (4) aliwaondoa wachawi na, wenye pepo n.k. (2 Wafalme 23:1-7, 24). "***Kabla ya huyo hapakuwa na mfalme mfano wake, aliyemwelekea Bwana kwa moyo wake wote, na kwa roho yake yote, na kwa nguvu zake zote,..***" (2 Wafalme 23:25).

**Maxie B. Boren (1954-2016) alikuwa mhubiri wa Injili na mzee katikakusanyiko la Brown Trail huko Bedford, Texas, Marekani.**

# Mwuaji wa Jitu Karibia Auawe

**Steve Higginbotham**



2 Samweli 21:15-17 inaleza kuhusu jitu kwa jina *Ishi-benobu*. Aliingia katika mapigano na mwanaume mwingine. Kumbukumbu inasema kwamba mpinzani wa Ishi-benobu ***"akaishiwa na nguvu"*** na angeweza kuuawa kama isingekuwa mmoja wa watumishi wake waaminifu ambaye alikuja kumwokoa na kumwua yule mnefili (jitu).

Kwa mshtuko mkubwa, mpinzani wa Ishi-benobu alikuwa Mfalme Daudi. Huyu ni Daudi yule yule aliyemwua jitu la kutisha Goliati. Hata hivyo, katika tukio hili, mnefili alifanikiwa kumshinda Daudi na alikaribia kumwua. Ebu tuchunguze baadhi ya mambo ya kiroho ambayo tunaweza kuyapata katika habari hii.

**Hatuwezi kuishi katika mafanikio yaliyopita.** Daudi mara moja

alifahamika kama **mwuaji mkuu wa mnefili (jitu),** lakini hili halikumsaidia kabisa katika wakati wake huu wa sasa vitani. Vivyo hivyo, Shetani hashangazwi na hadhi zetu. Tunaweza kuwa na hadhi ya kuwa mzee mtauwa, mhubiri, mwalimu wa darasa la Biblia au Mkristo na bado, hadhi zetu pekee hazitatusaidia katika vita vyetu vya kila siku na Shetani. Shetani hatishwi na mafanikio yetu ya nyuma. Kumbuka, alithubutu hata kumjaribu Mwana wa Mungu (Luka 4).

**Shetani hasalimu amri baada ya kushindwa mara moja.** Ingawa Daudi alimshinda mnefili mmoja, alifanya vita na wanefili zaidi baadaye. Kwa muda, tunaweza kumshinda vibaya Shetani, lakini tusijidanganye wenyewe kwa kudhani kwamba tumeona mwisho wake. Shetani anaelezewa kama simba mwenye njaa, angurumaye. Kwa hiyo, tunaweza kuwa na uhakika atatushambulia tena (1 Petro 5:8).

**Sote tunahitaji msaada kwa muda fulani.** Ingawa Daudi alikuwa shujaa mwuaji wa jitu, alihitaji msaada katika vita husika. Haijalishi sisi ni wakina nani au kazi gani tunafanya ndani ya mwili wa Kristo, sisi sote, kwa muda, tunahitaji msaada wa wengine. Daudi alibahatika sana kuwa na mtu pale wa kumsaidia. Tunahitaji kuwa tayari kukubali au kutoa msaada wakati unapohitajika (Wagalatia 6:2)

**Majukumu yetu wakati mwingine yanabadilika.** Wakati askari wa Daudi walipoona kwamba alikaribia kuuawa, walimfanya ahaidi kutojihusisha tena na vita ili **asije kuizima taa ya Israeli.** Daudi hakuwa tena shujaa ambaye mwanzo alikuwa, lakini Israeli bado iliendelea kumhitaji. Daudi alihitaji kubadili nafasi yake ya utumishi. Vivyo hivyo, wakati utakuja ambao tunahitaji kutambua kwamba hatuna uwezo wa kutumika katika kanisa la Bwana katika uwezo ule ambao tulikuwa nao kwanza. Hii haimaanishi kwamba tuweke nafsi zetu katika kabati, bali tunapaswa kuhamisha eneo letu la huduma. Kamwe hatuwezi kuziondoa tabia zetu zinazofaa katika kanisa la Kristo (1 Wakorintho 12:12-31).

Mungu atusaidie kutambua kwamba sisi sote tutakuwa na majitu ya kuyaua. Natumaini, mada za hapo juu zitatusaidia kuwaua wanefili

ambao wanatukabili katika maisha yetu yote. Viongozi ni wauaji wa wanefili!


**Steve Higginbotham ni mhubiri wa Kanisa la Kristo Karns huko Knoxville, Tennessee, Marekani.**




***"Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho."*** (Wagalatia 6:9). Majaribu ya kuacha kazi njema yamewahi kuwasumbua binadamu. Shetani daima amekuwa akijulikana kwamba ni mwepesi na njia ya hakika kusimamisha kazi njema kwa kuwakatisha tamaa watenda kazi. Adui yetu kama ***"simba angurumaye…akitafuta mtu ammeze."*** (1 Petro 5:8), akipendezwa katika kufunika tumaini lo lote linaloangaza kwa wingu la giza la shaka na kushindwa.

Mfano mzuri wa Biblia ambao mtu aliyeshinda majaribu ya Shetani ili aache kazi yenye thamani unapatikana katika Agano la Kale kuhusu Nehemia. Hakufanya kazi kwa muda mrefu kuujenga upya ukuta wa Yerusalemu kabla Sanibalati, Tobia na Geshemu, maadui wa watu wa Mungu, kusikia na kuanza uhamasishaji wa nguvu kuisimamisha kazi. Mwanzoni, waliukejeli mradi. Tobia aliupuuza ukuta kwa kuwa ni dahifu kwamba ungeweza kubomoka kwa uzito wa mbweha (Nehemia 4:3). Pamoja na hayo, kazi bado iliendelea. Hawa maadui baadaye ***"wakafanya shauri wote pamoja kuja kupigana na Yerusalemu, na kufanya machafuko humo."*** lakini kazi bado iliendelea kwa watenda kazi kushikilia kifaa mkono mmoja na silaha mkono mwingine (4:8,17). Sanbalati na Geshemu walimjaribu Nehemia achukue mapumziko ya kazi ili akutane nao katika eneo tambarare ya Ono wazungumze tena

kuhusu jambo hilo, lakini mwaliko ulikataliwa na kazi ikaendelea (6:1-4). Hatimaye, uvumi wa ubaya na uongo ulizunguka katika juhudi za kudhoofisha kazi na nia iliyokuwa nyuma yake (6:5-9). Pamoja na hayo,




kazi iliendelea, na ukuta ulimalizika katika siku 52 (6:15).

Nini funguo za mafanikio ya Nehemia? Miungoni mwa wengine, angalia hizi. Kwanza, ***“wakaitia mikono yao nguvu kwa kazi hiyo njema.”*** Wakiamini kwamba Mungu angewasaidia (2:18,20). Pili, ***“watu walikuwa na moyo wa kufanya kazi.”*** (4:6). Kwa sababu kazi ilionekana kama ni kuu kuliko wafanyakazi na kwa sababu ilionekana kama kazi ya Mungu iliyokuwa ikisaidiwa na Mungu, raia wenza wa Nehemia, ***“walikuwa na moyo wa kufanya kazi.”*** Hivyo, hawakuweza kukatishwa tamaa wala kuzuiwa.

Shetani alikutana na ukuta wa tofali alipokwenda kinyume cha Nehemia na watenda kazi wake. Naomba ukweli huo wa juhudi zake uwe kweli katika mambo yaliyo kinyume cha kazi zetu njema kama tunavyofanya kazi kwa Bwana wetu leo.

**Dalton Key ni mhariri wa Old Paths (Njia za Kale) na mhubiri wa kusanyiko la 10th na Rockford huko Tulsa, Oklahoma, Marekani.**

# Mungu Aliwaacha Kivipi?

**Dennis Gulledge**

Katika Warumi 1, inasemwa kwa watu wasio watauwa kwamba ***"Mungu aliwaacha katika tamaa za mioyo yao, waufuate uchafu"*** (mst. 24), ***"Mungu aliwaacha wafuate tamaa zao za aibu"*** (mst. 26) na ***"Mungu aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa"*** (mst. 28). Haya maelezo yanamaanisha nini? Kirai ***"aliwaacha"*** kinatoka katika neno la Kigiriki linalomaasha kutelekeza, kuacha katika mikono ya mwingine, kuacha katika nguvu za mwingine atumie. Nini Mungu anachofanya, au asichofanya, pindi hili linapotokea? Vifungu vifuatavyo vinatoa shauku kubwa ya utambuzi.

**Waefeso 4:17-19,** Paulo alitumia wazo sawa ambalo alilitumia katika Warumi 1:24, 26, 28 kuelezea kile watu wanachofanya kujitoa maisha yao katika maisha ya dhambi. Mataifa walikuwa sugu na kutojali, kujitoa katika uchu wa tamaa. Kitu Mungu anachofanya, sisi pia tunaweza kujifanyia wenyewe.

**Hosea 4:16-19.** Mungu aliwaacha Waisraeli kwa sababu walijiunga na sanamu kiasi kwamba kujaribu kuwarejesha tena haikuzaa matunda. Baadhi ya watu wanafikia kiasi kwamba hawawezi (hawataki) kutubu. Mungu alimwambia nabii, ***"mwache mwenyewe".*** Je, kuna hatua katika hali ya kiroho ambayo ni potofu ambapo haizai matunda kujaribu kuwafikia kwa Injili? Je, kuna hatua ambapo tunatakiwa kuwaacha wenyewe (Mathayo 7:6)?

**Zaburi 81:11-16.** Katika kuwaacha watu wake wafuate tamaa za mioyo yao wenyewe, Mungu alifanya nini au kutofanya? Alijiondoa kutoka kwao, ulinzi wake na nguvu ya uongozi wake. Angeweza kuwatiisha maadui zao, lakini hakufanya hivyo (mst. 14). Angeweza kuwa na ushawishi dhidi ya washitaki wao kama vile kuwaweka katika ghuba maadamu Israeli angekuwa mtiifu Kwake (mst. 15). Angewabariki kwa mafanikio (mst. 16). Je, anakana majaaliwa ya baraka zake kwa watu wale ambao wako kinyume chake?



**Mdo 7:39-43.** Stefano alielezea uzinifu wa Israeli tangu wakiwa jangwani mpaka kuchukuliwa Babeli. Ibada yao kamili ya ***"jeshi la mbinguni"*** imeelezewa katika Amosi 5:25-27. Yalikuwa ni matokeo kwa tabia yao ya kumwasi Mungu. Ilikuwa ni kilele cha mchakato wa uzinzi waliouanza katika jangwa la Yudea. Pindi upotofu unapoanza, hakuna nafasi kwa aliyerudi nyuma kuacha. Mungu ataliacha hilo liende bila kukoma.

**Ezekieli 20:25-26.** Mungu aliwatawanya watu wake katika mataifa ya watu wasiomjua Mungu (mst. 23). Israeli alijihisi kwamba alistahili Nchi ya Ahadi na kwamba Mungu asingeweza kuwaacha watu wake bila ya kujali nini watafanya. Kwa kadili Israeli alivyozama katika uzinzi, Waisraeli walijikuta wakitumikia dini ambazo zilikuwa za kipagani na mfu. Neno la Kiebrania ***"-acha"*** (*Nathan)* ni sentesi ya kimahakama iliyopita juu ya Israeli kwa uzinifu wao. Hii ni zaidi ya Mungu kuwaruhusu waende njia hiyo. Ni mfano wa ***"nguvu ya upotevu"*** na kuamini uongo ambao Paulo alionya katika 2 Wathesalonike 2:10-12. Israeli hawakuacha uzinifu na walipelekwa ndani zaidi katika nguvu ya uzinifu, **hata kiasi cha kutoa kafara ya mtoto.** Hapa ndipo tulipo leo? Pale watoa sheria wetu walipotelekeza mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha matakatifu, **tumeenda mbali sana hata kuua watoto wetu ambao hawajazaliwa (mimba).**

**Dennis Gulledge ni mhubiri wa Kanisa la Kristo huko Mabelvale, Arkansas, Marekani.**

# Amri Kumi na Agano Jipya

**Russell Bell**



**Swali:** "Tafadhali unaweza kunipatia vifungu vya Biblia kwa ajili ya amri nyingine tisa?" **Jibu:** "Katika makala iliyopita, nilizitaja hizo tisa za Amri Kumi halisi zilizotajwa katika Agano Jipya,isipokuwa amri ya nne. "Ikumbuke siku ya Sabato uitakase," haikuwemo katika Agano Jipya. Bila shaka msomaji aligundua kutokuwepo kwa amri ya Sabato katika Agano Jipya na kujiuliza kama tisa zingine hazikuwemo. Jibu ni, "Hapana," hizi hapa ni amri tisa kati ya Amri Kumi katika Agano Jipya. Hizi sheria za Agano la Kale zilizoletwa katika Agano Jipya si zote zilizoandikwa neno kwa neno, lakini fundisho linaloeleweka kuhusu hizo lipo.

1. Hapana Mungu mwingine (Kutoka 20:4)
   ***"Basi kwa habari ya kuvila vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu; twajua ya kuwa sanamu si kitu katika ulimwengu, na ya kuwa hakuna Mungu ila mmoja tu. Kwa maana ijapokuwa wako waitwao miungu, ama mbinguni ama duniani, kama vile walivyoko miungu mingi na mabwana wengi; lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake; yuko na Bwana mmoja Yesu Kristo,***

***ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo, na sisi kwa yeye huyo."*** (1 Wakorintho 8:4-6).

2. Hapana kuchonga sanamu (Kutoka 20:4).
***"Kwa ajili ya hayo, wapenzi wangu, ikimbieni ibada ya sanamu***." (1 Wakorintho 10:14).

3. Usilitaje bure jina la Bwana (Kutoka 20:7).
***"Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje,"*** (Mathayo 6:9).

***"Neno lo lote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia."*** (Waefeso 4:29).

4. Ikumbuke Sabato uitakase (Kutoka 20:8).
Hakuna amri, agizo au mfano katika sheria ya Agano Jipya kwa mtu kuishika Sabato. Amri hii iliondolewa kabisa katika Agano Jipya la Kristo. Siku ya Bwana, siku ya kwanza ya juma, ilitolewa ishikwe (Mdo 20:7; 1 Wakorintho 16:1-2).

5. Waheshimu baba na mama (Kutoka 20:12).
***"Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi,"*** (Waefeso 6:1-2).

6. Usiue (Kutoka 20:13).
***"Maana mtu wa kwenu asiteswe kama mwuaji, au mwivi, au mtenda mabaya, au kama mtu ajishughulishaye na mambo ya watu wengine."*** (1 Petro 4:15).

7. Usizini (Kutoka 20:14).
***"Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala wevi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi."*** (1 Wakorintho 6:9-10).

8. Usiibe (Kutoka 20:15).
   ***"Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji."*** (Waefeso 4:28).

9. Usishuhudie uongo (Kutoka 20:16).
   ***"Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake;"*** (Wakolosai 3:9).

10. Usitamani (Kutoka 20:17).
    ***"Maana neno hili mnalijua hakika, ya kwamba hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu, aliye na urithi katika ufalme wa Kristo na Mungu."*** (Waefeso 5:5).

**[Maelezo ya Mhariri:** angalau hivi vifungu vya Agano Jipya vimehalalisha uthibitisho kwamba tisa kati ya Amri Kumi halisi zimerejeshwa katika Agano Jipya. Bila shaka, orodha ingeweza kupanuliwa pamoja na nyongeza ya rejea ndani ya Agano Jipya. Mwisho, watu wa sasa wanalazimika kutekeleza amri zile tisa, si kwa sababu zilikuwa katika Agano la Kale, ila kwa sababu zipo katika Agano Jipya ambalo tupo chini yake na kwalo tutahukimiwa siku moja. ~ Louis Rushmore, Mhariri].

**Russell Bell ni mhubiri wa Injili na mmisionari wa kigeni ambaye anaishi huko Topeka, Kansas, Marekani.**

# NINI KILICHO SAHIHI KWA KANISA?

**Mark N. Posey**



**Utangulizi:**

Pale watu wenye dhambi wanapojaribu kulidhuru kanisa, inamuumiza Kristo na watu wake (Mdo 9:4; Mathayo 25:45). Pamoja na hayo, usivunjike moyo. Kanisa ni sahihi sana haliwezi kuwa si sahihi, kwa sababu limejengwa na kuanzishwa na Yesu Kristo (Mathayo 16:18; 1 Wakorintho 3:11). Zingatia baadhi ya sababu kwanini kanisa ni sahihi! Kanisa ni sahihi kwa sababu…

1. **GHARAMA ilikuwa sahihi!**
   - Gharama iliyolipwa kwa ajili ya kanisa ilikuwa kifo cha Mwana pekee wa Mungu juu ya msalaba wa kikatili kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu. WIMBO: "Yesu alilipa yote, yote ananidai; dhambi iliacha doa kwenye bendera, Aliisafisha ikawa nyeupe kama theruji" (1 Wakorintho 6:19-20; 1 Petro 1:18-19).

- Paulo alisema Bwana wetu "alinunua kanisa kwa damu yake mwenyewe" (Mdo 20:28).

2. **OMBI ni sahihi!**
   - Tunaomba Maandiko yawe kikomo na sheria yenye mamlaka katika dini. Tunanena kama maagizo ya Mungu (1 Petro 4:1).
   - Tunaomba kwa ajili ya marejesho ya mfumo wa Agano Jipya katika kila jambo muhimu. Lazima turudi katika Neno la Mungu katika mambo yote muhimu, kama vile; mpango wa wokovu (Mdo 2:38; 22:16), mpango wa ibada (Mdo 20:7; 1 Timotheo 3:1-13), na mpango wa usafi wa Mkristo (Wagalatia 5:22-23; 2 Petro 1:5-8).

3. **AHADI ni sahihi!**
   - Mungu aliahidi Mbingu kwa kanisa. Yesu alisema, "***Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo.*** (Yohana 14:3).
   - Mbingu imehifadhiwa kwa ajili ya ***"waliozaliwa mara ya pili"*** (1 Petro 1:3-5).

**Hitimisho:**

Kama unalipenda kanisa kama Yesu alivyofanya, fanya liwe kipaumbele chako (Mathayo 6:33), na Bwana atakupa baraka zote za kiroho (Waefeso 1:3).

**Mark N. Posey ni mhubiri wa Kanisa la Kristo Austinville huko Decatur, Alabama, Marekani.**

**Gharama iliyolipwa kwa ajili ya kanisa ilikuwa kifo cha Mwana pekee wa Mungu juu ya msalaba wa kikatili kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu.**

# Kumsahau Mungu!

**Kifungu: Kumbukumbu la Torati 32.15-18**

**Bobby Dockery**

**Utangulizi:**

A. Usahaulifu unaweza kuwa kichekesho… au huzuni!
B. Usahaulifu ni janga kubwa ambalo linaweza kufikiriwa ni kumsahau Mungu!
C. Tutazame kwa ukaribu asili na visababishi vya hali hii ya kiroho.

**Kiini:**

**I. Kumsahau Mungu ipo katika moyo wa kila dhambi.**

A. Dhambi zote, na aibu yake na kuvunjika moyo, shina ni kumsahau Mungu!
   1. Ubinafsi ni kumsahau Mungu katika shughuli zetu na wengine (Mathayo 25:45).
   2. Kiburi ni kumsahau Mungu katika kujikadilia wenyewe (Luka 18).
   3. Wasiwasi ni kusahau majaaliwa ya Mungu (Wafilipi 4:6).
   4. Wivu ni kusahau neema na baraka za Mungu (Zaburi 103:1-5).

B. Dhambi gani tunayoweza kuitaja ambayo shina lake si kumsahau Mungu?

**II. Kwanini watu wanamsahau Mungu?**

A. Inaonekana haieleweki kwamba watu wangeweza kumsahau Mungu (Isaya 1:3; Yeremia 2:32).
B. Kwanini hili linatokea?
   1. Kwa sababu ya mafanikio (Kumbukumbu la Torati 32:15).
   2. Kwa sababu dhamiri yenye hatia haipendi kumhifadhi Mungu katika mawazo yake (Yohana 3:20).
   3. Kwa sababu dunia ni adui wa Baba (1 Yohana 2:15).

**III. Kuna njia nyingi tunazoweza kuwa na hatia ya kumsahau Mungu.**

A. Baadhi yao ni zipi?

1. Pindi tunapokuwa si watu wa shukrani (Warumi 1:21).
2. Pindi tunapomwacha Mungu nje ya mipango yetu (Yakobo 4:13-15).
3. Pindi tunapokosa muda kwa ajili ya Neno la Mungu (Hose 4:6).
4. Pindi tunapolishusha thamani kanisa la Mungu (Mdo 20:28).
5. Pindi tunaposhindwa kutimiza ahadi zetu kwa Mungu (1 Petro 3:21).

**Hitimisho:**

A. Kumsahau Mungu kunapelekea anguko la kiroho (Zaburi 9:17)!

B. Hitaji letu ni kumkumbuka Mungu kila wakati katika maisha!

**Bobby Dockery ni mwandishi na mhubiri anayeishi huko Fayetteville, Arkansas, Marekani, na amekuwa akijihusisha sana katika kazi ya umisionari kwa miaka mingi.**

**Kumsahau Mungu ipo katika moyo wa kila dhambi.**

## Je, Ulijua?

Wamisri wameelezewa katika Agano la Kale, walikuwa watu waabudu sanamu sana. Waliamini katika miungu au miungu wa kike wa anga, Mto Nile, jua, kuzaa, kifo na mambo mengine mengi. Mungu alituma mapigo kumi kumhamasisha Farao awaache watu wake waondoke katika utumwa wa Misri. Kila pigo moja lilionesha kwamba Mungu wa Mbinguni alikuwa ni mwenyenguvu sana kuliko miungu ya Misri. Mtu anaweza kusema kwamba Wamisri wa kale walimsahau Mungu wa kweli (Zaburi 9:17; Warumi 1:20-32).

# Theolojia Ya Marejesho

**Cecil May, Jr.**

Ulazima wa ubatizo kwa ajili ya ondeleo la dhambi na kwa ajili ya wokovu, Meza ya Bwana katika mkusanyiko katika Siku ya Bwana, uongozi wa wanaume katika ibada wakati wote wanaumne na wanawake wanapokuwa pamoja, na uimbaji bila ala unatofautisha makanisa ya Kristo na vikundi vingine vya kidini vilivyopo. Wengi wanazungumzia haya kama "utamaduni wa imani yetu." Kila moja nina amini, ni mamlaka ya kibiblia, na kama ni ya kibiblia na si tamaduni za kibinadamu, yamekuwa ni sehemu muhimu ya ***"utiifu wa imani"*** (Warumi 1:5; 16:26).

> "Marejesho" – "kurudi kwa kitu fulani kama awali, halisi, kawaida, au hali isioharibika; ukombozi wa kitu fulani kilichoondolewa au kupotea" *(Dictionary.com) [Kamusi].*

Ubatizo wa kibiblia ni kuzika (Warumi 6:4), ni kwa ajili ya kupokea ondoleo la dhambi (Mdo 2:38), na kumvaa Kristo (Wagalatia 3:27), ni kwa ajili ya wokovu (Marko 16:16; 1 Petro 3:21) na kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu (Mdo 2:38). Kwa kuwa hivyo, watu wanaobatizwa (isivyo kimaandiko) wanaamini kuwa tayari wameokolewa, katika kuamini huko wanakana kila kusudi la kibiblia katika ubatizo. Ikiwa hawakuzikwa na Kristo (kuzamishwa) katika ubatizo, basi hawakuwa wamebatizwa kabisa. Baadhi wanakiri kuamini yote hayo lakini bado wanaendelea kuwachukulia watu ambao hawakubatizwa kimaandiko kuwa ni Wakristo. Je, hawakani kile wanachosema kukiamini?

> "Theolojia" – "somo kuhusu mambo matakatifu au ukweli wa kidini" *(Dictionary.com) [Kamusi.com]*

Kuna fundisho la Agano Jipya la kukusanyika. Wakristo wameamriwa wasiache kukusanyika (Waebrania 10:25). Wengi hurejea mkusanyiko kama "huduma ya ibada." Wengine wanasema kwamba Biblia kamwe haijawahi kutumia msemo huo kwa mikusanyiko yetu. Kulingana na Andiko, mikusanyiko yetu ni kwa ajili ya kutiana moyo (Waebrania 10:24-25). Kipi ni sahihi au si sahihi katika mkusanyiko kunategemea kama hautujengi (1 Wakorintho 11:3-5, 17). Uimbaji wetu si ndio kumsifu kote Mungu; pia kufundisha na kuonyana (Wakolosai 3:16)?

Pamoja na hayo, kusudio hasa la kukusanyika katika Siku ya Bwana ni kushiriki Meza ya Bwana (Mdo 20:7; 1 Wakorintho 11:20), tendo ambalo bila shaka ni la ibada. Kujumuisha, sala, kuimba, kuhubiri Neno la Bwana na matoleo haya yote ni matendo ya ibada yanayofanyika katika Siku ya mkusanyiko wa Bwana (1 Wakorintho 14:15; 16:2). Kukusanyika ndio wakati pekee Wakristo wanapoabudu, na inawezekana kuwa katika mkusanyiko na kufanya yote kwa hisia sahihi lakini isiwe ni ibada. Mioyo yetu na akili lazima zihusike vizuri, na maisha yetu ya kila siku lazima yaendane na imani yetu. Hiyo ndiyo sababu George Bailey alisema, "Kuketi kanisani, ibadani, hakukufanyi wewe kuwa Mkristo, kama kukaa katika nyumba ya kuku hakukufanyi uwe kuku."

Mambo mahususi ambayo ni sahihi katika mazingira mengine hayapaswi kufanywa katika mkusanyiko. Wale waliokuwa na karama za lugha hawakuruhusiwa kutumia karama hiyo katika mkusanyiko isipokuwa kwa masharti (1 Wakorintho 14:28). Wanawake hawatakiwi Kunena wakati wa mkusanyiko (1 Wakorintho 14:33-34). Mlo wa kawaida, wa kukidhi njaa ya mtu, si sahihi katika mkusanyiko (1 Wakorintho 11:21-22). Meza ya Bwana ni kumbukumbu, mkate ni kumbukumbu ya mwili wa Kristo na mzao wa mzabibu unatuongoza kukumbuka damu yake iliyomwagika kwa ajili ya dhambi zetu ( 1 Wakorintho 11:23-26).

Imani yetu na itende kazi kwa njia ya upendo, katika mikusanyiko yetu na katika maisha yetu, katika kushukuru kwa kile Mungu

alichotufanyia kwa njia ya Kristo.

**Cecil May, Jr. ni mkuu wa kitivo mstaafu wa Chuo kikuu cha Faulkner huko Montgomery, Alabama, Marekani.**

[**Maoni ya Mhariri:** Makala hayo yanahusiana na "Theolojia ya Marejesho" kwa sababu inazungumzia mambo yanayohusu kanisa ambalo kwa ajili yake Yesu Kristo alikufa ili kulianzisha, ambalo juu yake Yeye ni kichwa, na kwa ajili yake Atarudi kulichukua na ambalo habari zake kila mtu anaweza kusoma hususani katika sehemu ya Biblia ya Agano Jipya. ~ Louis Rushmore, Mhariri]